

DAHE-speech

DAHE-speech is a corpus of Swahili speech varieties. It was recorded on C-cassettes in 1989-1991 as a joint enterprise between the University of Helsinki and the University of Dar-es-Salaam. The institutes responsible for the work were the Institute for Asian and African Studies at the University of Helsinki and the Institute of Kiswahili Research of the University of Dar-es-Salaam. The fieldwork was made possible by the grant of FINNIDA, which is part of the Ministry of Foreign Affairs, Finland.

The aim of the project was to make a survey of Swahili speech varieties in Tanzania coastal areas and on the islands of Zanzibar, Pemba, Tumbatu and Mafya.

The material was collected using two methods. In one method, speech of people was recorded in informal discussions, as well in the form of local histories, habits, and various forms of oral tradition. Along with recording the speech on tapes, a list of 620 most common words was used for finding out whether there are lexical and phonological differences between speech varieties. These two forms of data together constitute the DAHE corpus.

The original aim was that the discussions would be stored on tapes (C-cassettes) and the wordlists would be initially filled in questionnaires and then transferred to computer form.

Because the project was a joint effort of two universities, it was decided that each tape will also be copied, so that both universities get a full set of recordings. It was also decided that the original copy went to the university, from which the interviewer was, and the copy went to the other university. Therefore, each university got a fair share of the tapes.

The transcription of tapes was done partly in Dar-es-Salaam and partly in Helsinki. The final editing of the transcriptions was done in Helsinki.

Because the durability of sounds on C-cassettes is limited, it was decided that all C-cassettes will be copied on larger magnetic reels. Therefore, a Revox recorder was used for copying the cassettes on reel tapes.

However, even these reels were not the final format of the recordings. When it became feasible to convert the sound to digital form, all tapes were converted into digital form. This ensures that the quality of speech does not deteriorate over the years. The digital sound material is not yet publicly available.

Each DAHE transcript has an information section before the actual content. Each tape has usually several interviewees, and one or more interviewers. In order to ensure the anonymity of the interviewees, the real names were converted into encrypted codes. However, the identity of the interviewees is not lost. It can be recovered using the key maintained by the host of the corpus.

On the part of the interviewers, it was not considered necessary to encrypt their names.

The tapes contain mostly speech in Standard Swahili. At least the interviewers use Standard Swahili, and very often also the interviewees use the same speech variety. However, there are several speech sections, where a Swahili dialect or some other Bantu language is used. Each speech variety has its own code, shown after the name of the speech variety.

speech section of one speaker normally constitutes a single line. The line begins with three codes. First is the language code, which reveals the language used in this section. The second code is the encrypted

symbol of the speaker. In case of the interviewer, the code is an abbreviation of the name of the interviewer. The third code tells whether the speaker is a male or female. These codes can be made use of in retrieving information from the corpus.

DAHE-speech-3 starts here!

DAHE 46A

Place: Tumbatu, Chwaka

Time: 17.- 18.10.1989

Interviewee(s): 1. (BA2), 2. Unknown (XX), 3. (FJ2), 4. (WE3)

Interviewer(s): J.S. Madumulla (JM)

Recorder: Sony Professional

Language: Kitumbatu (Tu)

Topic: 1. Stories, 2. Songs

NOTICE: Incomplete! Transcription missing in between the tape. Bad transcription. Proofreader not qualified to correct obvious mistakes. Placing of quotation marks not trustworthy.

Ki JM M Habari za kutwa bibi?

Tu BA2 F Salama.

Ki JM M Tunaomba ututajie jina lako kisha uendelee kutusimulia ngano.

Tu BA2 F Jina langu Amina Ali Makame.

Ki JM M Ni mzaliwa wa hapa Tumbatu?

Tu BA2 F Unguja, Tumbatu, ee.

Ki JM M Ahaa, Hapa Chwaka.

Tu BA2 F Hapa Chwaka.

Ki JM M Ahaa, mzaliwa wa Chwaka.

Tu BA2 F Ehe.

Ki JM M Sawa. Karibu. Tupate ngano yako.

Tu BA2 F Pokwa!

Tu XX F Pokwale!

Tu BA2 F Na msile...ngoja-- Pokwa!

Tu WE3 F Pokwale.

Tu BA2 F Msile. Makame wa Makame, wakayoyana, wakatakana, Wakakayaaa, wakakayaaa, wakakayaa, wakavyaya mwana yao mmoja tu. (kicheko) Wana ... kwa Kitumbatu safi! Wapovyaya mwana yao mmoja, wakakaya kijiji chao, wakayeshi, wakayeshi, hata yule mwanababa mkewe akafa. Akakaya vyeye tu na mtoto yakwe. Haya, akaleya mwanawe akaleya mwanaye hata akona: "A'a, miye nisikale hivi tu. Madali mke wangu keshakufa na huyu mwanagu yatima. Nimwezele mamie mdogo, wakale wosi awe kama ndo

mvyazi mwezangu humu nyumbani." Akauka, akenda kutaka mchumba akalyoya. Apokwisha yoya mtoto-- mke huyo, akakaya naye, akakaya naye na veye akavyaya mtoto vile vile.

Tu BA2 F Mwanamke. Kushasikiya? Apovyaya mwanamke na veye wakakaya pale nyumbani, ueshawa na watoto wao wawili. Wakaoa, wanaleyaleya watoto wanaleyaleya wanaleyaleya, hata! Halafu, yule mkubwa, akawa kanatumwa na mama yake mdogo, kanateka chuvi, kanakwenda maji, kanajisa kula kitu pale nyumbani. Akakaya, akamleya mtoto hata akakuya. Sasa alipiga dicho yule mwana-- yule mama mtu mama mdogo. Akaona: "Ah! Miye, hela yuno hatajamkalia mwanangu, lakini huyu-- samuuya huyu. Kushasikiya? Zamwezea njia huyu nimuule, wala kitu simpi." Sasa ndo apokaya yule mwana yule mamie mdogo, siku hiyo akayanjika maji moto yanapwa- "kupwa kupwa kupwa".

Tu BA2 F Akawambiya katika kuyaya kwenu, unasikiya? Muyale leo nyoti kitanda kimoja. Akamwambia: "Aka, mbona kunatwambia ivyo na kila mtu kana kitanda chakwe." Kushasikiya?

Ki JM M Mh.

Tu BA2 F Yule mwana akadumba, akasema: "Haya." Wakakaya pale wakakaya pale, hata usiku. Yule mwana mkubwa yule mnakwambiwa ayale kitanda kimoja, akamka mashauri nduguye sasa. Akamwambia: "Mwanakwetu!" -"Labek!" -"Tushakwambiwa leo tuyale kitanda kimoja. Heya kunasikia, katika kuyaya kitanda chetu kimoja tubadilishane nguo zetu sasa. Weye ujifinge hii - yangu. Miye nichukule yako nijifinge." -"Haya kwa nini, mbona kuanambiwa hivyo?" Akamwambia: "Enhe. Ndo nimavyojiwa tu leo na mazungumzo tuzungumze ja ivyo." Wakakaya hata wakapikiwa chakulya pale, wakalya, wapokwisha kulya ku ... hata usiku pale, kanataka kuyaya kule. -"Weye sekwambia myale kitanda kimoja na mwana kwenu.

Tu BA2 F Mtizama aah. Basi gana lile lina kani hi lile." Yule mwana akauka akenda. Hata apomona kishajisita, akamwambia vile: "Tulivyokwambizana, ile nguo yako nika nijifinge uchukule yangu." Akachukuya ile yakwe, akajifinga. Apokwisha ifinga yule mwana pale, wakayaya wakayaya, hata usiku kanawasiwasi wa vile avyokwambiwa ni yule mamie mdogo. Yule bibi alikoka moto, mama mtu. Bwana hana habari nyumbani. Akayapika maji yanachemka, "Kum-kum-kum-kum-kum". Hata apofika pale, akona: "Ah! Wasiwasi mbona katulili vile. Heya kwanza nenda choyoni." Yule mwana mna wasiwasi akauka kenda zakwe choyoni yule. Hata apokuja yule mwana, hapo pale kitandani.

Tu BA2 F Na yule kajinyorosho vile vile. Hata apokuja pale akamuza: "Kuvu kwende wa?" Akamwambia: "Aka! Kunanyona nyivu nende kojoya." Sekwambia: "Vyale na mwezio usimwache wekaye." - "Aka! Tena ndo nisende choyoni?" Tena yule mwana akarudi akayaya pale heyana wasiwasi. Akayala akayala kazauka palya, "vu!" ileta ya ikafa. (?) Sasa kufa ile taya, akenda kulya akachukuya lile julya kuweka yanalyo (?) kikiri kikiri apofika kausha kibiriti, "vu!" Kuwasha kibiriti pale, yule mna wasiwasi. Akajifanya ya mnajikunja akachogea kule uwanjani, yule mwanawe kayala kelekele juyu koyoko pale, basi kaji nyuyu kun- nrefu, kanasema "ndo yule mkubwa sasa".

Tu BA2 F Sapofika akachukuya yale maji akamnyunyuriza yule mkoyo aka urefu ile kakieka keshawa ndugu! Tena ndo kanasema ndo mwana ndugu, akamnyonyuriza, churu-ruru-ru tangu ncha-- mpaka mcha yale majina ya yao ya moto. Kushavitambuya?

Ki JM M Mh.

Tu BA2 F Hapo hejitukusa tena mwana. Kushavitambuya? Kayamku kesha kufa.

Ki JM M Mh.

Tu BA2 F Akakaya yule akakaya yule, akaya njo akayamka yuaju mama mtu akafyagia akosha vyombo, akatengeneza akapika, keshakazani mana yule mwanakesha muya. "Hako tena sakaya na mwanangu weka yangu. Hata nisikia roho yangu ... nilishe na wana wa mtu nisiyejuwa."

Ki JM M Mh.

Tu BA2 F Kanahimburika kanahimburika, akapikiya chai mnyumewe akanywa apokwisha akayawa akenda zakwe. Hata akajenda funguya mlyango leka nda (?), kenda watizama tena kanamona yule mwanae kusudia kuya uyoo kanampita kwa pani, mwanawe koyoko wa jana, keshakufa! Haujeshya. Refu.

Ki JM M Endelea tu, ee.

Tu BA2 F Wakakayaa, hata wapokwisha pale, akazikiwa mtoto yakwe kakarakakara, akalia, akawa kanajipiga nachi, sasa tena alimchulia tena yule mwana. Akona: "Ah! Wewe kula mbinu ninazozifanya, hwekufa kushanikakuuya mwangu lakini sakuzogesa nyumba hii kitu sikuki. Hata nimpikile Babiye sikupi kutenda kweza kwenu ukalye. Sasa hupika vitu akajakamka mume huyu. Akauzwa:"Huyu mtoto keshapata?" Husema: "Huyo keshakulya hiyo. Mwana wa mwivu huyo." Mamiye mdogo huyo hajesha, kumbe kanamchogezea riziki sasa. -"Keje kwa huyo keshakulya uguwe huyo kana njaya hata humwiji.

Tu BA2 F Kwani cho chosi akwacho hakimtoshi." Mwana hatongoyo, kimyaaa! Kajukunju tu, kamhamidili mwenye Muungu. Akakaya akakaya, na yule bwana hataki gombana na mkewe. Akeshakwambiwa vile na veye hujinamia. Kitu kitaligwa kile, pafyagiwe, watu wakesha wamwagike wende zao. Katauka yulya mwana akalechi kaburini pa mamie alile. Alile! alile! Na kilio chakwe takwambiani. Kanasema: "Mama kiyu! Mama njaya! Mama kiyu! Mama njaya!" Katapiga udangu yule maiti kule kaburini. "Ewe mwana we! kunichimbi tangu nili duniani hata tena kuno akhera nimakofika. Heya usiumwe ni njaya wala usiumwe ni kiyu. Kunasikia?

Tu BA2 F Nenda zako msituni, ukafika babiyo kana makundi saba ya ng'ombe. Lipite lya kwaza, ukalechi ulitizame. Litapita kundi lya pili ukalechi ulitizame. Litapita kundi lya tatu ukalechi ulitizame, nyumna chuchunguliya nini? Ku ndo (?) dirishani."

Ki JM M Endelea ...

Tu BA2 F "Litapita kundi lya tatu, lipite lya nne, lipite lya tano, hata hilyo lya saba. Litapita huyo mwe awali kutapiga udangu umwite. Umwite 'Kiwamba wa kiwamba!' Katakwitika, na kwitika kwake katatenda: 'Booooooh!' Kutasema:'Kiwamba wa kiwamba funguya lango nipite.' Katachakinywa wazi mwanangu, kutenda uko kati. Ukafika huko kutenda kulya vitu."

Tu XX M Naam.

Tu BA2 F Ngoja bado.

Ki JM M Endelea.

Tu BA2 F Akasema: "Kiwamba wa kiwamba!" Aketika: "Mbooooh, Ng'ombe wa baba na mama funguya lango npite!". Tena akatenda tena: "Boooh! Yulya mwana akangiya kule kati. Akenda kurubwi. Apofika kule katika tumbo lya ng'ombe shani zakwe mwenyewe Muungu. Akoswa. Apokwishakoswa akapikiwa, akalyishwa, akezewa nguo zakwe zuri kabisa, zile-- vile vigwanda vikavuliwa, vikawikwa. Apokwisha yule ng'ombe akamwita tena: "Ng'ombe wa baba na mama!" -"Boooooh!" -"Fungua lango npite." Akafunuya kinywa "uuuf!" Akapita akenda zakwe. Mtoto apofika kwa mamiye mdogo akakayachi.

Tu BA2 F Akajamtizama yule anavyometeka yulya mtoto. "Aka! Weye baya weye, nguruwe weye jinsi zinavyofanya kule, hikidi ndo kwaza kunameteka! Kwakwenda ukalya wapi nguruwe weye. Yulya mwana hatongoyo." Kanyamaya kimya. Sasa hata apokuja yule babiye humuuza tu: "Huyu mtoto keshakulya?" - "Uyo keshakulya. Kwani angewaja ivyo? Hunamona kanameteka!" Kushasikiya? Tena hatongoyo yule baba mtu. Akaendelea akaendelea, hata apompeleleza: "Huyo kanalye wapi? Jinsi nnavyomfanyia hikidi

huyu?" Ndo kwaza kanamemeteka. Helya ... tampeleleza anakokwenda. Anakopata kulya, na koga na kufuliwa.

Tu BA2 F Kula hamfanyia mbizi huyu auke duniani, hanauka. Huyu katajanizidi huyu kama ama geni kakumzidi mwanangu."

Tu XX F...

Tu BA2 F Alikwenda, akamvulia sasa: "Huyu mbona kananawirika hivi, kanakulya wapi, kanakoga wapi?" Hajeshambizi zakwe huyu mama mtu, mdogo huyo. Huyu samfanyia pingamizi mpaka nimtambule, anapokulya na anapokoga. Sasa alikaa hata zile taimu za yulya mwana nja-- ya inamuuma, akauka zakwe tena. Pale pale papo kaburi ya mamiye, akaanguya na kiguyu cha nyuma ile kam... yule lile kaburi lijengewa kule machakani ndo akojendazikiwa yule mama mtu.

Tu BA2 F Akamkwama akamkwama akamkwama akamkwama, hata apofika akakayachi yle mwana akalia: "Kwih! Kwih! Kwih! Kwih!. Mama kiyu, mama njaya, mama kiyu, mama njaya, mama kiyu, mama njaya!" Akamwambiya: "Ewe mwana we! Kunichimbi tangu niliduniani hata kuno ahera we! Hebu nendaa-ah! Wende kule kule nikokwambia kunako ng'ombe ya mami-- ya babioni . Na mamio-- kawako huko, kiwamba wa kiwamba kutenda kulya. Lakini hende mpaka kwaza afike aitoe kauli penye mamie ndipo auke, ende kule." Apofika pale

umuri wa saa nane...

- TRANSCRIPTION MISSING HERE -

Tu BA2 F Pokwale na msile nam makame waMakame, wakatana, wakayoyana, Akakaya mwanamke yule akayonya ni minyumewe. Akavyaya Makame masikini, mtoto yakwe mmoja tu, -pa! -Muyumewe akafa. Sasa yule Makame maskini, babiye kavu na kazi yakwe ya bunduki, kwenda msituni akawinja ndege na paya, kanga wale, kima, halafu akapata kitoweyo kile kingine akendesa sokoni, kingine akajisa akawakana wanakuza. Sasa -pa! Pale akakutwa ni ahadi yakwe ile baba mtu akafa. Amekwisha kufa yule baba mtu, akakaya mama, akachunga eda, hata apokwisha chungu eda pale hata akachanjwa. Apokwishachanjwa yule, keshayawa kizungu cha nyumba.

Tu BA2 F Tena yule Makame maskini. Mazungumzo yetu ee, nazungumza ... nilipokwisha. Maana nilikwisha, mama amewikwa mwali.

Ki JM M Mh.

Tu BA2 F Akakaa, hata wakati wa kuchanjwa ule, akawa kanazunguukazunguuka mji aliuka yule Makame maskini. Akamwabiya: "Mama wee!" - "Oh". "Kazi ayoja akafanya baba nini?" Sasa nishakuwa mkubwa nataka kazi ajayo akaifanya baba na miye niendlele. Nifanye. "Akamwambiya vino: "Babiyo! Kanaamali yakwe kevu na bunduki yakwe ya kunja huko msitituni, akapata rizki akajisa nyumbani tukawa tunaa." Kula.

Akamwambiya: "Sasa baba, nikaa. Amali ayo akijitumia baba, sasa nishakuwa mkubwa mimi Makami maskini. Niendelele na kazi."

Ki JM M Mm.

Tu BA2 F Mwana wa Makame wa Makame huyo, na mamiye huitwa Mize wa Mize. Kushasikiya? Sasa kampachuliya bunduki pale akampa, akaaza kumfundisha vile akaicheki bunduki ile, akaicheki bunduki ile, akaicheki bunduki ile, mpaka ikakaya sawa. Sasa pakaja kunguyu akatunga juu ya mjiti, akaaza kulekesheni: "Huyule hampiga ndo samkuta au ilama itakosea". Alikwenda akaisimamisha bunduki, akampiga kunguyu Mungu, akajaliya shabaha zakwe zikenda pale pale alipo, tuuu! Alitoja tiii! Ile kunguyu. Akasema: "Basi, kazi ya baba zishaipata sasa. Naendelea na kazi." Akauka sasa akenda zakwe msituni.

Tu BA2 F Msitu na nyika, msitu na nyika, msitu na nyika, msitu na nyika, kanakwenda msitu na nyika, kanakwenda msitu na nyika, akakuta pelele, akakuta kanga, akakuta kima, kanapiga, sasa akapata kanakuja zakwe katika mji. Akafika kanendesa sokoni, kanakuza, wengine kanachinja wanapata kitoweo, wananunuya mposho wanakulya mule nyumbani mwao mzee wakwe. Akaendelea hata siku hiyo akenda zakwe msitu na nyika, msitu na nyika, msitu na nyika, msitu na nyika, mpaka akaligunduya jumba kuuubwa! Akasema: "Aka! Kwani mbona kuno msituni? Kuna nyumba ijengwa ni nani?"

Tu BA2 F Aka! Mbona nimakwenda na msitu - uuu na sijasikiya msituni kupojengwa nyumba, nyumba ya nani ile? Lakini sakwenda. Haitizame. Nyumba ile ijengwa ni nani, ya nani ile?" Sasa apofika pale, pale chi' pana mifunguyu ibwagwa: pwa! Pale chini ya ile nyumba, inamemeteka: "me-me-me-me-me-me-me", kwa mapambo ya zahabu ile nyumba. Kushasikiya? Sasa pale, akachukuya mfunguyo sasa. Kanaamrushwa yule tena ni malaika tena. Akachukuya mfunguyo akafunguya. Apokwishafunguya, ikafunguka "kwaa", ile kufuli. Akajaakatizama nyumbani mpangwa kula! Azana ya kitu kuwa maguniya ya mchele mua sukari muwa samli, BA2 muwa mabokisi ya mabomba ya sabuni, muwaa-- izo mafuta ya kuweshwa, muwa mafuta ya kujipaka, ya yuto, muwa kimbo, muwa kila kitu. ... Hasiya ya duniya nzima iwa katika nyumba hiyo. Akasema: "Lo! BA2 Sasa nishapata pa kuja kwigama sasa. Senda mchukuya mama sasa ayawe kuleee katika mahaka kule. Japokuwa ikawa katika mji samambiya: "Mama njoo, twende kuno msituni nishakuta nyumba inayo vyakulya, tupunguzee. Mawazo ya hatari yavaitufikiliya miaka nenda miaka nidi anayobuga mama kwa umasikini. Ehe. Maana mpaka na miye ndo jina lyangu waniti makame masikini kwa kuwa hatari iliyowafikiliya hata baba akafa. Ikawa tena yale mwana muwa mabunduki muwa ma-- jambiya, muwa kuki za mipanga, muwa kula kitu, kule zana za kuliya bina adamu ziwa katika nyumba hiyo."

Tu BA2 F Apofika kule, akamwambiya mama mpa-- mbo' mabomba (?) haya-- hayayo mifereji ya ndani, mifereji ya juu, nyumba hiyo inakula hasiya! Sasa, akenda akamwambiya mama wee, nimenda zangu na nyika, nimenda zangu na nyika, maana msituni huko. Msituni huku juu. Porini huko, msituni. Ukasikiya na nyika ndo veko, akawa kanakwenda naye na nyika, ndo Kiswahili swafi hicho. Akenda zakwe na nyika, akenda na nyika akeneda na nyika, hata akaligunduya jumba hilyo. Apofika anifunguyo hiyo, ibwagwa hapo chini, akafunguya akatizama, akachekeki akachekeki akachekeki, sasa aakajafunguya chumba cha saba kile kina shetani.

Tu BA2 F Kina nyoka na vichwa saba, kajituya kule juu nyoka kule. Vyoti vichwa vyakwe kuvilekeze chini hivi. Hapo alijifunga, nda! Lakini hefanya hofu wala hajitukiya. Akasema: "Heya, akaso mwenyewe nyumba? Heya basi. Madamu nimeshakwa riziki ni munyungu senda mwambiya: "Mama tuje tuhamile hii nyumba hela hiki chumba hilo asijefunguya. Maana nishaoneshwa ni muyungu senda. Anda muhazarisha mama mapema. Chumba hiki cha saba asijekifunguya, vyumba vyoti afungule, achukule vitu tutumile." Akarudi yule mwana, akakwa fikira ni Mungungu akenda.

Proofread by MY

Edited by TR in October, 1996

DAHE 48

Place: Tumbatu, Mkwajuni

Time: 18.10.1989

Interviewee(s): 1. (FJ1), 2. (HG1), 3. (NM1)

Interviewer(s): J. Madumulla (JM)

Recorder: Sony Professional

Language: Kitumbatu (Tu)

Topic: Hadithi

Remarks: Because of the dialect quotation marks may be displaced.

Ki JM M Kwa hiyo, lile pande lipo pale pale.

Tu FJ1 F Lile lipo pale pale. Akali-- akalikokota we, akalikokota we, akalikokota we, hata kufika kule. Kufika katalikata lile. Alitile mle mle kaangoni. Akalipika, pale pale uwanjani. Apokwihalipika, kuja lifunula ikamwagika feza. Watu wote wakaelemea pale pale. Wanaaliana "ooo, ooo", wanaunguya pale kwa moto wanaaliana "oo", wanavunga. Na wale wanaompiga wote, palepale. Ehee. Tena pale ika-- (makofi yanapigwa mara mbili)... mhishimiwa huyo. Kanawambia hivi: "Nyamazeni kimya! Mnisikize, niseme." Sasa, nyie wajomba wawili, mnaonaje, mshapajua alipokwiba?

Tu NM1 F Wale watoto.

Tu FJ1 F Ehee, kakize hao. Mshajua alipokwiba huyu ndugu yenu? Itikiani, eti, akasema: "tushapajua. Basi, hii hatari mnayoifanya, tena mwagikeni nyote, mwende zenu. Nyi wa kaka zakwe nendeni zenu, nanyi watu wa mji nendeni zenu mmwache yeye tu."

Tu NM1 F Mwizi!

Tu FJ1 F Wakamwagika, wakenda zao. Kwenda zao kule, na yule mfalme akenda zakwe. Basi baada tu kwenda zakwe, keshajua huyu ni kalmaldi huyu kapata uradhi. Mfalume akachukua tiriki akawapa maboi. Mfalume akachukua tiriki akawapa maboi zakwe: "Nendeni kwa yule bibi, mja kapigwa, mkafika mwambieje: 'Twambiwa na Bwana kanakudaka.' Mm. 'twambiwa na Bwana kanakutaka'" -"Je, akuowe vipi?" Mwambileni huyo bwana:"sina mtu". Kama ananikuta, kaniona mwenyewe. Atapokuwa kama niowa miye. Mshauri yake nani! Wakatoka, wakenda. Wapofika wakamwambia: "Aa, katwambiaje, ati hana mtu yanayomfika kunayeona wewe mwenyewe!" Basi ye, kanasema: "Itakuwaje kukaa kwenu ye na vee?" Akasema:"Nendeni! Mwambieni hayo yanayomfika, ndiyo yameyonifurahisha. Ndiyo maana ninamtaka miye nimuowe". Wakenda, akawambia. Akasema kuwa yale anayosema hayo...

Tu NM1 F "Nimuyole, usisema nimuowe!"

Tu FJ1 F Ee, "nimuyole". Ee, kama ndo anayosema hayo kuwa "nimuyole", ehee, haya. Tena ikawa akawatuma wale: "Nendani kwa mashehe wale nilowatuma wakaja kunizika mama yakwe". Kawachukueni.

Wakaja. Wapofika pale, akawauliza: "Hodi hodi, namwambieni je, yule mtoto, hana kaka, hana baba, hana mama, amaefiwa ni watu wakwe wote. Wamebaki wa kaka zakwe wawili. Na sasa wamchukia sana wamamchukia veye, wataka hata wasimwone!"

Tu HG1 M Wamchukia au wamchulili?

Tu FJ1 F Ee! Wamchulili. Wamchulili. Sasa, inakuwa: "Nimiyole miye, Mfalume." -"Hii itakuwaje?" Akawambia: "Aa, maadam kwisha mtaka, naye kamakutaka, basi muyole." Ee, muyole. Na kila kitu kuwa haki yakwe kama vile vile. Mpeni mwenyewe. Ikawa tena wakatoka wale. Kesha kubali. Sasa wakatoka wanayo ile - ile ile tiksi, wakenda alipo. Wana buibui, wana khanga mbili, wana khanzu yawo, wana vikatu vya watoto, wakenda wakamwambia: "Ati twaambiwa na Bwana tukupakie, na kama ulichokuwa nacho, yeye ametwisha yakwe veye." Ejee. Akaeza ile feza yakwe akatia kiguniani, tena na wale watoto wakwe yakawakosha akawavika zile nguo, na yakakoga wakingia katika ile gari, uyoo, wakenda zao. Enhee, wakenda zake kwakwe. Baada ya kwenda zakwe wale, wataziika. Wataziika saana.

Tu NM1 F Nani?

Tu FJ1 F Wale kakize!

Tu XX F Wale wajomba.

Tu FJ1 F Enhee. Mhuu.

Tu NM1 F Ndugu zake.

Tu FJ1 F Mhuuu. Wakaziika sana, zikikubwa. Wakenda waka - wanamweza wa kumyoilia pale, wanakweze wakumvilia ata wakamtokezea pale pale pakwe. Wapomtokezea hivi wakachungulia. Na kucbungulia kwao bwana, wanapiga kofi hivi (anapiga kofi tatu, pwa! pwa! pwa!). Wanayomba, Ee. Wanapiga kofi hivi (anarudia kitendo), wanayomba. Watoto wakasema: "BwanaBwana! Yuko Bwana mgeni kule! Anapiga kofi akafanya hivi". Boi nendeni, mukamtazame. Wakenda wakamtazama. Wapoenda watazama wawili wa vile vile, hawana nguo. Mh. Wamaziika kweli nao wanawake na watoto. Wakenda, tena akawaambia nendeni ukamtizame. Mleteni huku, ee, mleteni huku. Akapelekwa kule aliko, wakafanyiziwa chai, wakanywa, wapokwisha kunywa...

Tu NM1 F Wote wawili!

Tu FJ1 F Wote wawili. Watu kama wale, akawambiaje: "Je, shauri yenu nini?" Akasema: "Shauri yetu siye ziki" Tukutwa ni ziki...

Tu NM1 F Twafaa ni njaa!

Tu FJ1 F Twakosa kwa kutia roho yetu. Eheee. Tukutwa ni dhiki twakosa kwa kutia roho yetu.

Tu NM1 F Twafaa ni njaa!

Tu FJ1 F Basi tena pale, ikawa wakafanyiwa chai wakanywa, wapokwishakunywa wakaanguliwa nini - ma--machungwa, wakang'olewa muhogo, wakatiliwa pakachani. Wapokwisha wakapachuliwa kila mtu shuka yakwe. Wakavaa vigoya pale. Wakaja kwenye chakula wakavaa vigoya. Ehe, vigoya. Wakachuka wakambiwa nendeni, halafu kisha vitu vyakulya hivyo, -"Njoooni!" Yule mfalme. Ee. "Njoooni." Hawayajua kwamba yule ndo alipo. A'a.

Tu NM1 F Kajifichi!

Tu FJ1 F Ee, kajifichi. Ikawa tena, wakenda wapokwishauka pale yule, mfalme akapiga upatu, akaweta. Akawetaje: "Watu nammwiteni hapa mnikutanikila mara moja. Ee mara moja mfike hapa, mkutane wakaja

kutana pale." Akawambia: "Nendani miti, pesa zenu tayari." Mzijenge nyumba mbili, siku mbili hizi hizi zishe. Na mnachokitaka, samkanis!" Ndo yule, mfalme. Wakazijenga, wakata miti wakazijenga. Wapokwishazijenga zile nyumba, tena pale atapokwisha kuja vile vitu vivokwisha wakenda. Wana vigoya vyao na vigoya wavaa. Wapokwenda pale tena, akawambia kwani: "Nye bwana, mna watoto?" Wakasema: "Tuna watoto". -"Mna wake?" -"Tuna wake." Keshakwambia ni yle bibi yakwe kuwa ndo wale. Nawe keshawajua. Mh. Basi tena pale, ikawa wakaja pale. Wapofika nyumba zishasimama, zishakandikwa, zishatiwa milango. Wakambiwa: "Nyumba zenu hizo, niwazokujengeani." Yule kanasema mfalme: "Kila mtu yakwe, nishazijenga miye. Tena mkachukule watoto ki - umoja wa kina mama walete hapa." Wakale. Wakaja wa kamtumikia yeye yule yule, waliyeja kampiga. Wanamlimia, wanamletelya kula jambo. Hapo basi. Tena, naye ndo kastarehe pale pale. Wakawa watu tena yamekwisha. Yangu miye nayoko kesha.

Tu NM1 F Makindano yamekwisha.

Tu FJ1 F Ehee. Ndo ilivyokuwa hivyo.

Ki JM M Asante sana, asante sana. Sasa "kigoya" ni kitu gani?

Tu FJ1 F Kigoya...

Tu NM1 F Nguo.

Tu FJ1 F Kishuka. Wavaa kama hivi vishuka tu, basi.

Tu NM1 F Hapa tu, (anaonyesha sehemu za kiunoni hadi mapajani) hakuna nguo nyingine.

Tu FJ1 F Kama hivyo hivyo, kigoya.

Tu HG1 M Bwana Madumulla kwa kumsaidia mama kuweka sawa zaidi, kigoya yaani, inaweza kuwa aina ya kishuka yoyote ile ya kujitoikeza hapa, si kwa kawaida. Ndo uvaaji kinaweza kuwa kimefika humu.

Tu FJ1 F Kidogo tu, kigoya tu wavaa (wanaongea kwa pamoja, hawaeleweki vizuri)

Tu NM1 F Ee ndo kigoya hicho. Huvaa ja hivo, amba hakifiki kutini.

Ki JM M Kinaficha tu hapa.

Ki JM M Kazi kwako, karibu.

Tu FJ1 F Yaani, nianze kutaja jina langu...

Ki JM M Ehee.

Tu FJ1 F Jina langu Fatuma. Fatuma Juma, mzaliwa wa Tumbatu Kisiwani. Tumbatu Kichangani.

Ki JM M Na mwenzio, mwenzio anaitwa nani?

Tu FJ1 F Mwenzangu, anaitwa Nachoshe Makame.

Ki JM M Na unatuelezea Kigano. Unasimulia Kigano?

Tu FJ1 F Ngano...

Ki JM M Ngano. Hizo ngano, umezipata wapi? Ulifundishwa na nani?

Tu FJ1 F Nilifundishwa ni shengazi, Bi Jabu Haji. Kesha kufa.

Ki JM M Ahaa. Karibu.

Tu FJ1 F Asante. Paukwa.

Tu NM1 F Pakwa.

Tu FJ1 F Hapo zamani za kale, wavuko watu Makame na Msile. Wakayoyana, wakavyaya wanao saba, ya saba kichinja mimba. Sasa katika kukaa yule Makame, ni mtu masikini sana.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Wakaeshi huko porini.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa baadaye hata wapokuwa watu wazima na wale watoto hawana cha kuvaa...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Baadaye, pale yule Msile, akaamua kwenda kuvua.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akawa kanavula. Mwenyewe hupata kidagala chakwe kimoja tu.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Wakaja wakala watu wote nyumbani. Wale watoto saba, pamoja na huyo Msile na mkewe.

Tu NM1 F Mh.

Tu FJ1 F Sasa hata baadaye...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Walikala, wakakala, siku za kukala...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Wakatembea kule kule. Mtoto mmoja, yule kichinja mimba alitembea porini.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Apotembea porini, mpaka akendka kagundrua kijiji kimoja...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F ...kina watu.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa, katika kijiji kile, akaamua: "Mimi ni mgeni hapa, nitaeshije?"

Tu NM1 F Mh.

Tu FJ1 F Sasa akapata bwana mmoja, aitwa Makame...

Tu NM1 F Mh.

Tu FJ1 F Ikabidi yule bwana Makame alimpenda yule Mboja, yaani yule kichinja mimba yule.

Tu NM1 F Mh.

Tu FJ1 F Alipompenda, akamwambia: "Twende zetu nyumbani, ikafanyike harusi."

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Sasa, wakaja zao mpaka nyumbani, muda wa siku saba msafara wao.

Tu NM1 F Eeh.

Tu FJ1 F Ikafanywa harusi. Ipfanywa harusi, sasa yule bibi harusi na bwana harusi ikabidi warudi kwao...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F ...kijijini.

Tu NM1 F Sasa pale nyumbani alipoagwa na wale wazazi, yule mzee Msile na yule wanamaangishwa yule, Mboja, na yule bwana Makame wa kijiji cha pili. Akaambiwa: "Katika msafara wenu kuna mjiti, una matunda."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Lakini katika matunda hayo, yamakwiva sana. Hela msijenda ya chuma mkalya. Sasa: "Haya tushasikia." -"Mshasikia?" -"Tushasikia." Walilawa Mboja...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F ...na Makame.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Yaani, ndo mumewe bwana harusi.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Wakenda zaooo, mpaka kufika karibu na kijiji kwa siku ya kwanza wako njiani, ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, mpaka ya sita. Wakanda-- anaona ule mjiti una matunda yeevu hayo. Yapo kwiva yule bwana Makame alimwambia mkwewe: "N'nda pale, chini ya mjiti n'nda haja."

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Akamwambia: "Usende mana ule ndo mjiti tulokwambia usijenda Iya zile tunda."

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Akamwambia: "A'a, miyenda haja." Alikwenda yule Makame. Sasa mkewe kamngojo njiani. Alichuma yale matunda, akawavia...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akawavia, mpaka yakamlevya. Hata pomlevya alikwenda akamwambia yule mumewe hananuka. Akamwambia:

Tu FJ1 F Tunda makame,

Tu WE nyambiwa haziliwa tunda.

Tu FJ1 F Tunda makame,

Tu WE F nyambiwa haziliwa tunda.

Tu WE F Zaweza n'shegesha zina

Tu WE F mke wangu, zinaenshegesha.

Tu WE F Zaweza n'shegesha zina

Tu WE F mke wangu, zinaenshengeshu.

Tu FJ1 F Akambururu mpaka pale njiani.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Hata apombururu mpaka pale njiani, ehe.

Tu FJ1 F Akaanza kumkokota tena:

Tu FJ1 F Tunda makame,

Tu WE F Nyambiwa haziliwa tunda.

Tu FJ1 F Tunda makame,

Tu WE F Nyambiwa haziliwa tunda.

Tu WE F Zaweza n'shegesha zina

Tu WE F mke wangu, zinaenshengeshu.

Tu WE F Zaweza n'shegesha zina

Tu WE F mke wangu, zinaenshengeshu.

Tu FJ1 F Maana ya kule "zinanshengeshu" "zinanilevya" hizi.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Sasa, kila akamwambia "tuuke twende zetu", hanavyezauka. Sasa yule bwana, hata kenda (?) akakaribia kile kijiji, yule bwana alikufa.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Apokufa, sasa nimtendeje, yuno yuli mke akalia:

Tu FJ1 F Tunda makame,

Tu WE F Nyambiwa haziliwa tunda.

Tu FJ1 F Tunda makame,

Tu WE F Nyambiwa haziliwa tunda.

Tu FJ1 F Sasa kule katika kuimba vile wana walikuja wanapika kofi lakini hawajui huo mwida huo una maana gani. Walijamsaidia yule bibi, sasa: (akipiga kofi):

Tu FJ1 F Tunda makame,

Tu WE F Nyambiwa haziliwa tunda.

Tu FJ1 F Tunda makame,

Tu WE F Nyambiwa haziliwa tunda.

Tu WE F Zaweza n'shegesha zina

Tu WE F mke wangu, zinaenshengeshu.

Tu WE F Zaweza n'shegesha zina

Tu WE F mke wangu, zinaenshegesha.

Tu FJ1 F Mpaka wapofika kijijini pale, akenda kuwaita-- akenda weta watu. Apoenda weta watu, wakaja kumtazama yule mumewe ambapo ndo bwana harusi, kesha kufa. Sasa nyie, akaulizwa ni mzee wa kijiji. - "Ehee wanangu, maafa gani hayo yayomkutani hata huyo mwenzio akafa?" Akamwambia: "Huyo bwana ameondoka ni ... harusi. Lakini huko kwetu wakati tunashidikizwa ni hao wazazi, watwambili kuna mjiti una matunda yevu sana, heya msijenda kulya! Maana hayo uchawi!" Sasa huyu mume wangu apoono huo mjiti, akanyambia kanda haja, kumbe ka'nda wavia yale matunda. Apoyawavia, ndo yakamzidia tena ndo ya-- hanamburura, kana roho yako (?) hata kanapofika hapa ndo kesha kufa. Ikabidi hapo, tena achukuliwe maiti na yule bibi ahaifaziwe. Akenda akazikwa yule maiti na yule bibi akarudishwa kwao akaelezea yale mambo yayomfika mle njiani. Tena na yule bibi akakaa kizuka pale pao. Na ngano yangu ndo ipokwishia hapo.

Ki JM M Loo, asante sana. Eee, nadhani usiposikia la mkuu, unavunjika guu. (Kicheko). Una hadithi nyingine?

Tu FJ1 F Ninazo, tena jua lilishatula, ... tele.

Ki JM M Ahaa

Tu FJ1 F Ehe, maana kuna ya hadisi ya papa na kima.

Ki JM M Papa na Kima.

Tu FJ1 F Papa na Kima.

Ki JM M Wakigombania moyo.

Tu FJ1 F Eee. Kuikua' yo.

Ki JM M Ee. Karibu.

Tu FJ1 F (Kicheko) Paukwa.

Tu NM1 F Peka.

Tu FJ1 F Hapo zamani za kale...

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Wavuko Papa na Kima. Sasa huyo mzee kima huyo, alienda zakwe kulee, pweko pweko kule, Magomani. Sasa pana mjiti mkubwa huitwa Mvuyu. Sasa katika ule mjiti yule mzee kima hulia pale, akemba michezo yakwe kya ile kima.

Ki JM M Mh.

Tu FJ1 F Sasa ile sauti ya kima ilisikika mpoaka baharini kunako Mzee Papa. Sasa na yule Mzee Papa huja zakwe mpaka pale kumsikiza yule kima.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa yule mzee papa alimwambia: "Mzee Kima we, tupange urafiki."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Aka-- "Tutauapanga vipi urafiki, nami miye kima niwa kuno juu ya Mvuyu?"

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F "Weye kuwako chuvini!"

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Akamwambia: "A'a, tupange urafiki." Tupange urafiki. Akamwambia: "Haya, kama kushaweza kupanga urafiki na miye, lakini miye, niwa juu ya Mvuyu. Na weye, kuwa katika bahari." Akamwambia: "A'a, basi miye urafiki wangu uliokuwa ni wa katika bahari ntakuja hapa, tuwe tunazungumza." Sasa wakawa wanazungumza kima na mzee papa. Sasa, kumbi yule papa kana mamiye mgonjwa kule baharini.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Sasa katika mamiye mgonjwa yule, zimatizamwa dawa, kama kwambiwa hapolo mamiye, mpaka upatike moyo wa Kima.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akamwambia aka-- --"Mama we, kutapola ukajaliwa ni Mulungu. Maana miye ninaye rafiki yangu mkubwa Kima."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akambia: "Kama kuna rafikiyo huyo mzee kima..."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F ...basi, nenda ufanyefanye mpaka umwibe, tuje tupate huo moyo wakwe."

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F "Tutaupata moyo vipi?" -"Tutamwula, tena tupate huo moyo." Haya. Sasa akenda zakwe, mpaka chavulani pa maji pale.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akamwita yule mzee kima: "Rafiki yangu Kima! Rafiki yangu kima!" Yule kima akatenda: "Nchya! Nchya!" Akaja. (kicheko) Sasa apokuja yule wakazungumza, akamwambia rafiki yangu miye nimeja kukuchukula. Aka-- (kicheko)

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F "Hohohohoho! Nchya nchya!" kanachogea. Sasa pale...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F ...alichogea, akamwambia: "Kutanichukuya vipi?"

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akamwambia: "Sakuchukula tukatembele huko baharini, ukakuona kwetu mana fwe huku kwenu, nishakoona hapo kwenu juu ya mjiti, lakini miye hujii kiti nnachokalia huku baharini. Heya twende."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa mzee kima akamwambia:"Haya twende!" - "Zakaya wapi?" Akamwambia: "Kafa hapa katika pezi lyangu, hili bewe lyangu hili."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Ulishika uzuri. Mzee kima pale akajitosa, wakenda zao. Wakenda zao kimya na Mzee Papa. Kanakwona maji yamo mengi yule Mzee Kima. Yako na masamaki, manyama mengine, mapapa mengine yanawapita. Pale na: "Salaam aleikum!" -"Aleikum salamu, unarudi?" -"Ah, nakwenda natoka kumchukua rafiki yangu Kima Bwana. Sasa hata kule baharini kanataka karibia pale pao." Alimwambia: "He, rafiki yangu leo, utakiona cha mtema kuni!"

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F "Maana huku leo k'nda chinjwa mana mama mgonjwa, upatike huo moyo, mama apole."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akamwambia: "Aka, rafiki yangu, basi we huna akili." Yule mzee kima kanamjibu mzee papa. We huna akili.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F -"Maana kama kuvu na akili ungenieleza kulekule juyu. Maana swiye kima hiyo myoyo yetu, twawika masundukuni, kukaye. Au juu ya mijiti hatutembele nayo, maana hiyo mioyo ya Kima ni mali." Anamwambia: "Sasa rafiki yangu, huna moyo na mimi nimekuchukula kwa haya maswali ya kwenda!" Akamwambia: "Basi wee, ungenirudiza henda hauchukula."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akamwambia: "Hata moyo kuna." Akamwambia: "Mi sina moyo. Maana myoyo yetu siye hatutembele nayo." Sasa yule, mzee papa akasimama na nyumba yao ndo ile pale mzee papa.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Ikabidi yule mzee papa kwa ujinga wakwe amrudrize mzee kima maana akautwale ule moyo. Wakaja zao na yule rafikiye mpaka vhavuyani pa maji.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa kufika chavuyani pa maji akamwambia: "Sasa we rafiki yangu, weye habaki hapa weye, kutaningoja hapa 'nda utwala ule moyo." Mzee Kima kushateremka beweni pa papa alirukia mjiti (kicheko) Alitenda: "Nchya! Nchya! Nchya! Hohohohoho! Hohohohoho! Nchya! Nchya!" - "Rafiki yangu, umenikosa! Tena rafiki yangu mnakusikitikia mana umanikosa, na tena katika watu wajinga na papa mmoja weye mzee papa." Akamwambia: "Kwa nini rafiki yangu? Aka, kwani we kuna habari, kuna mtu gani mweumbwa ni Mulungu akatiwa moyo na maini na nyongo ikesha ikayavigwa ni mtu akawika sandukuni?" Mwe kwambia: "Maneno iyo nani? Aa rafiki yangu teremka twende sikufanyi hivyo."

Tu FJ1 F Akamwambia:"Kushanikosa." Apokuwa alikaya Mzee Papa, akalia akahuzunika sana. Mpaka maji yakamkukiza, na mzee kima kanamtizama kule juu ya mjiti. Na mzee papa hana uwezo wa kurukia kenda kwa mjitini kunako misita kima...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Tena pale akakaa, kahuzunika hatapokwona chuvi ma--

Tu NM1 F ...ishatoka.

Tu FJ1 F Ishatoka. Akajiburura kenda zakwe, na ngano yangu ndo ilipokwishia hapo.

Tu NM1 F Ishakwisha.

Ki JM M Asante sana.

Tu FJ1 F Heya ziwako zijaya tena ndo sanduku zima

Ki JM M Ahaa.

Tu FJ1 F Zo ngano.

Tu FJ1 F Paukwa...

Tu NM1 F Pekawa.

Tu FJ1 F Hapo zamani za kale...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Kavuko Makame wa Makame...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Na Mwana Mize.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Walikaa, Makame wa Makame na Mwanamize wakavyala mwana wao mmoja tu. Wapokea mwana yao mmoja yule ya kike.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa, walikaya hali ya kuwa ni wanyonge, masikini sana. Sasa yule baba mtu...

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Mtu mzima. Kazi za kale ni uvuvi tu, hekujua kazi nyingine na kulima.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa wakenda zao wakalima, wapokwihalima sasa yule bwana, alikaa yule mtoto wao alipomaliza kukua yule...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F ... Mungu aliwkafungulia uzazi mwingine tena.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Wakafunguliwa uzazi watoto watatu wa kiume. Na yule dada yao ni mwanamke.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Sasa pale walikaya baba yao ni mnyonge. Kule pwani kanakokwenda kuvuya Munga kanamka hata kile kiburu.

Tu NM1 F Kidagaa.

Tu FJ1 F Kile kiburu hanamka.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Sasa, hata apokuja, Mwanamize na yule-- wale wanawe washikitamaja hivi.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Wakaya chi wangojo kulya nako hakuna kulya.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Sasa yule bi mwanamiza animwambia mumewe: "Ewe mulume wangu we nga hwenda rukaruka migogo we, nga hwenda rukaruka migogo."

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Kamwambia: "Harukaruka migogo, kesha rukaruka migogo kwani ndo tutakulya?"

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Akamwambia: "Eehe." Basi yule bwana alienda kata mashina ya mnazi ule.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Akarukaruka:

Tu FJ1 F "Narukaruka migogo,

Tu FJ1 F narukaruka migogo.

Tu FJ1 F Nipate kurya.

Tu FJ1 F Narukaruka migogo,

Tu FJ1 F narkaruka migogo,

Tu FJ1 F Nipate kurya."

Tu FJ1 F Akarukaruka ile migogo:

Tu FJ1 F Narukaruka migogo,

Tu FJ1 F narukaruka migogo.

Tu FJ1 F Nipate kurya.

Tu FJ1 F Sasa wakaja watu: "We bwana, kuwa mzima au kuwa mgonjwa, Nembwiwa ni mke wangu nirukeruke migogo:

Tu FJ1 F Narukaruka migogo,

Tu FJ1 F narukaruka migogo,

Tu FJ1 F Nipate kurya.

Tu FJ1 F Akarukaruka, hata jioni hana achomfumbula. Alirudi nyumbani.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F "Nachoka! Nimachoka narudi kurukaruka migogo." -"Umenda rukaruka migogo vipi? Mbona kuwa hali hiyo? Sikuniambili harukarukaruka migogo?" Akamwambia: "Kwani migogo kurukuruku vipi?"

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F "Nimakata shina lya mnazi, nimepata migogo yangu mine nimarukaruka tangu hunju mpaka sasa, na nisebata kulya." Akamwambia: "A'a, ukasikia kurukaruka migogo, mtu hwenda akafanya kazi kama kulima au akatumika mwa wenziwe mnamo vyakula akapata kugaiwa kulya."

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Akamwambia: "A'a, kama ndo hivyo haya, lete gunia."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akashukula gunia yule mke akamka gunia, akenda zakwe kutwa. Kumbi yule bwana kende lisindia mchanga lile gunia.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Apoenda lisindia mchanga...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F ...akaja nalyo pale nyumbani jioni, pwaa, akalibwaga. Baada ya kulibwaga tu yule bwana alilawa shuti.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Alipaga mbio.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Kanasumka, maana keshaja bwaga mchanga.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Sasa wale wana na yule mwamiza wana namna ya njaya.

Tu NM1 F Wishategemea...

Tu FJ1 F Waloiuka akamwambia mwanae nenda kakoke moto.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Akenda koka moto. Kafungule lile gunia. Mungu alijalia lile gunia lya mchanga uligauka mtama. Rehema za Mwinyenzi Mungu ule mchanga uligauka mtama. Wakachukula mtama ule, yule bwana kende zakwe huko, harudi.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Maana kaja bwaga gunia lya mchanga.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akakala wale watu wanatwanga mtama wakalya, wakatwanga bwana kasumku yule. Hata siku hiyo, kajipaka masizi muuso mzima humo.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Na mwili wake wote na kigoya chakwke hapa kajifungu. Kanaja kichugu kidugu kanachungulia. Aa, sasa yule mwanae mmoja yule mdogo: "Mama, ayo baba." -"We, siyo babayo" Hukaa yule mwana wanakulya. Tena humuyomba yule mwana yule vile wanavyokulya ule mtama. -"Mama, baba kananiomba." Tena yule bwana husumka. Hata wakakala wakakala, mpaka yule mama mtu akazunguka kule nyuma, kweli

akenda mkuta yule mulumewe. -"Ah, mbona mulume wangu kukaya hapa?" Sasa njia ya kupita hana kanatetemeka manake alibwaga gunia la mchanga (kicheko).

Tu NM1 F Mchanga...

Tu FJ1 F Sasa weye pita huku nyumbani ulye. Sasa kanatetemeka kuja pita, ubwabwa wa mtama unishapakulwa pale.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akalya, kule kulya kwakwe kiowoga woga mana asije kuambiwa we kutugisili mchanga. (kicheko) "Sa akalya pale apokwishakulya katumburizi midicho pale. Sasa kashigisi jinsi ya kuambiwa vipi hapa unapolya ubwabwa wa watu. Kayatumburizi midicho na matonge makulu". (kicheko) Apokwishayachota yaloe mitonge mikulu sasa kanataka sumka. Akamwambia: "Ah, sasa kwenda wapi bwana hunatunza hadi tangu siku ile ujatubwagia gunia ya mtama. Mpaka leo hatujakwona. Kwenda wapi?" Alimwambia: "Aka, kwani ule niojawabwagia ni mtama? Mke wangu?" Akamwambia: "Ee, ni mtama."

Tu FJ1 F Ndo huu tumautwanga. Alhamdullillah, Rehema za Mwenyezi Mungu kubwa. Mtama, niojawabwagieni wakamwambia ehee mtama, ndo huu tunaotwanga na tena ndo huu unaokulya."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F -"Sasa mbona kunaniuliza hivyo kama mtama, kwani wewe azima yako kutuletele nini?" Akamwambia: "Hata sikuhadithili, mpaka mtama huo uishe."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa walikala pale hata siku za mwisha ule mtama, akamwambia: "Basi mke wangu ule niojajiza si mtama. Nyende kumba mchanga wa fungu kwa hali ya taharuki. Haja habwaga pale, ndo kisa kichonisumsa miye ha pale."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akamwambia: "Basi kama ndo hivyo, shika mundu ule pale, tukalime."

Tu NM1 F Tukalime...

Tu FJ1 F Maana hii yote ni mafundisho kwa Mwenyezi Mungu. Ndo aposhika mundu akalima tena wakakaa hali ya kuwa ni watu wanadhifu weshakuwaa, ee, tena na hadisi yangu ndo ipo kwishia hapo.

Tu NM1 F Nzuri sana

Tu HG1 M Nzuri. Sasa ndugu Madumulla, unapata nini hapa...

Tu FJ1 F Ee?

Tu HG1 M Namwambia Madumulla. Kwa sababu hapa ipo mantiki nzuri sana

Ki JM M Ndiyo, ndiyo.

Tu FJ1 F Hela viganu vijala tele viko vijua sandukuni.

Ki JM M Nadhani mwenyewe anaweza akajazilizia.

Tu FJ1 F Miye?

Ki JM M Ee.

Tu FJ1 F Hapa tena kesho.

Ki JM M Aa, funzo la kigano hicho.

Tu FJ1 F Mafundisho kama haya, tunaambiwa tuache uvivu kwa hapa petu, kwa huko duniani, uzembe. Maana ukategemea kulishwa tu, hwenda njala ikakwangamiza. Sasa hapa, ningependa kama hawa watu wazembe wavivu...

Ki JM M Ehe.

Tu FJ1 F Tuanze kushika majembe bila hatujaambiwa. Maana, kwka huku kwetu tulikwambia "Mjima hambiwa". Isipokuwa tu, ukafika mwaka mtu kanashika mundu wakwe. Kanda lima. Sasa hilyo ni fundisho kwa sie wenyewe wanyonge.

Ki JM M Ahaa.

Tu HG1 M Sasa kuna fundisho lingine ... ficha, nyote hamjaliona. Pana fundisho hapa kwa pale unapoambiwa kusema uongo, unapozidiwa...

Tu FJ1 F Ehee, maana kila uyongo, haurongwa tu kiovyoovyo, isipokuwa panapofika kushazidiwa. Ndo utapozua uyongo. Upate njia ya kupia.

Tu HG1 M Hapa alipochota mchanga na akahakikisha mpaka sasa hivi.

Tu FJ1 F Huu mchaga:

Tu HG1 M Huu mchanga, akakimbia...

Tu FJ1 F Akasumka kwa sababu kede (?) cha mchanga nyumbani. Na sasa kumbi ule ule mchanga, Mwenyezi Mungu kwa rehema zake kaigeuza chembe ya riziki. Ilihali huwa kanafundishwa sasa ni Mwenyezi Mungu. Angilepo ini akalime.

Ki JM M Nzuri sana.

Tu HG1 M Alivyo.

Tu FJ1 F Kwa hiyo, mgaagaa na upwa hali wali mkavu.

Tu NM1 F Haya, kwako.

Tu FJ1 F Paukwa...

Tu NM1 F Pekawa.

Tu FJ1 F Hapo zamani za kale ku-- kuna bwana mmoja, Mwenyezi Mungu kamwumba shoti.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Yaani uso wake upande...

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Pua yake upande...

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Shavu lyakwe upande...

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Mkono wakwe upande...

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Mpaka ubavu. Pamoja na mgulu wakwe upande.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Sasa yule bwana, akaka hali ya kuwa ni masikini sana.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akakala mpaka akawa mtu mzima.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Ikawa hana hata kibwanda cha kuvala.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa, pale katika mji wao pana majahazi yanasafiri.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Yaposafiri, majahazi Pemba na Unguja.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Sasa, akenda kwa nahoza wa kwanza: "We bwana we, nipakiya nyende hawe uledi wako, nikapate bwandalya kuvala."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akamwambia: "Mwanaharamu, nuhusi yule. We mtu Mungu kaukumbu upande upande tena kunaja nipumbaza kunanihusi!"

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F -"Ngoja kwanza", huambile mabaharia.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa, akenda kwa mabaharia.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akenda wambia wale mabaharia...

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 kama kule kamaja yule kibwana kuapande, kanataka apakiwe eti akapate bwanda

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Akasema: "Nuhusi huyo", wale mabaharia, "nuhusi huyo". Kama katangia chombo hicho...

Tu NM1 F Sachelea.

Tu FJ1 F Sachelea.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Maana huyo nuhusu hatunajenda pata cho chosi.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Sasa yule Bwana Upande aporudia kwa yule nahoza, akambiwa: "Siye hatutokupakia mana mabaharia wote hawataki, mana kuumbwa upande." Sasa yule kibwana upande, alenda - wale wenyewe weshakuja huku julu...

Tu FJ1 F Walija zao nyumbani kwao. Sasa yule Bwana Upande akenda jitia mle chomboni akajificha iko fogonyani huko.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akajiziba magunia kule fogonyani.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa apojiziba kule maguniani...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Hata wenyewe wapokuja wenye kile chombo, wakanza kutweka lile, chombo chao, hawana habari kama yule bwana kawamo.

Tu NM1 F Kawamo, ehe.

Tu FJ1 F Hata wapofika baharini yule bwana alijifichula. Akazamka kule fogonyani.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Apozamka kule fogonyani, kila mtu: "Ah! Nuhusi huyu-- nuhusu huyu basi huku chombo hiki leo kitatiwa upepo mwingi mwanaharamu mana tukwambili huku kuna mawimbi! Nawe huyeza kazi hiyo si hali yako ya kuumbwa upande."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa yule Bwana Upande akawambia: "Miye leo hata mnitukane. Nikafa miye humu baharini na nyuwe mtakufa. Nikapona miye na nyuwe mtapona. Ikawa kila mtu pale kachukiwa." Sasa wakenda zao, hata kufika kule Pemba, ile bandari wanayotula zile inayo wenzao ina vyombo vingine...

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Wasitule mana hewapakia mtu mana wapakili nusu mtu.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Wasijenda kwona haya.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Sasa wakenda bandari hiyo, kumbi ile bandari ile...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F ...ya jini.

Tu NM1 F Wakatua jahazi yao pale, wapakika. Sasa bwana upande wapopakua vile vyakulya, tulye na bwana upande kila mtu: "Miye sitaki kulya na nuhusu! Miye sitaki kulya na nuhusu, mtu kaumbwa upande ni miye mije niwe Upande."

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Sasa pale yule bwana upande akapokuliwa chakula kaja kagelewa huko.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Akalya, apokwisha kulya akashukuru Mungu. Hata usiku...

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Wakakaa pale hata usiku kila mtu keshagweza kigunia chakwe mwenyewe, kama jitungika huko juyu ya chombo kalala usiku.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Sasa na yule Bwana Upande na veye, akezaha pale (?) yape kumbi kule kidamu kule kunako kasama kule. Akalala. Lakini katika kulala vehe, helala usingizi.

Tu NM1 F Kana wasiwasi.

Tu FJ1 F Kanasikia kishindo kinakuja cha upepo. Upepo unavumavuuuuu, na kile chombo kinakuja juyu na chini kwa chini kwa ule upepo na mawimbi.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Sasa kufika pale jahazini kumbi lile jini.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Akaanza lile jini:

Tu FJ1 F "Aliyelala nani,

Tu FJ1 F aliye macho nani?"

Tu FJ1 F -"Ni mimi Ngeko, Kibwana Upande,

Tu FJ1 F mimi Ngeko, Kibwana Upande."

Tu FJ1 F -"Wewe Pande hulali, kwa nini?" Lile Jini linanjibu, "wewe Pande hulali, kwa nini?" -"Ng'ombe hao wananihangaisha." - "Kama ng'ombe wanakuhangaisha, kesho wote watachinjwa." Sasa ule mjini ule, ulivuma ukenda zakwe. Wakakaa, siku ya pili yule bwana Upande asiseme kitu, maana ndo mnyonge hasemi na mtu. Sasa pale wakashinda kutwa asiseme. Wakashinda, wapakika, wakalya na jioni wapakika hawatokezi kule kunako wenzao mana ndo wakaja kaa kule kusudi.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Mana aligwe bwana Upande.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Hata siku ya pili wakalalapo, hata waposhakala, hata jioni pale kanasikia tena wenzie weshalala ve, kanasikia kishindo kinakuja vuuuuu, upepo ule.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Jahazi linatingishika kwa maji makali.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Hata apokuja:

Tu FJ1 F "Aliyelala nani

Tu FJ1 F aliyeamka nani"

Tu FJ1 F -"Ni mimi Ngeko, Kibwana Upande,

Tu FJ1 F ni mimi Ngego, Kibwana Upande."

Tu FJ1 F -"Wewe Pande hulali, kwa nini?" -"Ah, mbuzi hawawananihangaisha." -"Kama mbuzi wanakuhangaisha kesho wote watachinjwa." Siku ya pili wale mbuzi wote majini yakawalazalaza wale. Pamoja na ng'ombe...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Wakenda zao.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Wakakaa, siku ya tatu yakwe, yakawa hivyo hivyo.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Jua lilipotua vile vile, akaja lile jini: vuuuu! Hata kufika pale, jahazini:

Tu FJ1 F "Aliyelala nani?" Tena kwa ukali:

Tu FJ1 F "Aliyelala nani,

Tu FJ1 F aliye macho nani?"

Tu WE F "Ni mimi Ngeko, Kibwana Upande,

Tu WE F ni mimi Ngeko, Kibwana Upande."

Tu FJ1 F "Kwa nini wewe Pande hulali, kwa nini?" - "Ah, kondoo wananihangaisha." Kesho wote watachinjwa. Mana nna haja ya kula nyama zangu humu. Akamwambia: "Haya bwana, nami nalala." Wakenda wakachinjwa wale kondoo. Siku ya nne, hivyo hivyo akaja tena. Ahamwuliza:

Tu FJ1 F "Aliyelala nani,

Tu FJ1 F aliye macho nani?"

Tu FJ1 F -"Ni mimi Ngeko, Kibwana Upande,

Tu FJ1 F ni mimi Ngeko, Kibwana Upande."

Tu FJ1 F "Wewe Pande hulali, kwa nini?" -"Ah..."

Ki JM M Tena siku zote...

Tu FJ1 F "Hulali kwa nini siku zote! Kila nikaja, we uko macho! -"Ah, Kuku wananihangaisha" -"Kuku wote kesho watachinjwa."

Kuku wote wakenda wakachinjwa. Sasa akaendelea hivyo hivyo hata apoona wale wanyama wote weshamaliza. Akaja bwana. Lile jini:

Tu FJ1 F "Aliyelala nani,

Tu FJ1 F aliye macho nani?"

Tu WE F "Ni mimi Ngeko, Kibwana Upande, ni mimi Ngeko, Kibwana Upande."

Tu FJ1 F "Wewe mwanangu Pande hulali kwa nini?" Akamwambia: "Minazi nanihangaisha." Akamwambia: "Kama minazi nakuhangaisha yote itakatwa." Basi, ile minazi yote ilikatwa. Akasema : "Ah!" Hata pale tena siku ya sita ile akaja:

Tu FJ1 F "Aliyelala nani",Maana kwa ukali yule Pande atishike: "Aliyelala nani, aliye macho nani?"

Tu WE F "Ni mimi Ngeko, Kibwana Upande, ni mimi Ngeko, Kibwana Upande."

Tu FJ1 F "Wewe Pande hulali, kwa nini?" -"Bahari inanihangaisha". Maana tena hana cha kuzulia. "Bahari inanihanganisha, inanitikatika, chango zote zinaja juu na chini!" Akamwambia: "Kama bahari inakuhangaisha, kesho yote itakaushwa." Sasa hata yunju, ile bahari yote ilikauka, mana tena hapa hapana njia. -"Isipokuwa tena nitafanya kazi yangu, nikawalye wale." Sasa pale, akawambia wenziwe: "Mna habari?" -"Mpaka hivi, sasa tunaja ligwa ni jini." -"Mwanaharamu huyoo, nuhusi halina mana kwanza nuhusi. -"Tulyambili hili hela lisije lina nuhusi." Kabla vile bahari kwanza hayafun-- haya--

Tu NM1 F Haijakaushwa.

Tu FJ1 F ...hayakaushwa, akawambia:"Kama miye nawanuhusi kwa vile ni wa Upande, Mwenyezi Mungu kaniumba Upande 'ngoiani sasa'." Kila mmoja samfunga shuka yakwe, hapo jini litapokuja, mtu asijesema akaja nichimbka roho yangu.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Sasa pale, hata usiku wanasikia kishindo kinakuja: vuuuuu, kabla jini halijafika lile wo-- akaanza kutingisha kile kishuka. Kila mmoja akaamka. Akamwambia: "Mnyamale kimya, msije nikakuligwa hapo." Kanasikia:

Tu FJ1 F "Aliyelala nani, aliye macho nani."

Tu WE F "Ni mimi Ngeko, Kibwana Upande, ni mimi Ngeko, Kibwana Upande."

Tu FJ1 F "Wewe Pande hulali, kwa nini?" - "Mbu wananihangaisha." Akamwambia: "Mbu wote leo, watakufa asubuhi." Hata lile jini lilipoenda zakwe na wale, wakasema: "Mpaka hivi sasa bwana Pande, tunakuangukia." Hivi sasa, bwana Pande kutawawe ndo nahoza. -"Je, bwana Pande, twende bandari gani hivi sasa. Akawambia: "A'a. Miye mnyonge hapa. Kila kitu Mungu kaniumbu Upande. Wala sina nnalyo kweza hapa. Sina sina kazi yo yosi." -"A'a, wewe tena kutakuwa ndo bwana mkubwa humu chomboni." Akawambia:"Sasa kama ndo hivyo, sasa hapa tuukeni, twendeni bandarini, nmana lile jini leo lilivyoaga, leo nyoti mtakufa, mtaligwa." Sasa pale, wakaondoka pale bandari ile ya jini, wakenda zao kwengine, hata lile jini lipokuja wale, hawapo, washakwenda zao.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Wakarudi kule kijijini, yule bwana huyu, Kibwana Upande akapewa ufalume, ni yule nahoza, tena ule bwana Upande aka ... nahoza, na hadisi yangu ikaishia hapa.

Tu NM1 F Ikashamaliza.

Ki JM M Hadithi nzuri kabisa. Lakini walirudi namna gani kijijini wakati

Tu FJ1 F Walirudi kijini!

Ki JM M Wakati jini limemalizka maji yote ya bahari?

Tu FJ1 F Ehee, tena kabakia pakavu yule jini. Kwa maarifa ya Kibwana Upande. Maana ndo amewanusuru wote wale wenziwe wale yule Kibwana Upande. Wakati ndo anayesema na yule jini wenziuwe huwa hawana habari.

Ki JM M Ahaa, kwa hiyo, ikawa sasa maji yaliletwa tena.

Tu FJ1 F Kabla hayajakauka yale maji, walianza kuki-- akawakimbiza wale wenziwe yule Kibwana Upande.

Ki JM M Ahaa.

Tu FJ1 F Apokuja jini kanaikausa ile bahari, hawapo wale, eshatoweka wamenda zao.

Ki JM M Ahaa. Halafu... halafu "fogonyani" ?

Tu FJ1 F Fogonyani... kile chombo kile, kuna tezi kule. Sasa huko tezi kunakoo kichochoroni huko ndo fogonyani.

Ki JM M Fogonyani. Halafu, "kuzamka" ndo kufanya nini.

Tu FJ1 F Kavuzama, kavu kajifichi, maana.

Ki JM M Halafu.. "chango", "aligwe"... "Aligwe" ni nini?

Tu NM1 F Kuliwa.

Ki JM M Aliwe, niyo shetani.

Ki JM M Aa, na "bwanda"?

Tu FJ1 F Nguo, ya kiume, ndo bwanda. Ehee. Ile nguo ya kiume ya kazi ile ndo hwitwa bwanda.

Ki JM M Asante sana.

(interruption)

Ki JM M Mh...

Tu HG1 M M Fogonya - ile kando kando ya jahazi.

Ki JM M Mh.

Tu HG1 M M Unaona, kwenye sehemu ile ya gidamu ile. Baada ya ile staha ya gidamu ile.

Tu XX F Sitaha ni gari kesha tajiwa.

Tu HG1 M Huko chini huko. Mbele lakini, sehemu ya mbele. Kule fogonyani. Sasa ikiwa kwa sehemu ya tezi, huwa banduruni.

Tu FJ1 F Paukwa...

Tu WE F Pekawa.

Tu FJ1 F Hapo zamani za kale...

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Kavuko babu mmoja.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Huitwa bwana Upinde.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Sasa bwana huyo ni mtu mzima katika mji.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Akakaaa na wanaweee, mpaka akawa mtu mzima kabisa.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Sasa wale wanawe, wesha kufa. Wakabaki wajukuluze.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Wapobaki wajukuluze, ikawa wale wajukuluze wanakimwa sasa kumlisha. Maana wanachoka kumlisha. Sasa wale-- yule babu akenda omba kama hivyo, jahazini yaani: "Nipate kulya, yaani sitaki kufanya kazi, lakini nigawile kulya tu." Sasa apokwenda kule jahazini, yule nahoza akakatala. Apokatala, na wale mabaharia vile vile wakakatala, kama mfano wa ile ya mwanzo.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Sasa, akasema nywie leo mnavyojaliwa, lakini chombo hicho niwamo.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Sasa wakenda zaooo, hata watapokwenda, hata wakati wa kupakua kitu, chakulya mle chomboni. Kila mtu hataki babu hilyoi kongwe hata kufula halifulu, hata makucha halikata, makucha yamerusi mikwembe...

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Linanawa mate, "miye sinalya nalyo". Sasa lilipakuliwa kibati akagelewa huko, cha ugali...

Tu NM1 F 'Sa kwisha sahou.

Tu FJ1 F Sasa pale, wakenda zao, hata kufika baharini hivyo siku hizo, kuvu na yale majahazi ya Wamanga yale, ya matanga sita. Sasa wakenda zao, kile kibabu hukitiliwa upepo kusudi kile, mana kipate kitishike.

Ki JM M Mh.

Tu FJ1 F Na ile safari akaitaja: "Ve, kama fanyani hivi, katakwambiwa toka veye usafiri wa zamani siye hatuutaki." Kunatwambia usafiri wa kizamani, pumbavu nini weye.

Ki JM M Ee.

Tu FJ1 F Sasa pale, akaja shika kamba, kananyang'anywa ile kamba. Akashika kasia kananyang'anywa. Hata huko usoni, Mwenyezi Mungu kanataka kulamula haki sasa. Lile lauya jombo lya Wamanga lina matanga sita, na kile chao vyo, kina tanga moja. Sasa ikawa na siku hizo Wamanga, na Waafrika wavu wakachukulwa wakawa ni Wamanga wakawkapilika huko kwao. Sasa pale, akawambia yule babu: "Kuja tazama hivi kanaliona lile jombo linakuja lya matanga sita." Na wale wapojanua macho, jombo lile, na bila shaka linatufuatia swiye.

Ki JM M Mh.

Tu FJ1 F Sasa wakanza kwenda kwa kile kibabu walichokichukia. "Babu, we ndiyo mzee wetu humu chomboni." Jombo lile lya Wamanga linakuja, na bila shaka lile linatufuata swiye. Linatukwama lile lije

liwaje watuchukule. Akjawambia: "Aka! Miye nimtendeni vipi! Miye hapa sina nyezalyo, miye hapa mkongwe ya Mungu, miye hapa mjinga, mjina wa wajinga ni hapa nilipo, nisamtendani vipi, na wale ndo weshafika. Aa, babu tufanyile maarifa, sasa wananza kutetemeka. Babu, tufanyile maarifa." Akawambia: - "Miye sina maarifa hivi sasa. Ngojani jombo lile lije mchukulwe."

Tu FJ1 F Sasa wakakaa lile jombo sasa kila mtu kanatetemeka hawezi kufanya kazi yo yosi. Sasa lile jombo limekuwa hatua, sasa wanaona na wale ndo binadamu na hawa huku wanaona wenzao wale ndo binadamu. Linakuja. Sasa yule bwana mkubwa aliwambia hivi: "Mnasikia, mpaka hivi sasa lile jombo lina matanga sita, na linatufata siye pamoja na miye. Lakini sasa kila mmoja avimbe. Nyoo chukulani makasia na wengine ma-- pondo, mchukule pondo, na wengine, hata mkaliona linataka wakaribiani nyoti mvimbe mlizuwile lile jombo mtende: 'Joooshi!'" Sasa, kufika pale lile jombo lishawakaribia, wanakwona wamavimba wale na mikasia, washika, jooshi! (kicheko)

Tu FJ1 F Ile jooshi mjombo ulikwima, na ule wa matanga sita kule ulikwima. (kicheko) Upokwima ule, aliwambia vino, wale Wamanga: "Mpaka hivi sasa wale chombo kidugu, kisha soza pale, kishapwewa, na siye tukawakimbilia wale tutapewewa. Heya, tusiye tuzinguluke. Sasa wale wa matanga sita wale..."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F ...walianza kukisi wale, woote wenda zao, wanapita chi kwa chi huko, julu kwka julu, kwa julu hata wapojaaa...zima wale na wale wakatweka wakenda zao. Na hadisi yangu ikeshia hapo.

Tu XX F Haya!

Ki JM M Asante. Ehe, "kwembe" ni kitu gani?

Tu FJ1 F Kwembe? Zino, zino zino kucha, zino ndo kwembe.

Ki JM M Asante.

(interruption)

(kicheko)

Ki JM M Ehe. Sasa hadithi hii inatufundisha nini?

Tu FJ1 F Hadisi hii, inafundisha pahali pasipo mzee, hapafanikiwi na kitu cho choti. Isipokuwa panapo mzee mana mzee, ndo mwenye maarifa mengi, ya baharini, ya nchi kavu, ya porini, ilimradi ukapitika unafanya neno baya anaweza kukwambia, hili usifanye, ndo mbele hivi sasa ni nzuri lakini mbele yake, itakuja kuwa na hasara. Hiyo ndiyo mana yakwe. Na hiyo ingepitika na hasara, kama si huyo mzee aliyekuwamo. Lau mzee asingekuwamo ndo wangechukuliwa na jahazi ikafa.

Ki JM M Ahaa. Asante. Kwa hiyo, penye wazee haliharibiki neno.

Tu FJ1 F Ehe, haliharibiki neno.

Ki JM M Ahaa, asante.

Ki JM M Karibu.

Tu FJ1 F Paukwa.

Tu WE F Pekawa.

Tu FJ1 F Hapo zamani za kale,

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Alikuweko bwana mmoja.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Alieshi kijijini, akawambia wale wenziwe...

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F "Mimi naweza kusema, naweza kufanya mbinu, mpaka nikajipatia mapesa...

Tu NM1 F Mh.

Tu FJ1 F Ya kueneza katika mji huu.

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Akambiwa: "We ni walezi wo weye ukajaliwa ni Muyungu, hutatueneza mapesa wala huna ya kwenda mnyang'anya pesa, maana huna kazi yo yosi."

Tu NM1 F Ehee.

Tu FJ1 F Akawambia: "Nani?" Basi, hapa sakuja na mapesa kwa magunia kijiji hiki.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa yule bwana, alenda jenga kibanda chakwe kooo, kando ya msitu, yaani njia ya kwendela watu visimani.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa yule bwana, apojenga kiti kibandra cha makuti, alikusa makaratasi mengi, akayakata uzuri, kama misahafu...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F ...na juzu zile. Halafu julu akabandika ile misahafu ambayo ya kikwelikweli...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F ...na juzu. Akazijaza kile kibanda cha makuti tele!

Tu NM1 F Ee, ee.

Tu FJ1 F Akasema: sasa nataka ninyang'anye watu pesa, na watazitoa kwa hiari yao.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Sasa yule bwana, akatafuta mrifau wakwe...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F ...na mkeka wakwe mweupe...

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Apokwisha, akatandika pale njiani karibu na njia hiki ya kibanda kando hivi, sasa vyakakaa karibu na kibanda hivi.

Tu XX F Kutafuta ...

Tu FJ1 F Sasa, akaweka ule msahafu wakwe juu ya ule mrifaa ule.

Tu NM1 F Ee.

Tu FJ1 F Akawa yule bwana kanasoma. Husoma hata kuona watu wanapita, katasoma hata sharti aitike "Labeka!" Asume, asome. "Labeka!" Asume, asome. "Labeka!" -"Mola wangu unaniita, nije nifanye nini?" Sasa, hata akaja bwana mmoja akamwuliza: "Mbona we unasoma halafu unaitikia, unaitwa na nani?"

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akamwambia: "Miye, nakwitwa ni Mwenyezi Mungu kule kibandani ndo aliko..."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F ...lakini huyo Mwewnyezi Mungu, ukamtaka umwone, ukawa mwana ya haramu hutamwona."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F "Ukawa ya halali kutamwona."

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa, samwona vile - toa pesa hapa, tia pesa hapa kikapuni, halafu ukafika humo kibandani kutamkuta huyo Mulungu kakala shi.

Tu XX F Allah al Akbar!

Ki JM M Kakaya chi?

Tu FJ1 F Kakala shi. Sasa, watu hungia mle nyumbani. Vule kibandani wanamwuzwa yule Mwenyezi Mungu, hawanamwona, sasa: "Ah, pengine kwa vile sikumwona miye mwana ya haramu." Sasa akarudi yule mtu aloingia mle kibandani, humwuzwa: "Je, umemwona Mwenyezi Mungu?" -"Ndiyo bwana nimemwona, maana asiye hivi atakwambiwa yule ni mwana wa haramu." Sasa watu wakaja hivyo hivyo mpaka watu wakasikia ule mlingano kawia huko kuna Mwenyezi Mungu anaonekana. Kuna bwana mmoja kawekwa ni Mwenyezi Mungu, kazi yake kusoma na kuitikia, kusikiliza amri za Mwenyezi Mungu. Sasa pale akakaa wakaja watu wengine pale wa kiume. -"Ah, Labeka!" Mwenyewe husoma pale msahafu wakwe kesho huitikia: "Labeka! Labeka!"

Tu FJ1 F Sasa pale wa kesho: "Ah, bwana unasema na nani? Nasema na Mwenyezi Mungu, si mnguanayetaka kumwona aingie humo kibandani atoe pesa hapa, halafu aingie humo kibandani. Sasa watu wanamimimonia mapesa pale vi (?) wanaingia mle kibandani. Wanaona matabu mengi, na misahafu. Sasa pale hutizamizama hata wakawona hawanamwona wanatoka nje.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Je, umemwona bwana? Ndiyo bwana nimemwona. Nimemwona bwana. Sasa watu wanambizana maana akiwa hamwona ah, akasita asema akaja haja hambwa miye ni wa mwana ya haramu.

Tu N M F Ehe.

Tu FJ1 F Sasa akakaa hivyo hivyo mpaka wakawa wanangia mpaka wanawake. Wanangia mle. Wakatizama hawanamwona yule Mwenyezi Mungu. Lakini wakatoka yule bwana anawauliza: "Je, umemwona?" -"Ndiyo. Nimemwona." Maana asiyemwona atakuwa mwana wa haramu. Anayemwona ndiye wa halali. Asiyemwona wa haramu. Sasa wakaendelea watu hivyo hivyo mpaka akapata mapesa mengi akawa hatasiku ile kanataka kupunguza zile pesa kwenda nazo kule nyumbani kwao.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akawambia, kesho Mwenyezi Mungu kanituma sehemu fulani nende, kuna laika mwingine 'nda mjuwilisha ujumbe.

Tu NM1 F Ehe.

Tu FJ1 F Akambiwa, haya, na siye tutakuja hapo utakaporudi. Akawambia: "Sitachelewa asubuhi ya pili 'sarudi." Akenda weka mapesa yakwe, pale apokwisha akarudi. Akanza kazi yake ile ile: "Labeka! Labeka! Bwana nataka kumwona Mwenyezi Mungu." -"Tia pesa hapa, nenda kibandani ukamwone Mwenyezi Mungu. Lakini usipomwona utakuwa mwana wa haramu." Wakaanza kwenda wanamiminika watu kwka wingi kila mtu kamtaka kamwone Mwenyezi Mungu. Na hakuna a--

Tu NM1 F Haijatokezea mtu akasema mimi sijamwona.

Tu FJ1 F Hakutokezea maana aogopa kuwa yule, mwana wa haramu. Hata apokwisha pata mapesa yale kwa wingi, sasa hana pa kuzifanya, akaaza kuhamisha kile kibanda chake. apoaanza kuhamisha kile kibanda chake, akenda katika mji. Akawambia: "Je, yale tuliyoambizana siku zile mna ya kumbuka?" -"Kama yepi bwana? Mmesema siwezi kuwanyang'anya watu pesa, isipokuwa nyende hachume kwa nguvu zangu. Hizi nizipata wapi?" Sasa wale hawana njia ya kumwulizia kama ulizipata kivipivipi mana hakufanyia kijiji kilechawe.

Ki JM M Hawajui?

Tu FJ1 F Ee, hawajui. Tena ndo akaweleza: "Basi, mimi nimekwenda kufanya kazi fulani, nimejenga kibanda, nimefanyieni, nimeweka misahafu, juzu, mirifau, mikeka na mwenyewe nkaweka kiatu kizuri cha kubazi hapo chini ya mkeka." (kicheko). Anayekuja na mwambia: "Ngia kibandani ukamwone Mwenyezi Mungu ndo aliko. Na asiyemwona Mwenyezi Mungu, huyo ni mwana wa haramu. Na wote hawekubali waitwe ni wana wa haramu, wote walikubali kuwa wao ni halali. Sasa hapo nami ninshakwenda zichukua hizo pesa. Atakayeniweza mimi ni nani hapa." Akakambia: "Kwa njia hiyo umayoitumia hakuna mtu akuweza weye hata mmoja." Na hadisi yangu ikeshiya hapo.

Ki JM M Nzuri sana. Mhuu, na hiyo inatufundisha nini?

Tu FJ1 F Inatufundisha nini? Hii, inatu-- haitufundishi endeleva mambo mabaya. Mana hawa vijana wetu kunako kaka zetu, ndugu zetu, watoto wetu, wanatumia njia sana wanaweza kwenda mwambia mtu: "Nipa kiasi fulani nimeweka mzigo fulani, 'nda nunua, nikeschauza nakuletea p'sa zako." Ndo kimoja hizo huzono.

Tu HG1 M Kuna njia ya pili pia inafundisha.

Ki JM M Ehe?

Tu HG1 M Lipo fumbo fulani mie nimelikuta

Ki JM M Ehe?

Tu HG1 M Fumbo lenyewe, binadamu ye yote, hasa kama mkamilifu hapendelei kupatwa na aibu. Huwa lazima...

Tu FJ1 F Na hao waliogopa hivyo, wasije mawawili wanaogopa kuwa kama, mimi sikumwona. Fulani we mtoto wa haramu, sasa kila mmoja katika mji, mwana wa haramu yule mwenyezi Mungu hakumwona. Kenda kwa Mwenyezi Mungu na yeye hemwona yule, mwanaharamu yule. Sasa kila mtu alijisitiri na jina baya lya kwambiwa mwana wa haramu.

Ki JM M Ahaa.

Tu HG1 M Imo mantiki humo. Imo mantiki ndani yake...

Ki JM M Imo mantiki.

Tu HG1 M Na muundo kama mfano wa hadisi ya Abduli kama umeisoma...

Ki JM M Ee, ndiyo.

Tu HG1 M Unaonaje?

Ki JM M Muundo ni kama ule.

Ki JM M Aa, nina maswali machache ya kukuuliza. Swali la kwanza ni hilo, kwamba hadithi, mlikuwa mnasimuliwa wakati gani wakati huo wa utoto wenu? Wakati wote wa siku au wakati maalum wa siku?

Tu FJ1 F Usiku, tunawinga shamba, muhindi.

Ki JM M Ahaa.

Tu FJ1 F Huwa tunawinga, mana huku kaye, hetuja tukaja mpaka watu wavune. Sasa tukafanyiwa mambo ya haya ndo tunabembelezwa menake tusije taka kuja huku katika mji. Mana tunagoja bibi he, jioni pana ngano nzuri hapa ukenda kaya hunaja sisikiya.

Ki JM M Ahaa.

Tu FJ1 F Tena ndo tunaja jalika tuvika shamba heya tupate hayo mambo hayo.

Ki JM M Ahaa. Ndiyo. Na alokuwa akisimulia ni nani?

Tu FJ1 F Ambaye kesho kufa, nikwambili jana.

Ki JM M Ah, kwa kawaida, ni watu gani walikuwa wakisimulia?

Tu FJ1 F Huko ni kwa hadisi ati huku kavuko bwana mmoja Haji Hamadi haya kisha kufa. Na bi Kidu Shaha, yaani ni mama mkulu. Ndo waja wakatuzungumzia hivyo.

Ki JM M Ahaa. kwa hiyo, wanaosimulia, au waliokuwa wakisimulia ni wale mama vizee.

Tu FJ1 F Ehee, mama zetu, yaani makamo kupita hao mama zetu.

Ki JM M Ahaa. Ndiyo. Waliwaeleza wakati huo kwamba hadithi hizi zilikuwa zinatoka wapi?

Tu FJ1 F A'a, hewaja wakatwambila. Tena tukeshafanyiwa ja hivyo kama panapigwa na kingoma wenyewe tunacheza tena ikesho tena, hivyo basi.

Ki JM M Ahaa.

Tu FJ1 F Unakweza vishaga vyetu, tunalala.

Ki JM M Mh. Ah, asante. Au mzee Haji ulikowa una lo lote la kuongeza kuhusu namna ya masimulizi.

Tu HG1 M Cha kuongezea sina, isipokuwa simulizi zilielezwa sehemu tafauti kama hizo. Kwa mfano, kama vile makondeni, isitoshe. Kambini kwa mwavuvi. Pia zilielezwa hadithi tafauti baada ya usiku watu weshakula mihogo yao, basi hokusanyika wakakaa kitako, kila mmoja akataka kushindana na mwenzake. Yule akitoa chuma hiki, huyu anatoa hiki. Isitoshe, mpaka wakati tuko jandoni, pia wale wauguzi wakitusimulia habari kama hizi. Kwa hivyo, bila shaka hadithi au ngano, kwa huku kwetu utumbatuni ilikuwa ni tumbuizo kubwa sana zilizosafiriwa kwa muda mrefu, kwenye sehemu kama hizo.

Ki JM M Na kawaida hii ya kusimuliana hadithi bado inaendelea mpaka siku hizi?

Tu FJ1 F Mpaka kesho kutwa, inaendelea.

Ki JM M Mpaka leo hii!

Tu FJ1 F Hii leo nakwambia ukakutka humo wamo kaa chi kutasikia wanatenda ja hivyo. Lakini huwezi kuwatambula ja veye. Mana siku hizi ile mikusanyiko ya kukala nje, hakuna. Isipokuwa yenyewe ja nyumbani, mfano, sasa huwezi kumjua nyumba gani inafanywa mambo hayo.

Ki JM M Kwa hiyo, zamani ilikuwa ni huko--

Tu FJ1 F Zamani nje, za wazee, siku hizo za wazee walipokuwa wengi wale wazee, nje. Ni usiku kama huu wa mwezi, ndo huwa zaidi watu, kila wanapokaa watu wanafanya. Wengine kutasikia wanaimba. Zikishatolewa zile ngano na bibi zao, wengine wanacheza wanakpigiwa na vigoma. Maana kila hadithi, inaletwa na mambo yakwe na pongezi zakwe. Nyingine za kukaak hivi hivi, tu nikasiliza tu, nyingine mnaimbka halafu mnacheza, ndo ilivyokuwa hivyo.

Ki JM M Na vigomo walikuwa...

Tu FJ1 F Na vigoma vyetu vya videbe, tunapiga.

Ki JM M Ahaa. Na siku hizi limekuwa ni suala la familia.

Tu FJ1 F Ehee.

Ki JM M M Kila familia, ina mambo yake.

Tu FJ1 F Ehee. Mana tuvua na michezo mingine wenyewe, ja hivyo siku ya mwezi tunakweza michi yetu ile. Na vifulu, tunapiga ponda tunaita ngoma yetu ya ponda. Yaani michi mine na vif...(?) tunapiga, tunakwimba, tunacheza. Huo huo mchi huo, ndo njia ya kwenendela mgulu hiyo. Huku unarushwa we huku wapanda juu ya mchi tena kunacheza.

Ki JM M Alaa. Na unaweza kuwacheza mpaka...

Tu FJ1 F Hivi leo na upangwe utaniona nnavyorukaruka!

Ki JM M Asante.

Tu XX F Halooo! (kicheko)

Tu FJ1 F Na huku tunaimba:

Tu FJ1 F Nipike ubwabwa,

Tu FJ1 F nchanganyile choroko,

Tu FJ1 F mkubwa ponda,

Tu FJ1 F Mweka uno katoroka pa - pa - pa!

Tu FJ1 F Tena hivyo tunaruka.

Proofread by MP

Edited by TR in October, 1996

DAHE 86

Place: Pemba

Time: --

Interviewee(s): 1. (MC2), 2. Unknown (XX)

Interviewer: Mlacha (ML)

Recorder: Sony Professional

Language: Standard Swahili (Ki)

Topic: A story about a king and a rich man.

NOTE! End of the story is on another DAHE, which is written on paper but the cassette in question has not yet been found.

Ki ML M ... weza kudupatia hadithi nyingine kama unatupatia sasa ile ilipopita, hivyo nafikiri moja kwa moja tunaweza kuanza na hadithi yetu.

Ki MC2 M Hasante sana. Tayari, nianze?

Ki ML M Tayari.

Ki MC2 M Zamani alikuweco mfalme na tajiri, lakini huyu tajiri Mswahili, huyu mfalme Mwarabu. Hapo walifanya urafiki. Walikuwa rafiki kwa mfalme hakilii kama hajafika tajiri na kwa tajiri vile vile hakilii kama hajafika yule, mfalme.

Ki ML M Sawa.

Ki MC2 M Sasa waliendelea hivyo hivyo mpaka wakajibaini hivi sasa, kwa muda tuliokaa hatujapata mtoto na wake tunao, sasa tufanye maarifa yakutafuta mtoto. Alitoka mfalme kwenda kwa tajiri kwa kwenda kumweleze hivyo kwasababu alifikiria peke yake kule nyumbani. Na yule tajiri yule-- na yule tajiri keshafikiria kwenda na swala hilo hilo kwa mfalme. Walikutana njiani. Huyu hajafika kwa tajiri na huyo hajafika kwa mfalme wakakutana hapa katikati.

Ki ML M Ndiyo.

Ki MC2 M Walipokutana: "Salam aleiku, aleikum salaamu, habari za siku salama, eh bwana, nakusudia kwako." Amwambia: "Na mimi vile vile nakusudia kwako, ee nini haja yako?" Amwambia: "Tende zetu nyumbani." Sasa walifatana. Tajiri na mfalme wakenda kwa mfalme. Kufika kwa mfalme amwambia: "Bwana mimi haja iliyonitoe kwangu kuja kwako. Ni kuwa kwamba maskitiko yangu mie, mimi tajiri weye mfalme lakini mambo yetu haya yote hayana maana. Ufalme wako hauna maana na utajiri yangu hauna maana. Kwa sababu mimi muda wangu ni mfupi kwa makamu ndio nayo. Na mimi-- na wewe mda wako mfupi kwa makamu uliyonayo. Lakini hatujapata mtoto. Sasa kama utajiri wangu mimi sina mtoto, nikiondoka mie utapotea tu. Na ufalme wako vile vile, ukiondoka wewe uta-- utapata watu mbali. Sasa isipokuwa tufanye rai, twende kwa wata'alamu watu saidie maarifa ya kupata mtoto."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 H Hapo alimwambia: "Basi na mimi hilo ndilo lililonitoe. Kwangu kukujia wewe tukakutana njiani. Sina mengi mie kusema isipokuwa kushamaliza. Sasa wasemaje?" Amwambia: "Kesho asubuhi tukijaliwa tuondoke. Wala tusende mahala fulani tunapopata mbua. Tuende tu kutafuta. Kwasababu hatupajui wapi tutapata lakini isipokuwa tuondoke hapa kwa kukusudia kutafuta, kama tutakapopata ndio tushabahatika."

Sasa walichawalikia na kila mmoja akenda kwake, shauri yao shapanga kesho. Walikaa hata asubuhi mapema, mfalme alikwenda kwa tajiri. Kufika amwambia: "Bwana ile safari yetu tayari." "Tayari?" "Ehe, tayari." Sasa walitoka. Walitoka wakenda zao lakini hawajui tunamwendea nani.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Wanakwenda tukakutafuta. Walikwenda zao lakini nchi zama bara mizitu mapori mengi. Waliingia porini. Tuseme kama hapa mpaka ntambile wanapita kwa ndani ya mapori hawajakuta mji. Hata walipokuta mji, huko huko ndani ya pori walikuta kijiji ambacho kina nyumba moja tu na hiyo nyumba moja, gorofa moja. Walipiga hodi. Walipopiga hodi, mle nyumbani mulitikia mtu, lakini mtu mwenyewe zimwi. Huyu mtu alieyetikia zimwi. Maana zimwi sijui tunamfahamu?

Ki ML M Ndiyo.

Ki MC2 M Tunamfahamu zimwi ee?

Ki ML M Ndiyo.

Ki MC2 M Hapo alipoitikia zimwi, aliwakaribisha. Kuwakaribisha wakakaa kitako barazani, aliteremka zimwi, aliwauliza, kufika yule zimwi pale aliwauliza: "Je, mfalme na tajiri nyinyi mnakwenda wapi? Mbona mnafika hapa pangu mnapiga hodi mnanijua mimi nani? Mimi nawajua wee mfalme, wee tajiri. Lakini mimi mnanijua nani?" Asema: "Sisi tunakujua wewe binaadamu kama sisi. La, hatukujui wewe nani kama unavyotujua, lakini tunakujua wewe binaadamu kama sisi." "Haya, basi karibuni, wakakaa kitako." Walipokaa kitako zimwi yule alikwenda pika chai akawaletae, wakanywa. Kishakunywa awaambia: "Hebu semani haja zenu."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Asema: "Sisi haja zetu hatuwezi kumwambia mtu. Isipokuwa huyo mtu afanye ujuzi wake atuambie yeye mwenyewe hiyo haja yetu. Sasa hapo tutamtaka kuwa awe mtengenezaji wa haja yetu." Zimwi aliwaambia: "Wee mfalme na wee tajiri kula mmoja nyumbani kwake alikusudia kwenda kwa mwenziwe. Mlikutana njiani. Mlipokutana njiani, na hiyo haja mnayofatiana ni kuwa hampati mtoto. Nyote hamna watoto na haja yenu watoto. Mwende, mwondoke majumbani kwenu, mwende mkatafuta watoto. Na hii ndio haja iliyowaleta hapa. Je, sikweli?" Asema-- asema: "Hiyo kweli." "Sasa basi kama kushajua hivyo tunakuomba ututengenezee haja hiyo kama unajua." Asema: "Mimi najua lakini nashuruti." "Shuruti yangu naweza nikawatengenezea mpaka mkapata watoto na watoto mtakao wapata wanaume. Lakini shuruti yangu, wenenu mtakapozaa wewe mfalme mwanao mwite Usi. Na wee tajiri mwanao mwite Usi? Je, mmekubali?" Hapo mfalme alisangaa kidogo lakini yule Mswahili akakubali. Asema: "Mimi nakubali."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M "Mwanangu ntapo mzaa nimwite Bwana Usi. Je, wewe mfalme unakubali?" Alimwambia: "Nawee kubali, kamwambia namii nakubali. Na mimi mwanangu ntamwita Usi." Kwa sababu kanaona kinyezi yule Mwarabu mwanawe kuja akamwita Usi. (Kicheko)

Ki ML M Na Usi si jina la kiarabu?

Ki MC2 M Usi si jina la kiarabu.

Ki ML M Na mfalme alikuwa Mwarabu?

Ki MC2 M Na mfalme alikuwa Mwarabu.

Ki ML M Tajiri alikuwa mweusi?

Ki MC2 M Ehe. Tajiri alikuwa Mswahili. Sasa kwa-- kwa Mswahili kumwita mwamawe Usi si chochote.

Ki ML M Eee.

Ki MC2 M Lakini Mwarabu kuja kumwita mwamawe usindo, a'a halifanani.

Ki ML M Ahaa.

Ki XX M ...?

Ki MC2 M Ehe. Hapo walikubali, lakini kukubali ya mfalme kijuujuu. Kwa sababu yeye Mwarabu vipi mwanawe aje wee Usi. Kijuujuu kabisa kukubali yake ah! Si-- si kwa furaha. Walimwambia tumekubali bwana.

Ki ML M Sawa.

Ki MC2 M Alitoka. Alijitia ndani yule zimwi alikwenda akachukua panga.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Panga maana perezi kwa jina jingine. Kwa majina mawili hamnajua(?) lipi zaidi?

Ki ML M Panga.

Ki MC2 M Panga. Alikwenda kuchukua panga. Akaingia ndani ya pori. Alikwenda-- alikwenda panapo mti anaoujua yeye. Alikata mzizi mmoja unaofika makamu haya. Alichimba sasa kuukuta mzizi aliukata. Unaofika kiasi zira moja. Alikuwa nao nyumbani. Kufika nao, aliukata vipande vidogo vidogo vidogo vidogo vidogo mpaka vikatokea kula mmoja apate saba tatu. Ndani ya kipande-- ndani ya vipande vile.

Ki ML M Saba tatu, ndiyo?

Ki MC2 M Maana ya vipande saba, saba mara tatu.

Ki ML M Saba saba mara tatu.

Ki MC2 M Ehe, ndio saba tatu. Na kula mmoja apate hizo saba tatu. Aliukata kidogo kidogo kidogo kidogo kwa kuwa nia ya kula mmoja apate saba tatu ndani ya mzizi huu huu. Aliwapa. Amwambia: "Wee ukifika nyumbani huu umpe nkeo." Lakini iwe "time" uzakuwa hamtakula tena mshakula ki-- mshakula chajioni maana hamli tena. Isipokuwa kuna kulala tu. Sasa mpe hanjike hii halafu anywe upawa mmoja. Na nendo vile vile. Na hii dawa hii, inyewe kwa muda wa siku saba. Ikimaliza siku saba basi. Sasa mutakaa muda wenu miezi mitatu mj... m... bieshe vipi? Tumefanikiwa au hatujafanikiwa. Wanaambiwa wale watafutaji wa watoto. Walichukua, walikwenda zao. Kufika nyumbani wakakaa hata "time" za kutaka kulala waliwapa akamwambia hii nenda kaichemsha ee. Wakenda wakaichemsha wale wanawake, halafu wakaja-- wakamwambia, sasa, hii dawa hii kwa muda wa siku saba, kula siku moja uje(?) upawa mmoja unapotaka lala. Kazi yao ikamaliza. Sasa wale wanawake hawajaambiwa, lakini kwamba hii dawa tunatafta mimba.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Wale wanawake ikawa kazi yao hiyo. Wanapotaka lala hui-- hui-- huichemsha ile halafu wakanywa. Hata kufika ile miezi mitatu, bahati nzuri yule-- yule tajiri yule aliona mke wee tayari sasa. Ile mimba ile, tayari.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Alitoka sasa. Kwenda kwa nani, kwenda kwa mfalme, kwenda kumwambia kwamba mimba tayari kwangu. Na yule mfalme kwa siku ile ile aliyobaini yule mwenzie naye mfaini-- mfalme yule ali-- alibaini kwamba mke wangu tayari sasa mimba. Naye alitoka walikutana pale njiani wakutanapo pale.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M "Bwana wee, mie nakuja kwako na amwambia: "Na mimi nakuja kwako." "Wee haja yako nini?" Amwambia: "Twende nyumbani." Siku ile walikwenda kwa tajiri hawakwenda kwa mfalme. Kufika kwa tajiri amwambia: "Bwana haja yangu nayojia nyumbani? Naona kama ile haja ...etu inataka kuwa. Kwasabu naona mke wangu tumbo linakuja juu." Amwambia: "Na mie ilikuwa nakuja kukuambia hayo hayo." Sasa kwa hivyo tuliambiwa: "Ni yule Bwana Usi twende tukamjibishe." Yule mfalme alianza matatizo amwambia: "Mimi-- kwenda nnaona uzito sana kwa sababu yule zimwi yule bwana, tumeshaomba tumeshapata tena basi tusende kule, yule zimwi." Amwambia: "Yapo kuwa zimwi, lakini yule inasababika na yeye. Hizi mimba za wake wetu, kwa sababu tuliondoka hapa kwa kwenda tafuta tulipata. Sasa na alitupa suruti tusende vipi, twende." Walikwenda, lakini kwa kungongeza.

Ki MC2 M Kufika walimjibisha. "Bwana kwa haja yetu tuliojia hapa tunaona kama tumefanikiwa. Kwa sababu hivi sasa wake wetu tunawabaini wanatuna matumbo." Asema: "Hiyo ndio mimba hiyo. Lakini ninavyoambia, kapumzikeni wala musije(?) tena hapa isipokuwa wazaliwe hawa watoto." Lakini siku watayozaliwa hiyo siku ya pili muje. Maana kuja kuwachukulia dawa. Hawa watoto wenu kuja kuwachukulia dawa kwa sie tunaita fuo. Kumfua yule mtoto maana kumkinga-- kumkinga mabaya mabaya. Hapo walirudi wale wakenda wakakaa hata siku yakuza-- waozaliwa wale watoto. Siku ya pili tajiri alikwenda kwa mfalme. Kufika amwambia: "Bwana, mimi nimeshazaliwa wee..." Amwambia: "Na mimi nimeshazaliwa."

Ki ML M Safari hakutana njiani?

Ki MC2 M Hawakukutana njiani. Amwambia: "Sasa kama wewe umeshazaliwa na mimi vile vile nimeshaliwa tunafikira gani?" Anaulizwa nani? Anaulizwa mfalme ni yule tajiri. Amwambia: "Fikira yangu wee ukakae na mwanao na mimi nikae na mwanangu. Wewe mwanao umemwita vipi?" Asema: "Mimi mwanangu Muhammed bin Sultan."

Ki ML M Ahaa.

Ki MC2 M Amwambia: "Wee, umemwitaje vipi?." Amwambia: "Mimi Bwana Usi yule. Yule mwanangu mimi Bwana Usi. Bwana Usi makame yule."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Amwambia: "Wee mwanao unamwita jina ya zimwi, mimi mwanangu zimwiti jina ya zimwi, wala sendi tena kule-- hizo siku ndizo kwenda sendi tena kwenda kumnadisha mwanangu kwa zimwi."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo alimwambia: "Bwana twende, yule mtu alitute--alitutengenezea haja yetu hii, na alijua haja yetu bila kuipata. Na akatutengenezea ikawa sababu mpaka tumepata. Kwa kumrazau tunajua atafanya nini? Twende!" Amwambia: "Mimi sendi." Sasa bwana yule alitoka hali ya kuwa njonge sana kwa kukataliwa maana yeye nia yake ende kule.

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Kufika nyumbani kwake alikwenda. Lakini bahati nzuri kutokeza tu kabla hajasema neno, Bwana Usi kasimama nje. "Salaimaleiku aleikum salaamu. Habari za siku?" "Salama". (NOTE! It's very difficult to know who says and what and where to put the quotation marks. The storyteller is saying all of this as a one sentence.) Amwambia: "Bwana usiseme neno." Anayeambiwa yule tajiri yule. Ni yule Bwana Usi

amwambia: "Usiseme neno." Kwa sababu hunajakusema mimi sijajitambua, nimeshatambua. Wee, a-- asubuhi wa jana ulikwenda kwa sultani ukamwambia: "Twende tukajibisha kwamba wake wetu wameshazaa."

Ki ML M Huyu Bwana Usi ni yule zimwi?

Ki MC2 M Ehe. "Twende tukajibishe kwamba wake wetu wameshazaa." Alikuambia: "Mimi siwezi kwenda kwa zimwi kumjibisha, kwamba mwanangu kazaa." Ulimuliza: "Jina gani uishamwitamwan-- ak-- akakambia bw-- mwanangu Muhammedi bin Sultani. Kwa hivyo siwezi kwenda kumjibisha, wala siwezi kumwita Usi. Kama unanadisha mwanao kwa zimwi, nenda peke yako." Alikwambia: "Wewe hivyo, si kweli?" Amwambia: "Hakika. Sasa basi njoo." Alifika pale. Kufika alijitupa ndani ya nyumba yake yule zimwi. Alikwenda tafuta dawa akampa, amwambia: "Hizi nenda kampake kwa muda wa siku saba. Ukisha muosha, maji ya mwisho umpake yeye. Ukisha muosha." Maana hutamuosha tena elalale tu. Tena umpake hiyo dawa alale hivyo hivyo mpaka asubuhi, kwa muda wa siku saba.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M "Na tena, nenda kamwambie Sultani, siku atakayo ona amtahiri mwanawe, kabla hajapata nafasi muje hapa muje muchukue pambo yakuwapamba wa-- jukuu, wa-- somo zangu." Amwambia: "Ntakwenda sema", lakini bahati kukubali. Amwambia: "Wee kamwambie tusi kazi yako kukubali." Hapo alitoka, keshapewa dawa. Keshapewa na chakula chakumlisha yule mwanawe lakini ch-- kwa sultani hepewa ch-- jambo lolote kwenda kumpa. Alirudi yule, alikwenda kaa na mto-- watototo walee, wakakaa nao watoto wale, hata ilifika siku ya saba kutahiriwa. Waliwatahiri wale watoto. Amwambia: "Bwana sultani unazo habari yule Bwana Usi aliniambia, siku ya kuwatoa nje hawa watoto wetu, twende tukajibishe. Kwa hiyo tumeshamatahiri na umeshapata nafasi tunakusudia kesho kutwa kuwatoa nje hawa watoto kwa furaha nzuri nzuri. Twende tukamwambie."

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Amwambia: "Mimi sendi, sendi kabisa kabisa."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Alimwambia: "Kama huendi mimi nitakwenda." Alikwenda. Kufika amwambia: "Bwana usiseme neno lolote mimi nimeshajua. Kwa sultani umemwambia kwamba watoto tunapo watahiri wanapopoa twende tukamwambie, kwamba siku ya kutolewa nje siku fulani na kesho kuambia yeye hataki kabisa kabisa. Musha watahiri lakini yeye hataki. Lakini wewe unayetaka chukua hizi nguo nenda kampambe huyo mtoto wako. Na nnakuambia, ukisha mpamba huyo mtoto wako kakae naye mwezi mmoja, halafu ukimaliza mwezi mmoja nlete huku kwangu ajatembee. Na sultani mwambie somo yangu amlete aje atembee." Lakini ana zimwi kuwa magumu kwa kumtaka aje atembe mtoto kwa jina hetaka ende akatembee kule kabisa hatataka. Hapo alimwambia: "Hewala(?) ntakwenda mwambia." Alikwenda mwambia, mtoto wake yule alikwenda mpamba nguo kwa pale mji ule ajabu. Hapana nguo kama zile alizopambwa mtoto wa tajiri ni yule somoye. Lakini wa sultani hakupata nguo kama zile, ingawa mfalme yule lakini hakumpatia nguo kama zile. Kwa sababu zile nguo zile ni nguo za kijini.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo amwambia: "Mimi mwanangu hendi hata siku mmoja kwa zimwi, wala nguo hizo si chochote. Mimi ntampa nguo zangu. Ntamtafutia nguo za sufi, ntamtafutia fulana nzuri na shati nzuri ambazo kuwa hata na wee hujaziona hivyo hivyo. Si lazima nipate hizi. Hizo nguo gani? Sitaki mimi mwanangu kabisa, kabisa unasibiwa na zimwi." Hapo alimwambia: "Basi. Lakini asema tumpelekee somo zake wakatembee, asema hilo ndilo jambo muhani kabisa halipatikani. Siwezi kumwita jina lake nimpelekee

akatembeo hilo ndilo jambo halipatikani." Hapo alimchukua yule Mswahili akampeleka. Kumpeleka kule nyumbani alimwambia: "Haya, nenda zako huyu mwache hapa hapa atembeo kwa muda wa siku tatu njoo umchukue. Alikaa naye pale, akatembea kwa muda wa kiku tatu, akenda akamchukua mwanawe. Hapo alimwambia: "Nenda kamwambie sultani." Lakini sasa yule mtoto tayari kukaa kitako sasa. Yule mtoto wa kifalme yule tayari sasa kanakaa kitako.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Lakini hiyo kukaa kitako yenyewe, kanafanyiwa hifadhi ya kuficha hata nje hatoki kwa sababu asije kuja yule zimwi akamchukua.

Ki ML M Mhhmm.

Ki MC2 M Hapo alimwambia nenda kamwambie sultani; siku ya Jumapili, ifikapo saa sita, mimi nitakuja. Na haja nnayojia kwa sultani, kuja kumchukua somo yangu. Akataka mwambia akitaka nitamchukua asitake nitamchukua kwa nguvu. Na kama anayo majeshi aweke, anao askari aweke, kama ana bunduki akushanye, lakini siku hiyo ndiyo siku nchukua somo yangu. Kwa sababu alishindwa na nini yeye kumpata mpaka akaja kwangu na kuja mchukua, somo yangu. Hapo alikwenda kufika amwambia: "Bwana wee nimeambiwa ni Bwana Usi. Siku ya Jumapili atakuja hapa kuja kumchukua somo yake." "Asema atampata wapi? Somo yake, somo yake kazaliwa ni mwanawe yupi hapa. Hakumzaa mwanawe huyu, somo yake kwani mimi mtoto wake, hata nimzae awe somo yake mwanangu? Hampati huyu. Si Usi kamwe. Muhammedi huyu bin Sultani, vipi atakua Usi, Usi nani? Kwani mimi Mswahili mwenziwe au mimi nani. Hampati huyu naye. Kama anakuja naye majeshi wapo hapa na bunduki zipo."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo, basi. Alikaa yule Mswahili hata kufika siku ya Jumapili asubuhi mapema, lilitanda wingu kubwa ya mvua. Na wingu lililofanyika kama utasimama hapa, aliye nyumba ile pale humuoni kwa giza. Hapo ilianza kunya mvua asubuhi, mvua ililiendelea mpaka ikafika saa sita. Haijapita. Sasa kufika saa sita, ilipita ile mvua likabakia wingu. Sasa alikuja yule. Alipokuja, kama hii hapa tulipo ndio nyumba alifika kama hapo kisimani.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Kufika alianza kunadia. "Mimi Bwana Usi mvaa nguo za sufi, siku ya kufa harusi, nakuja kumchukua mwanangu Bwana Usi. Nakuja kumchukua somo yangu Bwana Usi. Mimi Bwana Usi, mvaa nguo za sufi siku ya kufa harusi. Nime-- nimekuja kwa makusudio kumchukua somo yangu Bwana Usi. Sultani kama unamfichamfiche lakini nakuja kumchukua. Kama una majeshi tayarisha lakini nakuja kuchukua somo yangu mwanao. Kama ulivyonavyo ... ya ushujaa wako tayarisha. Mimi leo lazima, lazima lazima nimchukue somo yangu." Sasa mlingano ule aliusikia yule sultani. Hapo aliamrisha majeshi jamani huyo anayekuja huyo asijike hapa. "Huyu anayekuja huyo anakuja kishari lakini asifike hapa." Walitoka majeshi wakajiandaa wakajaza risasi zao tele ndani ya bunduki. Kumg'ojea yule anayekuja nani na atapokuwa katakusudia kuja wampige.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo, alikuja. Ase-- alipiga kelele tena awaambia: "Je, sultani! Umeshatayarisha majeshi wako, mimi nakuja." Alimwambia: "Njoo, kama unakuja, njoo!" Sasa kutangulia yule, wale jamaa walilinda zile risasi lakini kwa bahati nzuri, kama risasi inayotupwa ina-- ina-- inaviya ina kubwa hapa chini. Kama inayo-- inayotolewa mle ndani ya bunduki, inafusa ina kubwa hapa chini. Haili(?) popoti.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Zilimaliza zile risasi zote zika-- zikakushanyika hapa. Maana hazi-- hazi aliki wala hazendi. Zinatoka tu. ... toka kubwa pale chini. Amwambia: "Kama unazo nyingine sultani ongeza. Mimi nakuja." Hapo alikuja mpaka mlangoni, lakini sasa ile mvua tayari inakunya tena. Hapo alimwita: "Bwana Usi, Bwana Usi, Bwana Usi mvaa nguo za sufi siku ya kufa harusi toka twende zetu." Yule mtoto, kule aliko kamatwa kule ndani kule, mtoto ambaekuja(?) hajaenenda. Kwa siku ile alifanya nguvu mpaka wakashindwa wale nikumzuia na akatoka, kwa miguu yake. Alikuja mpaka pale mvuani amwambia: "Twende zetu." Mtoto yule aliongolea usoni wakenda zao. Zimwi nyuma yule mtoto usoni.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Na zimwi mwenyewe huyo ndie yule Bwana Usi na huyo mtoto ndio yule aliyesema awe somo yake yule Bwana Usi. Walikwenda zao. Hapo akabakiwa sultani hana mtoto. Akabakia vile vile kama awali hana mtoto, keshachukuliwa ni zimwi.

Ki ML M Ndiyo.

Ki MC2 M Mtoto yule lakini wa kiarabu ee.

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Zimwi alikwenda naye mpaka nyumbani kwake. Wala nia ya zimwi si kwenda kumvumiza yule mtoto wala kumzuru chochote. Alikwenda akamlea mtoto yule- (silence)

Ki ML M Endelea tu.

Ki MC2 M -alikuwenda akamlea mtoto yule mpaka akapata makamu. Alikuwa mkubwa sasa ku-- kukumbia baleghe. Lakini kwao yule mtoto hakujui, wala hajaona watu wengine badilia yule somo yake, kwa sababu porini kule. Lakini mtoto mzuri kabisa, kabisa na anapata shiba kweli kweli mnene kajaza. Hana shida yoyote. Sasa yule mtoto wa Kiswahili huenda akatembea siku moja, mbili halafu akarudi kwao. Lakini huyu hamrudishi.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Iko siku, na kati ya nyumba ile yote yule mtoto yule, Bwana Usi, karuhusiwa kutumilia vyumba sita maana nyumba ina vyumba saba, laki katumiliwa sita akaambiwa hiki somo usijefungua, siku moja. Aliambiwa: "Yule mtoto ni yule Bwana Usi, somo hiki, chumba hiki maisha yote utayokaa usije ukafungua wewe hiki."

Ki ML M Usi ni Mwarabu au Usi-?

Ki MC2 M Usi Mwarabu yule anayeambiwa ni somo yake, usije ukafungua hiki chumba hiki. Amwambia: "Somo muna nini humu toka ... ambia usije fungua? Amwambia: "Ah, usifungue tu wee." Humu usifungue, sasa funguo huzificha saana yule somo. Hata siku moja, yule Bwana Usi zimwi yule alimwambia yule Bwana Usi mdogo. Amwambia: "Bwana Usi leo, mimi nataka kuondoka. Na safari yangu hii, sitarudi leo ntarudi kesho."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Nataukia kumchukua akamweka pale hajawahi kuondoka asirudi ikabidi arudi kesho, hajawahi. Lakini leo ndo amwambia: "Leo ntaondoka hapa na sitarudi safari yangu hii mpaka ntarudi kesho." Alimwuliza: "Unakwenda wapi?" Amwambia: "Mimi nakwenda kuwa-- kuwachukua wazee wako waje wakutizame, ulipo. Lakini si nia yake ile kumdanganya yule mtoto ndo anamwambia hivyo. Hapo alitoka, asubuhi-

Ki ML M Makame hayupo?

Ki MC2 M Nani?

Ki ML M Usi makame.

Ki MC2 M Ah, Usi makame hayupo yuko kwao.

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Yule yuko kwa wazee wake, yule hana tabu, anapomtaka wakati wote, humpata. Huyu ndo anayemficha. Sasa alitoka yule zimwi. Alikwenda zake zimwiiii, hata kiasi ya kuchukua taukia alipoondoka kutimia saa moja.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M "Yule mtoto aliona jamani huyu somo yangu, nyumba hii pendo anayo nipenda kundi ya ... zile, nitakaye nikamate nichinje, kuku nikitaka nikamate nichije, michele nipike, kula kitu mimi kanisabilia hapa nitumilie. Humu muna nini anayotaka silione. Lakini leo lazima nikifungue. Hilivyo kuwa leo harudi nikifungue hichi chumba nitizame muna nini."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo alikwenda akachi-- akatafuta funguo, akaikuta pori. Kocha nzima funguo zo-- vyote vyumba saba akazona pahala pamoja. Alikuwa aka-- akafungulia mmoja, mmoja kula anaufungua au fungui, kumbe vile wa chumba kile yule zimwi heamini aliondoka nao.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo alikwenda chukue mtayimbo. Alikuwa akaikwamiza ile kufuli akaienunua ikabanuka. Kubanuka akatoa reza kufungua ule mlango. Sasa mule ndani ya chumba muna simba.

Ki ML M Reza ndio nini?

Ki MC2 M Reza ni kile kikomeo cha mlango.

Ki ML M Ahaa.

Ki MC2 M Mwonesha hapo reza.

Ki ML M Ni kama kipi? Ahaa.

Ki MC2 M Ile ndio reza ile.

Ki ML M Ndio.

Ki MC2 M Ndo aliivuta hivi mlango ukafunguka. Hapo, kufunguka ule mlango kutizama hivi ndani ya chumba muna simba. Lakini yule simba, kafungwa kwa mnyororo wa-- wa shaba. Ule mnyonoro mara chuma laki chuma yenyewe shaba. Kafungwa baraaabara kafungwa na nguzo. Hapo aliufunga kwa nguvu ule mlango yule mtoto, kufunga ule mlango simba yule alimwambia sasa. Yule simba, alisema kumwambia binadamu." Eeh, binadamu wee. Wee Bwana Usi, hebu rudi ufungue hue mlango kwa sababu lau kama ungejua leo le-- kesho yatakayo tukuta mie na weye huu mlango ungeufungua. Na ukitaka salama yako mlango ufungue ndo upate uhai wako na kuendelea usoni, lakini kama hutaufungua mlango leo, kesho siku yamauti yako pamoja na mie unayefungia mlango." Hapo yule mtoto aliona simba siku nyingi, wanakamatwa ni huyo Bwana Usi na hawasemi, ilikuwaje huyu leo akasema. Na maneno anayosema mbona ya kitisho kikubwa sana. "Kana nambia(?) leo ndo mwisho wa uhai wangu mie na yeye, kesho sisi sote tutakufa vipi?" Alimfungulia. Ali-- alifungua tena ule mlango. Amwambie: "Wee Bwana Usi unazo habari hapaulipo huyu somoyo zimwi."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M "Huyu somoyo mie ni kwambia zimwi na mimi unavyoniona simba alinifugua huyu taukia mimi nikali kijana na akanika mata halafu kunikamata alining'oa meno." Sasa humu ananifuga humu chumbani hujaakanipa majani, hujaakanipa mbuzi mmoja mmoja kula. Lakini yeye ananifuga ... nipate kunona kabisa i-- waje wanije siku moja tu, wanipikie na wali na wenziwe waje wanije tena pamoja na weye. Na yule hendi kwenu kuwachukua wazee wako anakwenda kwao kwenda kueta wazee tuje tuliwe miye na weye."

Ki ML M Ahaa.

Ki MC2 M "Kwa sababu weye umeshanona na miye nimeshanona. Sasa kesho pata kuwa wali mwingi hapa kitoweo miye na weye."

Ki ML M Naam.

Ki MC2 M Kwa hivyo waonaje kama kutakuja ukanifungua hapa, nikakupa marifa tukakimbia. Hebu chagua wee kunifungua miye, tuka-- tuka-- tukapeana maarifa tukakimbia au kubakia hapa tukaja tukafanywa kitoweo tukaliwa wali. Mtoto yule aliona simba, hasemi, alikwenda akamfungua. Alikwenda akamfungua.

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Kumfungua amwambia: "Mimi-- mimi simba, na simba wakati wo woote kukimbia na binaadamu. Na yule simba mwenyewe, wakati wo wote anapokutana binaadamu tayari kumzuru binaadamu, lakini ninavyokwambia mimi wee siku zuru, kwa sababu mimi weye kushakuwa rafiki yangu, mwokozi wangu na mimi mwokozi wako weye. Kwa hivyo weye rafiki yangu moja kwa moja, wala siku zuru wala usiningope(?) kabisa ondoa shaka.

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Simba yule kana(?)mwambia binaadamu. Hapo alimwambia lakini na njaa kubwa sana mimi mwenzio kwa sababu leo sikuwahi kuposhwa. Nenda kamkate ngombe mmoja-

Ki ML M ... kuposhwa, kuposhwa ndiyo?

Ki MC2 M Kupewa chakula.

Ki ML M Ahaa.

Ki MC2 M Ndio kuposhwa. Amwambia: "Nenda kankamate ngombe mmoja ntamba umchinje unkatete kwa sababu mimi niling'olewa meno sina meno, umkate kidogo kidogo, uniletee hapa nitafune." Alikwenda kamkamata ng'ombe akamchinja akamletea nyama pale yule simba akala mpaka akashiba. Amwambia: "Na weye pika uje mpaka ushibe kwa sababu yule haja yule."

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Leo haja yule katakuja kesho. Amwambia: "Mimi sinajaa nataka kama weye unayomwambia ni kweli hayo tukimbie."

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Amwambia: "Basi kama tukimbie, haya twende zetu, ufunge mlango, lakini nenda huko chumbani anakolala somoyo utizame kama hapa juu, pana vibuy-- pana-- pana mkoba upachue huo(?) mkoba. Ndani ya mkoba muna mabuyu saba." Maana-- nanma ya vibuyu, vibuyu vibuyu saba. "Sasa kati ya vibuyu saba hivyo vipachue ulete-"

Ki ML M Vibuyu ... nini?

Ki MC2 M Halimo humu buyu ukamonyesha.

Ki ML M Subiri kidogo...

Ki MC2 M Ahaa. Hapo alikwenda akaupachua ule mkoba, sasa kupachua mkoba muna vibuyu vitungwa.

Ki ML M Vitungwa? Vitungwa ndio?

Ki MC2 M (Laugh) Maana ni kama hidhi(?) tizama, tizama, sihii.

Ki ML M Ahaa, vimetungwa.

Ki MC2 M Ehe, vimetungwa.

Ki ML M Sawa.

Ki MC2 M Maana kama hidhi(?) hakin-- chaku-- pakukamatia, ukatunga ukatia kamba patakukamatia.

Ki ML M Ehe. Sawa.

Ki MC2 M Vimetungwa ndio vimetungwa. Sasa alikwenda akauchukua ule mkoba akaja nao muna vibuyu saba. Amwambie: "Hebu toa kimoja kimoja unipe." Sasa yule mtoto alitoa kibuyu kimoja, akampa yule simba. Amwambie: "Hebu tizama humo ndani muna nini." Amwambie: "Humu muna ncha moja ya ukoka." Sijui mnaelewa?

Ki ML M Ndio.

Ki MC2 M Ukoka mnaelewa?

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Amwambia: "Humu muna ncha moja ya ukoka." Amwambia: "Basi huo si ncha moja ya ukoka huo ni ... ya ukoka. Hiyo unaona ncha moja ya ukoka jani moja, si ncha moja ya ukoka ni t...

Ki ML M Kuta kuna nini?

Ki MC2 M Cha tatu alikutakuna cha tatu kile ali--

Ki ML M Moja?

Ki MC2 M Kuna tojo la maji?

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Kwani cha nne?

Ki ML M Cha tatu.

...

Ki ML M Akatwende bahari nzima kabisa.

Ki MC2 M Ehe. Amwambia: "Hebu toa cha nne muna nini." Amwambia: "Hiki cha nne naona namna ki-- kidude namna ya kidu-- namna ya kichupa kina kishimo. Amwambia: "Basi hijo ni shimo kubwa sana hiyo kama, kama utakiangusha hapo arizini pata thi-- pata tokea shimo hadima ukomo kwenda chili."

Ki ML M Ahaa.

Ki MC2 M Amwambia: "Hebu toa cha tano mna nini." Amwambia: "Hiki cha tano, naona mnakama kisu cha ncha. Amwambia hicho si ki-- si kisu cha ncha, huo ni ukuki huo." Ushasikia, ushasikia uzuri?

Ki ML M Ndiyo.

Ki MC2 M Hapo, vibuyu vitano visha(?) vipata vina silaha, lakini vile viwili havina cho chote. Hapo amwambia: "Basi uchukue hivyo vitano, hivyo viwili viachilie mbali." Hapo alivichukua vibuyu vile amwambia: "Panda mgongoni kwangu. Hii-- huu mchororo huu wa shaba huu niliofungwa, wee gauza hatamu." Hatamu unaijua?

Ki ML M Ndio.

Ki MC2 M "Gauza hatamu univishe uzuri upate kuikamata mimi unipandie. Tukimbie, kwa sababu hivi sasa, haya tunayo ya zungumza hapa Bwana Usi huko alikokeshwa fahamu. Na huko aliko Bwana Usi kwa safari yake, keshafika na wanarudi hivi sasa kunifuatia si-- kutufuatia sie kwa sababu keshwa ya fahamu haya kama tunataka toroka. Na keshafahamu kama ... nifungua weye, panda juu ya mgongo wangu twende zetu." Binaadamu yule alipanda, Bwana Usi yule alipanda juu ya mgongo iliwakimbie. Kupanda juu ya mgongo amwambia: "Ukamate uzuri." Alikamata uzuri. Hapo alikwenda yule simba. Alitoka simba, lakini wanapokwenda hawapajui wapi.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Alitoka simba, isipokuwa wanatoka pale nyumbani kumkimbia yule zimwi tu. Lakini hawajui tunakwenda wapi.

Ki ML M Wote wawili?

Ki MC2 M Wote wawili. Simba wa pori lakini kakamatwa mchanga naye na yule mtoto naye kakamatwa mchanga. Na wote wakalelewa pale.

Ki ML M Sawa.

Ki MC2 M Hapo mtoto yule alikaa juu ya mgongo wa simba. Simba alikwenda mbio ndogo ndogo, hata halafu amwambia: "Hebu Bwana Usi tizama upande wa kusini kuna nini." Yule aliye kule mgongoni alitizama hivyo upande wa kusini. Amwambia: "Bwana Usi kusini kuna wingu kubwa sana, sasa hivi tutachezea mvua." Amwambia: "Bwana Usi amwambiahu-- hiyo si-- si wingu, hao ndio huo umati wa binaadamu, huo wanaokuja kutufuatia siye mazimwi hao. Na wale wameshajua kwamba sisi tunatoroka wanakuja mazimwi hao, si wingu." Amwambia: "Ata-- hii rafiki yangu si mazimwi lile wingu, na sasa hivi tutapata mvua." Hapo walikwenda wakenda, wakenda amwambia: "Kutizama tena." Amwambia: "Miye nilikwambia wingu lile wee ukanambia si wingu mazimwi, sasa hivi tutapata mvua. Amwambia: "Wee hujui wee, mazimwi wingu wa mazimwi huo, kiza hicho wingu wa mazimwi, sio wingu." Walikwenda zao. Hata halafu amwambia: "Hebu, tizama tena." Amwambia: "Kweli, sasa naona, kama ni watu wale." ML M Ehe.

Ki MC2 M Amwambia: "Je, ...wambia, basi wale hatuna mbio za kwenda mpaka wa situkamate. Sasa lakini kamata uzuri, mtaka kwenda mbio." Yule binaadamu amb... simba. Hapo alikamata uzuri. Simba alikwenda mbioo, halafu amwambia: "Hebu tizama." Amwambia: "Aaaala! Wale watu baraaabara hivi sasa pia sura zao zina juilikana." Amwambia: "Basi, nilikua bado sijaenda mbio. Sasa ntaka kwenda mbio." Na zile mbio anazokwenda yule mtoto pumzi zinamaliza, kwa mbio nyingi cha simba. Lakini pia akamwambia: "Bado sijenda mbio, nataka kwenda mbio." Amwambia: "Lala mgongoni, huzi wii miye pumzi zako weye ninapokwenda mbio. Lala mgongoni."

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Alilala pale akakamata yule simba alikwenda mbio. Amwambia: "Hebu ... kichwa utizama nyuma." Amwambia: "Sasa hivi Bwana Usi yuko usoni, na watu wengine wako nyuma siwajui nani, lakini wanakuja kwa mbio kweli." Amwambia: "Sasa basi, tutakamatwa sasa hivi, lakini vile vibuyu vile, tumilia." Hapo walikwenda mpaka sasa mweshafika(?) kama hapo kisimani. Amwambia: "Aa, sasa hivi hatuna, hatuna mbio za kwenda mpaka tusikamatwe." Amwambia: "Basi kile kibuyu cha ukoka, kimimine, alimimi na pale mpaka zukakuoka unao kimo cha mtu ule ukoka.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Sasa wale waka-- wakazuilika mbio kidogo, kwa ule ukoka. Maana anapo ungana hivi, huku kweupe, lakini huku ndo ukoka.

Ki ML M Ndio.

Ki MC2 M Umeshafahamu, ee?

Ki ML M Ee.

Ki MC2 M Hapo alimwambia: "Mwaga na cheche ya moto ukoka wake. Alibwaga ule lile kaa ya moto ule ukoka ulivipuka na wale wamo mule mule ndani ya ukoka. Unafahamu uzuri ninavyosema?"

Ki ML M Ndiyo.

Ki MC2 M Kwishakuwaka ukoka, lakini sasa kati ya wale mazimwi, wengine waliruka moto ule, wengine waka-- waka-- wakabakia kufa pale pale.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Sasa waliobakia waka-- wakaendelea na kumfukuza. Hapo alimwambia, alimwambia: "Tunavyo vibuyu vingapi." Amwambia: "Vita-- vitatu. Tumeshatumia viwili." Amwambia: "Sasa mwaga hicho cha mashimo". Alimwaga cha mashimo. Sasa wengine wakaruka, wengine wakatumikia mule mule mashimoni. Sasa wakabakia kidogo. Amwambia: "Tuna vingapi, tuna viwili."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M "Haya, viwili hebu kimwage hicho kinacho, kinacho, kinacho chuma, kinacho chuma kina kisu kama kisu." Akakimwaga. Sasa ulikuwa mkuki ule ukafumafuma mmoja mmoja. Sasa alibakia mmoja Bwana Usi, mmoja yule Bwana Usi. Alimwambia: "Usitumie hiyo silaha iliyobakia usitumie, mpaka uone tayari, sasa Bwana Usi kutukamata ndio um-- um-- umwagie ndani ya macho."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Na uliobakia ni mkuki mmoja tu. Hapo walikwenda mbiooo mpaka yule Bwana Usi akamfika-

Ki Y# Mkuki au bahari iliyobakia?

Ki MC2 M Bahari kati ya kufanya hadithi hii bahari nimaikaa(?) mwisho. Lakini uliyobakia mwisho mkuki. Bahari ndio hii-

Ki Y# Ambayo tushaizungumza hivi sasa-

Ki MC2 M Tushaizungumza hivi sasa. Ehe. Sasa bakia mkuki.

Ki ML M Sawa.

Ki MC2 M Hapo, alimfika. Amwambia: "Weye nilikukamata kijana, je, hivi sasa weye, nshakufuga mpaka nishakupa vitu vyangu na nilikukamata bado ukali na nguvu, hunenda mbio hunenda mbio weye."

(Anaposema anapiga makofi.) Yule zimwi yule anamwambia simba, amwambia: "Wee simba wee hunenda mbio hunenda mbio."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo alikwenda mbio mpaka simba ikawa pale wanapokwenda mbio simba na zimwi hapaoneke kwa vumbi.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Vumbi sijui tunalelewa(?) sote.

Ki ML M Mhh. Ndio.

Ki MC2 M Hapo, alimwambia: "Tumia ile silaha." Alitoa ule mkuki ku-- ku-- kukifanya hivi kile kibuyu ulitoka mkuki, ulifuma hapa mpaka ukatokeza huku. Yule zimwi akanguka chini.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Lakini kule kwangu kaa chini, simba hapa keshafika buranji. Ule muda wa kuanguka chini zimwi, simba keshafika buranji. Amwambia: "Hebu tizama nyuma kuna nini." Amwambia: "Hakuna jambo." Amwambia: "Basi turudi."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo walirudi. Walirudi wakenda mpaka pale alipoanguka yule zimwi, amwambia: "Kate kate, kate kate yote huyu nami ninje(?)." Alimkata, alimkata kwa kisu akakatakata. Sasa yule simba akantafuna, halafu amwambia: "Basi, sasa kunipanda miye basi kwa sababu hakuna tena ya kutuzuru weshamaliza wale. Sasa tufatane hivi hivi, lakini kati ya kufatana kwetu, mimi unisaidie kutafuta nyumba yangu, kwa sababu mimi simba, wee binaadamu. Sasa huku porini tusi-- tusimalize kulitoka pori ulisaidie kuitafuta nyumba yangu. Nikishaipata nyumba yangu, wee utakwenda zako huko ukatafute kuna kwa binaadamu wenzio, na mie utaniacha huku porini." Akamwuliza: "Haya nyumba yako ni kama ipi?" Amwambia: "Nyumba yangu ni mvungu wa jiwe." Tunaelewana?

Ki ML M Ndiyo.

Ki MC2 M "Nyumba yangu miye ni mvungu wa jiwe, tutapokutia jiwe nishafanya mvungu hivi. Sasa hiyo miye itakuwa myumba yangu kwa kwetu tunaita koma."

Ki ML M Nkoma?

Ki MC2 M Ehe. Ule mvungu wa jiwe tunaita koma. Na kwenu mnamumilia hivyo. (Kicheko)

Ki ML M Hapana. Hiyo ni pa-- kama panga vile.

Ki MC2 M Ata, kwetu panga mbali na koma mbali natundu mbali na turuzi mbali na tomo mbali.

Ki ML M Do. Haya.

Ki MC2 M Hapo, walitafuta maana koma lile jiwe likaa hivi. Sasa huku mvunguni ndio koma lile kwa kwetu. Umeshafahamu ee?

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hii tunatumia sehemu mbili. Sehemu moja koma, jina jingine, jina-- jina moja koma hii hili hili, jina jingine mvungu wa jiwe .

Ki ML M Sawa.

Ki MC2 M Hapo alipitia pale getoni. Pia geto ndo lile lile. Kwisha kujitia pale amwambia: "Ba-- basi hapa rafiki yangu hapa, mimi ndipo nyumbani pangu, na weye na amini huko unakokwenda, wee binaadamu kutenda wakuta binaadamu wenzio. Lakini hao binaadamu utaokwenda wakuta. Kwanza ujue weye mzuri kama hao utaokwenda wakuta, kwa sababu weye ulilelewa upate u-- unone upate uliwe ulifugwa uzuri sana. Na mnene sana na mtakatifu sana. Sasa na amimi utaokwenda wakuta wazuri zaidi-- mzuri weye zaidi kuliko wao. Lakini mnavyo kwambia weye nenda. Itapokukuta shida uje hapa. Mimi ntapiga mbuzi hapa. Ntakula nusu, ntakula nusu na robo, robo ntaa cha hapa. Sasa wee huko kama hujapata kitu uje hapa uje na kibiriti uchome. Upate chakula, ntapiga kuku hapa, ntakula sitamaliza, ntakuwekea. Mradi kama itakukuta shida ufike hapa, mimi ndo mwenzio, hewala." Alitoka sasa yule binaadamu kwenda zake, binaadamu mwenyewe yule Bwana Usi, ee?

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Alikwenda hata kufika kama hapa na kisimani, simba yule alimwita: "Aloo, aloo, njoo njoo njoo." Alirudi yule Bwana Usi akenda kwa simba. Kufika amwambia: "Amma rafiki yangu weye mzuri sana, weye mzuri sana, kwa sababu ulipoondoka hapa ukanipa mgongo na kutizama. Naona choyo kwa uzuri ulio nao."

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M "Sasa kama miye naona choyo, hao utaokwenda fikia huko watasidi kuona choyo, haswa wanaume wenzio. Kwa sababu unawazidi kwa sura, kwa hiyo njoo nikurambe. Upate ukomae kidogo mtu huende ... kwa watu mzuri, huenda mbaya mbaya."

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Hapo alikwenda, kufika amwambia: "Vua shati." Akavua shati, akamramba kamramba kamramba, alikomaa yule.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Alikomaa akawa na mapwepwe, mapwepwe tere tere tere mote, mwili mzima. Amwambia: "Nenda." Ha-- akamwambia: "Mbona rafiki yangu, mie tenda karibishwa nani, kwisha nifanya koma namna hiyo." Amwambia: "Ndioo, mtu huenda mjini kwa watu mzuri, huenda mjini kwa watu mchafunhafu, kwa sababu utapokwenda mjini kwa watu na sifa yoyote. Watapokuonea choyo watakufanyia uhi-- ufa-- ufisadi, watakuwa na uhasidi mwingi juu yako kama utafika na kuwazidi wee kwa uzuri, nenda." Hapo alikwenda. Bahati nzuri kufika hatua kama hapa na hapo sokoni petu hapo, alisikia majogoo. Akaona tayari juu-- majumbani iyoo(?), alifatia. Bahati nzuri hajafika kule anakosikia majogoo alikutia shamba, shamba ilipandwa mitango kama hapa mpaka majumbani kwa yule bwana. Mitango mitupu. Na shamba ile kumbe ya vibaraka wa mfalme, yale matango yale matango ya vibaraka wa mfalme.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Na wenyewe wapo pale wanayainga, kwa sababu huibiwa.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo hajui yeye badili ya kuikuta ile shamba hajui nipite upande upi. Alipita mule ndani ya matango. Kupita ndani ya matango, vibaraka wale walimwendea(?) kamkamata mwizi, jamani huyu mwizi, mwizi mwizi mwizi, wakamkamata. Haya tumfanyeni tunchinje. Wale wenye shamba wale vibaraka wale, waliambia: "Na huyu tunchinje, kwa sababu mwizi huyu." Asema: "Jamani mimi sinchinje mimi si mwizi isipokuwa mimi mgeni." Asema: "Haiwezekani, matango yetu siku zote yanachumwa humu. Kila siku tunapokuja hapa matano-- sita yeshachumwa, leo tunakokuta wee amba wee mgeni. Mgeni unaetoka wapi,

wee? Wee mwizi." Hapo alitokea mmoja asema: "Jamani huyu tusimchinje. Isipokuwa, kama hukumu akatoe mfalme, tumpelekeni kwa mfalme."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo alipelekwa. Bwana Usi wee.

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Hapo alipelekwa, kupelekwa kwa mfalme yule, ambiwa baba wee una-- yule mfalme akamwona mbovu mbovu mbovu mbovu, hafai. Na ile sura ya kiarabu hana. Kwa ile kukomazwa ni yule simba, sura ya kiarabu hana. Hapo asema: "Ninyi huyu msimchinje huyu ni mtu ana njaa tu, kama kaja kuiba kama vipi, lakini huyu msinchinje, mchukueni awe kibaraka mwenzenu. Nendeni mukainge nyote haya matango. Na mukipiga matango na endajeni(?), maskini huyu hana haja ya kunchinja, mchukueni."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo walivunjikiwani zile hukumu zao mkabidi wanachukue. Wawe nae kule sasa napopika matango hung'a ile. Hapo hatajua kutua wale wanakwenda zao, maana hulala pale pale shamba ee.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Wanakwenda zao vibandani, yeye alitoka. Alimwambia: "Jama(?) mimi naenda haja kidogo." Alikwenda zake mpaka kwa yule simba.

Ki ML M Ndiyo.

Ki MC2 M Kufika kwa simba amwambia: "Rafiki yangu mimi nina shida kubwa sana, shida niliyonayo leo bado kidogo ningeliuliwa; ule ugeni wangu? Nilikwenda tokea shamba, shamba sijui nipite wapi, nikapita katika shamba. Kupita katika shamba vibaraka wa mfalme walinikamata. Waliponikamata waliambiana waliuwe, kwa nichinje. Sasa akatoka mmoja akahuzunika, akamwambia: 'Tumpelekeni kwa mfalme.' Yule mfalme hukumu aliyotoa juu yangu miye, kwamba mimi maskini na mimi niwe kibaraka. Sasa nimechukuliwa na mimi hapo naenga matango ... chakula changu matango."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Amwambia: "Haya, njoo." Alikwenda. Kufika amwambia: "Vua shati." Alivua shati, akamramba, akakomaa zaidi kuliko vile. Amwambia: "Rafiki yangu mbona kusha nikomaza zaidi vipi." Amwambia: "Wee nenda tu kwa sababu wee unaona bado ukali nzuri. Hao vibaraka wenzio watakuonea, ilivyo kwa ukali nzuri watakuchua. Nenda hivyo hivyo mbaya zaidi watakuonea huruma." Hapo alikwenda. Lakini sasa ile kwenda mwenyewe, kidole hiki anacho hiki hana, hiki anacho hiki hana.

Ki ML M Mhh. (Kicheko)

Ki MC2 M Kesha katwa katwa.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo alikwenda. Kufika alikwenda kuta vibaraka wanazungumziani jamani, leo sultani ka-- kapiga upatu huko kiamboni, kapiga upatu kawaalikia watu wenye kiambo kwamba anao-- ana watoto wake saba. Na watoto hao hawajapata waume na aliweka naziri yeye alikuwa hapati watoto wakaweka naziri. Pindi apatapo watoto. Kama wake! Asiwaose waume mpaka amalize kuzaa, kama waume asiwaose wake mpaka amaliza kuzaa.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Na kapata watoto wanawake watupu watoto saba, kwa hiyo watoto wanawake wale, wameshafikilia makamo naye keshajeamini kwamba hazai tena na mke wee keshakonga. Watoto hao sharia yake mfalme anataka wachague waume watakao wao wenyewe ndio amuoze. Sasa alivyofanya mfalme kapigisha-- kapigisha upatu kapigisha mbiu, kawaita watu wa misiri mzima, hapo wajikushanye. Wakisha jikushanya mabaniani Wahindi, Wazungu, Waarabu, Waswahili, Wanyamwezi kula kabila, mpaka watumwa pia, wajikushanye. Sasa huyo atakaechaguliwa ni mwanawe ndio mume wa mwanawe, vibaraka alikwenda wakuta wanazungumziana hivyo. Alikwenda mwambia simba, yeye yule alikwenda mwambia simba: "Bwana wee, rafiki yangu, mimi nataka mke." Amwambia: "Unataka mke halio ulio." Amwambia: "Ehe, minataka mke, kwa sababu miye ninakwenda kule, kunako wale vibaraka wenzangu.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M "Nimenda wakuta wanazungumziana kwamba mfalme kaweka naziri. Apatapo watoto kama waume awaoze wake siku moja kama wake awaoze waume siku moja. Maana alikuwa hazai. Basi kwa hivyo na miye nataka mke vipi." Amwambia: "Njoo nikurambe." Alikwenda, alikwenda, akampiga ulimi mgongoni, halafu alinyonyoka kichwa kizima ikawa hata nywele hana.

Ki ML M Ahaa.

Ki MC2 M Na jicho moja pofu chongo.

Ki ML M Ndo, ndo.

Ki MC2 M Amwambia: "Haa, rafiki yangu miye ntaka kwenda posha mke, tena mtoto wa kiarabu nawe kwisha niramba nywele sina, mpaka jicho moja pia chongo. Vipi ndio ntapata mke miye. Amwambia: 'Nenda tu wee.' Amwambia: 'Nenda tu wee.' Mimi sitaki uwe mzuri kwa sababu ukawa mzuri watu watakuonea."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M "Lakini nenda hivyo hivyo mbaya." Lakini hawezi kuenenda. Maana hivi vidole vyote vibuku, vidonda--

Ki ML M Vibuku?

Ki MC2 M Vibuku unajua?

Ki ML M A'a, ... ulize.

Ki MC2 M Ee.

Ki ML M Vibuku ndio nini?

Ki MC2 M Maana vimekatika kwa madonda hivi vidole.

Ki ML M Mhhh.

Ki MC2 M Sasa kile kinacho bakia kwa kwetu ndio kibuku.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Tuseme hichi kidole kizima, laki kimesha katika hapa. Hichi kipande kilicho bakia kwa kwetu tunaita kibuku.

Ki ML M Sawa na butu.

Ki MC2 M Ehe.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Sasa wali-- alikwenda zake. Lakini wale vibaraka wenziwe wanazindi kumchukia kwa sababu sasa hivi harufu tupu hapa kaliki ... (Noice)

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Kanaruka(?) ajabu na kujikuna hivi ule unga wa mwili unaeruka. Maana pere nyingi. Sasa anapojikuna hivi, hueruka ule unga. Sasa hawa ... kukaa nae. Ilifika ile siku. Mfalme yule akawalika watu: "Jamani leo mimi niliweka naziri kwamba pindi nipatapo wanangu, nisiwaose waume na kama wake nisiwaose kama waume nisiwaose wake na kama wake nisiwaose waume mpaka nimalize kuzaa. Na hivi sasa ninaamini nimemaliza kuzaa wala sizai tena kwa mke wangu alivyo."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Sasa imefika siku ya kuwa wanangu wachague waume watakao. Na waalikia: "Jamani wenzangu wa misiri nzima kama-- kama kabila yoyote, kama mtu vyovyote alivyo. Aje hapa, atakae chaguliwa ni mwanangu ndio mume wa mwanangu." Watu walikushanyika. Sasa walipokushanyika alikwenda wapanga sasa. Na alivyowapanga yule Mwarabu aliwapanga hawa wa usoni msitari wa kwanza hawa. Maana aliwapanga rauni ee, hawa msitari wa kwanza aliwapanga Warabu wenziwe, msitari wa pili akapanga Wahindi, msitari wa tatu akapanga Wazungu, msitari wa nne akapanga Waswahili waliokuwa, sio watumwa, msitari wa tano huku mwisho akapanga wale vibaraka wale.

Ki ML M Mhhh.

Ki MC2 M Vibaraka vyote! Hapo wale wanawe aliweka hapa katikati ya msururu wa watu wale wote, akaweka hapa katikati. Hapo aliwapa ndimu, kula moja ndimu, kula moja ndimu, wale wanawe watoto saba. Hapo alimwambia: "Ndimu hizi mama na baba mimi, leo ndio siku yenu ya kuolewa. Kula mmoja mwanangu achague mume atakae ampige ndimu ni muoze, marufuku kwenda ukamguza hivi, lakini si marufuku kwendapapo ukampiga ndimu yako."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Ueshafahamu sijui ninavyosema.

Ki ML M Ndio nimeshakuelewa.

Ki MC2 M "Kwenda ukangusa kwa mikono yako."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M "Si ruhusa, lakini kwendapapo ukampiga ndimu yako, ndo tutamjua huyo ndiye mumeo." Hapo walipewa ndimu walewa-- zile watoto saba. Na kati ya watoto saba wale, wale watu waliokushanyika woote weshachagua yule kichinja nimba.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Kichinja mimba sijui tunamfahamu?

Ki ML M Yule wa mwisho.

Ki MC2 M Mtoto wa mwisho.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo kula mmoja kanaomba mungu apigwe ndimu ni yule kichinja mimba.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Na yeye mwenyewe yule mfalme nia yake, maana ya wale Warabu wenziwe kuwa ... wasoni-- usoni kwamba wachaguliwa wale Warabu wenziwe. Si nia yake wachaguliwa Wahindi wala Wazungu wala Waswahili. Nia yake wachaguliwa hawa Warabu wenziwe aweka usoni." Sasa mtoto wa kwanza alimpiga ndimu Mwarabu mwenziwe tena mfalme. Mtoto wa pili akampiga ndimu Mwarabu mwenziwe tena anaehusudi wa kifalme. Mtoto wa tatu wakendalea hivyo hivyo wote wakapiga warabu wenziwao wale matajiri, wale wanaohusudi wa kifalme wale-- mradi wa kachagua wanavyo vitaka. Lakini akapewa ndimu mtoto wa mwisho yule, ile ndimu yake, na yeye kwa nia yake keshachagua kwamba ampige Mwarabu mwenziwe. Lakini kwa vile, kwenda pale panapo yule Mwarabu mwenziwe kuifanya hivi ndimu, yule simba yule, yule simba yule, alinjamiwa ni jini, kinjamiwa unajua, sijui?

Ki ML M A'a.

Ki MC2 M Maana alichunukwa ni jini, je, kuchunukwa unajua?

Ki ML M Kupendwa.

Ki MC2 M Kupendwa. Sasa alipopendwa ni jini, yale maneno yale hasemi yule simba. Husema yule jini.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Sasa yule jini alikuja akaifetua ile ndimu akaitamba cha chini kwa chini mpaka ikenda ikampiga kidole yule kibaraka. Ile ndimu ya kichinja mimba ile.

Ki ML M Mhh. Mhh.

Ki MC2 M Ilitambaa chini ile mpaka ikenda ikampiga, kumpiga alirusha ngua. Asema: "Jamani ndimu yenu hii huku imenitonisha."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Kutizamwa-

Ki Y# Kibaraka mwenyewe ... Bwana Usi yule?

Ki MC2 M Bwana Usi yule. Kutizamwa ile ndimu ndio na ndimu ile ya yule kichinja mimba na ndo mzuri anaewaniwa pale.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Halafu yule babaye alisema: "Huyu hakukusudia ndimu yake imemtoka mpeni mwenyewe."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Kwa kumtizama hali alivyo kibaraka anao-- (Kicheko) kumpa mwana yule. Asema: "Huyu hakukusudia lakini isipokuwa ndimu imemtoka, mpeni mwenyewe." Alipewa mwenyewe. Kunua nkono hivi ndimu ile ikabyatuliwa kwa nyuma ikagwa tena, ikabingiria ikenda mtonesa(?) yule yule. Asema: "Jamani ndimu yenu imekuja tena hii." Asema: "Wee huoni." Sasa yule-- yule babangwa keshanuna, sasa yule Mwarabu. "Wee huoni, wenzako wanapiga wananpata wee ndimu ukinua hivi inakutoka tu, vipi weye? Hebu mpeni mara ya mwisho."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Akapewa tena mara ya mwisho kwa sababu yule baba hariziki kuwa apate kibaraka yule. Hapo alipewa mara ya mwisho. Amwambia: "Ikamate uzuri uende ukampige yule unayemtaka."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo aliikamata uzuri yule mtoto, lakini kwenda kunua nkono hivi, hujitahamaki anapotaka fanya hivi hukuishatoka. "Sasa na inapotoka huanguka chini bila kumgusa mtu yeyote. Huenda ikampiga yule kibaraka."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo bwana mkubwa yule alihamaki. Amwambia: "Nyinyi vibaraka nyote mchukueni huyu mkamfanyie harusi yake chakula matango. Na hawa wanangu wote ntawafanyia harusi mwenyewe. Wote wale akawaoza pale. Na yule akamuozaye lakini harusi ikafanyi kule ... vibaraka." Akawafanyia harusi kwa uzuri watoto sita wale. Yule akenda akafanywani vibaraka wenziwe. Wala hana kufanyiwa harusi basi tu akam... chukua "madam" kushaoza basi. Lakini mtoto yule alishikwa ni kilio ajabu kubwa sana, kwa sababu kapata mume asiyemtaka . Na wale furaha kubwa sana kwa sababu washapata Warabu wenziwao, waume wao. Kwa kuwachagua. Sasa huyu anafuraha hu-- hawa wanafuraha, huyu anamsuiba kumpata mume mbovu tena kibaraka masikini kabisa kabisa.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Hapo hao wanaume wao wakakaa nao na huyu ije akabakia kulia na kuzofu sana, hazungumzi wala hali wala-- yule kibaraka anapokwenda mule. Kwanza yule kibaraka anapoingia mle ndani ya kivuru kule shamba. Kivuru unakijua?

Ki ML M Hapana.

Ki MC2 M Hapana eh?

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Kivuru ni nyumba, lakini hio nyumba, nyumba ndooogo sana, nyumba ya kuvimba kwa makuti.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Ushafahamu eh ?

Ki ML M Mhh.

Ki XX M ... ? (Question can't be heard.)

Ki MC2 M Kwa kwetu ndo tunaita kivuru.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Sasa ilifika siku moja, yule bwana yule mwenye wale watoto wanawake. Alipata kuumwa ni macho.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Alipomwa ni macho alikanayo macho yale kwa muda wa wiki moja yanazidi yale macho, sasa kuona haoni. Na macho hayafunguki yameshavimba uso nzima. Alilala sasa. Hata kula-- uzingizini. Aliota. Mfalme macho yako haya. Huwezi kupata nafasi, isipokuwa upate dawa ya paka mweusi. Na dawa hiyo isilete mtu yoyote isipokuwa ije na wakuwezo watu saba.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Mojawapo ndo itakupoza.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Lakini kwa dawa mtu yoyote asikuletee hupati nafasi. Isipokuwa upate maziwa ya paka mweusi na maziwa hayo yaje na wakuwezo watu saba. Tunafahamiana?

Ki ML M Ndio.

Ki MC2 M Tunalokuwa hatulifahamu tuulizane.

Ki ML M Ndio ndio ndio.

Ki MC2 M Hapo asubuhi mapema aliwaagiza: "Jamani hebu wapitieni hawa wakwe zangu. Mwambie waje hapa naumwa mimi nije niambie maafa yangu yaliyonipata." Hapo waliambiwa wale wakenda pale. Kufika amwambia: "Jamani macho yangu mimi yananiuma sana wakwe zangu. Mupo nyote?" Asema: "Tupo." "Je na kibaraka yupo?"

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Maana-- nyinyi mupo na kibaraka yupo. Na Asema: "Tupo, nipo bwana nipo." Ambwiwa: "Basi mimi nimeota usingizini kwangu leo nilipolala kwamba macho yangu haya. Siwezi nikapata nafasi isipokuwa nipate maziwa ya paka mweusi, na maziwa ya paka mweusi asilete mtu yoyote isipokuwa mlete nyie wakwe zangu. Watu saba mojawapo yoyote basi huenda nikapata nafasi. Basi baba nawatuma mkanitafutie maziwa ya paka mweusi kama yalipo." Hapo walianza kumwambia yule kibaraka, wale waozi wenziwe. Waozi wenziwe mnajua?

Ki Y# Ndio.

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Walimwambia: "Weye paka kwa mji huu hapana mwenye paka, isipokuwa paka wana Warabu watupu. Weye kwenda mwambia vipi Mwarabu mpaka aweze kukukamia maziwa yake ya kupe wee, huyapati maziwa wee. Kushapata mke ya bure basi."

Ki ML M (Kicheko)

Ki MC2 M Hapo alimwambia: "Jamani na nyinyi mkiyapata na mimi ntayapata kama hamkuyapata na mimi sijapati." Hapo walitoka. Kutoka nje, walimwambia: "Siye hatutaki kufatana na weye pita yako njia nasije tuache tupite yetu njia." Yule kibaraka aliona uzuri sana. Walibaguka sasa njia zile, kibaraka alisimama akawapisha wote wakenda zao usoni kibaraka alipiga mbio akenda kwa simba yake. Kupiga mbio hawezi alikwenda tu. Kufika amwambia rafiki yangu: "Mke nishapata. Lakini mke wangu taukia juzi kuja hali kulala halali kukoga hakogi wala hafanyi chochote kilio moja kwa moja kwa sababu mimi ni mbaya yeye ni mzuri."

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M "Na mimi mbovu yeye mzima. Na yeye Mwarabu mimi hali yangu ndo kama hii. Basi kwa hivyo mke wangu anaponitizama hanafuraha na mie. Je, rafiki yangu na hivi sasa mkwe wetu kapata ugonjwa wa macho. Tushaambiwa tupeleke maziwa ya paka mweusi. Nitampata wapi hali yangu hii niliyo na paka wana Warabu tu?" Amwambia: "Njoo, njoo nikurambe." Alimramba. Akamramba, akamramba alitoka Mwarabu zaidi kuliko ile siku ya kwanza.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Mzuri kabisa kabisa. Amwambia: "Weye nimeshakufanya hivyo, lakini chukua pete hii, nenda zako mpaka hapo njiani ukafika iangushe. Utoe amri yako useme ujengwe nyumba inayositwa ghorofa

moja." Alichukua pete ile, Mwarabu sasa, alichukua pete ile. Sasa yule simba ikawa hapo pale keshajigauza paka, walifatana na paka na paka mwenye mweusi anavyo vitoto vyake.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Walikwenda mpaka chini ya njia. Akaamrisha pete ile paka jengeka nyumba ya ghorofa moja. Sasa ile nyumba ya ghorofa moja, hapa chini pana ile nyumba inabaraza na hapa chini pana kiti.

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Sasa yule akakaa pale juu ya kiti na yule paka yake hupita humu miguuni paka mweusi. Wale walitafuta maziwa pale misiri nzima wasiyapate. Sasa jamani maziwa hatuyapati hatuyapati turudini twende tukajibishe maziwa hatukuyapata. Walibahatika na kupita pale. "Salaimaleiku aleikum salaamu bwana, habari za siku salama, eh bwana?" "Tuna shida." Akawauliza: "Mna shida gani Warabu?" Ndiye yule kibaraka.

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M "Mna shida gani?" Asema: "Sisi shida yetu tunatafuta maziwa ya paka mweusi. Na leo tumemwona hapa wee unaye bwana utuuzie. Amwambia: "Warabu mtoka huko makwenu mkuja hapa kunitukana kusudi kwanini ninasikia mimi maskini niuze maziwa ya paka ndo npate kula. Au vipi? Mkusudia nini? Hebu niambieni."

Ki ML M Ehe.

Ki MC2 M Asema: "Sisi hatukuoni masikini, lakini haja yetu tupate haya maziwa ya paka mweusi. Utukamia kwa hali yoyote." Asema: "Mimi siwezi nikawauzia kwa sababu paka wangu hana cha kunyonya. Nimue paka wangu kwa maziwa ya kuuza. Mimi si masikini wa hivyo. Mkitaka maziwa nitawauzia lak-- nitawakamia lakini kwa shuruti yangu si kwa pesa zenu." Asema: "Una shuruti gani bwana?" Asema: "Mimi shuruti yangu niwauzie maziwa ya paka wangu, lakini niandike isimu yangu kichwani mwenu, utakubali?" Asema: "Tumekubali." "Haya basi kama mmekubali aje mmoja mmoja hapa ninyoe(?) nipate ngozi ya kuandika isimu yangu kichwani mwake."

Ki ML M Mhh.

Ki MC2 M Sasa alikwenda mmoja akavuliwa kofia. Akaniolewa kama hapa. Mpaka paka peupe. Halafu bwana yule alichukua kalamu. Aliandika; mimi Bwana Usi mvaa nguo za sufi siku ya kufa harusi nimemnunua kwa maziwa ya paka mweusi mtuma wangu mwamduki.... (End of cassette one.)

Tunafahamiana yule bwana Mwarabu yule aliandika kichwani mwa yule muozi muoziwe mmoja lakini hajijui. Aliandika mimi Bwana Usi mvaa nguo zaa sufi siku ya kufa harusi nimemnunua huyu kwa maziwa ya paka mweusi mtumwa wangu mwamuki. Kwa maneno haya niliyoyasema tumefahamiana? Alikwenda na mwengine akamwandika kama vile. Akenda na mwingine mpaka watu sita wale akwamaliza kwa isimu ile ile. Hapo aliwaka (This part is only on paper.)

Proofread by MP

Edited by TR in October, 1996

DAHE 101

Place: Pemba, Shumba

Time: --

Interviewee(s): 1. (BH1) 2. (WS) 3. (AJ1) 4. Unknown (XX) 5. (SS2)

Interviewer: Mlacha (ML)

Recorder: Sony Professional

Language: Standard Swahili (Ki), Pemba??

Topic: 1. Story about a lion, a rabbit, a guinea-fowl and a jackal and another about a lion. 2. A short history of Shumba. 3. A story about a lion, a rabbit and a hyena. 4. A story about a rich man and a dog. 5. A short history about Micheweni.

Ki ML M Labda tena ujaribu kurudi huku tuambiani jina lako nani na una umri gani?

Pe BH1 M Jina langu nikiwa ni Bakar Hamisi Hamadi Kombo, Shumba ya mjini.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Na umri wangu, nina miaka thelathini na moja mpaka sasa hivi.

Ki ML M Mhh. Inaelekea una hadithi nyingine nzuri unataka kupatia?

Pe BH1 M Ehe ninayo nyingine nzuri ambayo pia nilizungumziwa hivyo hivyo ni marafiki zangu, wakati niliposafiri kuelekea njia ambayo ya sehemu nyingine za mbali mbali kidogo.

Ki ML M Mhh. Tafadhali mtusimulie.

Pe BH1 M Haya. Nilisafiri nikaenda zangu nchi jirani kama sehemu za Nairobi huko Kenya, nikampata rafiki yangu mmoja akanitolea hadithi hii inayofuata. Alinambia kwamba yeye alizungumziwa ni babu yake vile vile lakini na mimi pia nikaipenda hiyo hadithi nikahifadhi mpaka leo hii, kwa pale ambapo alinisimulia ndio hivi nami nakusudia kuitoa. Aliniambia hivi, kwamba kulikuwa na wanyama wote katika ulimwengu.

Ki ML M Tuendeleo, tuendeleo.

Pe BH1 M Kwa hivyo mnyama wale wakakaaaaa, mkubwa wao alikuwa ni simba.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Simba yule alikaa bado ni kijana ana nguvu za kuweza kuchumia, hakuwa na wasi wasi kwa kuwa na nguvu. Kumbe zile nguvu zinapomalizika, huwa ni hasara kama hukujiekee hakiba huku nyuma. Sasa simba alikaa mpaka alipofikiria umri wa kwamba hawezi tena kuchuma.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Aliwakusanya wanyama watatu. Alimwita-- alimwita mbweha, akamwita na khanga, akamwita-- akamwita na sungura.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Wanyama watatu hawa alipowaita alikuja kuambia. "Jamani ee, wale wanamopoalitwa ni simba." Walianza kuambiana.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M "Jamani twenda kwanze simba. Simba ni ntu mbaya na hasa huyu keshakuwa mzee na sisi ni wanyama ambao twajulikana ulimwengu mzima kama siye nisi wanayama wakwe. Kwa hiyo tusije tukashindwa akili chukuyu(?), huyu hana ugonjwa wa pesa moja. Bali ni ku hana nguvu za kuchumia." Lakini umwambiavyo mtu asije nkaribia, khanga yeye alisema: "Mimi katika mkutano wake wote atakokwenda kuhutubia mimi ntaaka kwenye boriti."

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Mbweka yeye alisema: "Na mimi ntachimba."

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Apa kizingitini.

Ki ML M Ndio.

Pe BH1 M Na sungura vile vile akasema: "Na mimi ntachimba." Sasa tutansikiliza maneno yake akayotuambia.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Sawa, sawa sawa-- atakayekuja legea hiariye, haya walikwenda wale wanyama watatu. Walipofika kuambia: "Wenzangu nimewaita hapa kwa kuwa nyinyi ni wakubwa wa wanyama, ingawaji mimi ni mkubwa lakini nyinyi bora. Sawa. Sasa aliwaambia: "Jamani naliwaitia hapa. Mimi nimekuwa mzee."

Ki ML M Ndiyo.

Pe BH1 M Kwa hivyo kati ya wazee wangu wote si kwamba pia nshazidiwa ni mzee. Bali nshazidiwa ni maradhi na ngonjwa na nimekwenda kwa mganga nataka-- nambiwa sipowi mpaka nilemwe wanyama wote.

Ki ML M Alemwe?

Pe BH1 M Ehe, alemwe.

Ki ML M Kulemwa ndio nini?

Pe BH1 M Kulemwa ni kupigiwa mianzi kwa kukwetu ngangadaa ngangadaa ngangadaa.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Kuaguliwa.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Sasa wale wanyama wakimwambia: "Ha mzee utalemwa vipi?" Akiwaambia: "Mgangaamenambia nitafute bafuta warasaba na nishatafuta hii hapa. Lakini mpaka wanyama wote wakutane, kwa kuja pigia huo goma." Mhh. Wale wanyama walisema kwamba huyu si ngonjwa huyu, pataliwa wanyama hapa nkepite baa, mhh. (Kicheko) Sasa wale walirudi waliambia: "Asante mzee, maneno tulishasikia na tuwaita wenzetu tuwaambie."

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Walikuja wakapiga upatu.

Ki ML M Upatu?

Pe BH1 M Mhh.

Ki ML M Upatu ndio nini?

Pe BH1 M Kama mbiu.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Wanyama wote twawataka wahudhurie kwa muda wa saa tisa.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Mahali fulani uwanjani pao. Sasa wale wanyama walipokuja, waliambiwa ni yule khanga na sungura na mbweha: "Jamani si tumeitwa ni simba, ametuambia kwamba simba agonjwa. Na hawezi kupona ameambiwa ni mganga mpaka alemwe. Na kulemwa tumleme siye, lakini tuambiavyo simba hagonjwi, bali atakatafuta unyaji anye."

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M "Kwa hivyo twenda." "Mwasemaje twenda?" "Aa, twendeni, twenda lakini, kila mtu akili kichwani mwake. Atakapokuja nkalia karibu simba wahimu mtaliwa mpaka mmaliza." Khanga alisema: "Miye sipatikani." Na mbweha akisema: "Mimi hali kadhalika." Na sungura akisema: "Na miye nachomoka." Sasa siku gani yule bwana akimwambia kwamba kulemwa kwangu kwote njooni mnilemwe mwezi wa mfunguo pili mwezi mosi. Haya. Watu walimaliza mkutano wao baada ya kushalibiana vile, ikifika ile siku walikwenda kumwambia bwana: "Tayari wale wanyama tushawajibu wenzetu na sasa hivi jitayarishe siku fulani tutakuja."

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Walikwenda. Walipofika khanga alichukua chapuo. Alikaa juu kulee!

Ki ML M Chapuo ndio?

Pe BH1 M Chapuo ngoma hiyo, kama dutu.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Na mbweha akichukua yakwe wakati kashanza kuchimba kwamba hapa ikija ikatokea mkasa vup! Hafiki simba hawezi kuchimba. Na sungura naye keshachimba kiyakwe, wanka pembeni. Mmoja pembe hii, mmoja pembe hii, khanga yupo hapa.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Sasa wambia wale wanyama katika vile kupiga ngoma zao. Yule khanga asema kwamba si ngonjwa si ngonjwa simba. Yule mbweha aditiza kwamba pataruka kivumbi.

Ki ML M Aditiza ee?

Pe BH1 M Aditiza ile ngoma.

Ki ML M Anaitikia.

Pe BH1 M Ehe, katika ile ngoma ya vile akipiga. Mbweha eh-- khanga awaambia wale wanyama: "Jama si ngonjwa simba, mkaleni mbali."

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Mbweha awaambia: "Pataruka kivumbi." Yule-- yule sungura awaambia: "Chapanyikani, musin-- musinsogeeleni chapanyikani", ilianzwa ngoma hapo.

XX M Ndio nini chapanyikani?

Pe BH1 M Chapanyikani yaani kutawanyika, maana ... akija wao wakimbie.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Kila akikaribia wakimbie. Sasa-

Ki ML M Lakini ni ngoma hiyo?

Pe BH1 M Ehe ni ngoma.

XX M Yaani katika ule ulio wake.

Pe BH1 M Sasa katika ule ndio wa ngoma, nawashanza kuwaambia huku kwamba sie katika ngoma zetu zote. Twataka wapigie hivyo ili kwamba msijenkaribia simba atavibisha visha.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Khanga alikalia pale: "Chapanyikani, chapanyikani, yule alisema si ngonjwa, si ngonjwa huyo-"

XX M Maana zile ngoma.

Pe BH1 M Zile ngoma.

Ki ML M Ahaa.

Pe BH1 M Sasa yule akisema kwamba pataruka kivumbi, pataruka kivumbi hapa, pataruka kivumbi. (Kicheko) Basi bwana simba baada ya pigiwa hivyo lilikaa, lilikaa pale chini kwanza werevue ngonjwa ata kiasi kidogo ile ilianza kutukutika: "Ngoma inanogea", ilianza kutukutika: "Ngwaa, ngwaa si ngonjwa, si ngonjwa, pataruka kivumbi, chapanyikani, chapanyikani!" Ngoma zinafika mpaka waliponogewa. Ama simba hapo alianza kunuka tena na mayowe: "Kyaaa, kyaaa, kyaaa! Kashaingia shetani, kyaa kyaa kashaingia huko, wooo wooo wooo! Jamaa wale ... ambia: 'Jamaa pataruka kivumbi', woo woo woo." Simba kashachagawa sasa.

Ki ML M Ehe.

Pe BH1 M Kashapandwa ni shetani. Hapo miguru ... tena minyama isiopinda: " ... aa mwanangu sikilizia." (Kicheko) Simba alianza kumwomba Mungu, alianza kumwomba Mungu, gafla, kanawapiga amba huku hawapungui kiasi ya mia moja. Ama kuona vile khanga yee juu juu, mbweha alijivuta kishimonive na sungura alijivuta kishimonive yanayobakia manyama haya...ujinga wenu. Tangu juzi tulipokuja ... tuliwaambia vipi msikaribieni huyu, si ngonjwa akafuta rai tu hanganyie, mizoga ile pale sasa ikawa kusanywa kitia mwagwe(?) tu. Hakusanya akitia mwagwe akisikusanya, haya tena yakwenda mwituni. Sasa hiyo ikiwapo ilifika mwisho. Lakini ipo nyingine.

Ki ML M Nipe. Hapo kuna nafasi yako bado ipo.

Pe BH1 M Ipo nafasi?

Ki ML M Haswa.

Pe BH1 M Haya. Hadithi nyingine ni hiyo ya simba. Simba aliambiwa ni wanyama wote kwamba simba watuonea siye wanyama lakini katika hivyo matembezi yako. "Unapotembea ogopa mwanadamu."

Ki ML M Sawa.

Pe BH1 M Sasa simba akashangaa, "Mwanadamu nini, mwanadamu kwanza ni kitu gani?" "Isiwe ndovu, isiwe nyati, mie na buya kilenga tu. Je mwanadamu-"

Ki ML M Na buya kilenga?

Pe BH1 M Na buya nikilenga nikifanya ninavyotaka.

Ki ML M Kubuya ndio?

Pe BH1 M Kubuya ni kushika.

Ki ML M Nashika tungetaka-

Pe BH1 M Akishika kihasiri tu aki-- akitumia takavyo.

Ki ML M Ahaa.

XX M Kama kukamata.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Akiambia: "Simba sikiliza huyu mwanadamu hapana habari ni kidude kidogo sana.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Lakini akili alizonazo katika ulimwengu hakuna. Na siku utakuko(?) na binadamu. Basi hizo nguvu zako zote, hutoki. Asema: "Msibisheni, mtu mna nguvu kama hivi halafu ... " Akiambiwa simba ogopa mwanadamu.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Asema: "Haya." Alikaa simba hata siku moja hiyo Mwenyezi Mungu akajalia mwanadamu akagonja mwitu. Katika kuingia mwitu-- ikawa akatakata vijiti vyake vyakwenda jengea. Baada ya kukatakata vijiti mpaka akafikia mahali ambapo kama nichezioni pao wale wanyama. Kufika vup! Simba tayari na wanyama wote wapo. Sasa wale wanyama walianza kumwambia yule simba kwamba simba leo umekwisha umri wako.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Mwanadamu tayari hule pale kashatokea. Walianza kwenda kaa kule walisema kwamba simba leo amefika. Wakati kashatokuwa binadamu amefika. Simba alipoambiwa vile alighazibika alikwenda(?). Amwambia: "Wee ndio binadamu". Amwambia: "Naam", amwambia: "Basi mie katika dunia tangu siku niliyozaliwa ... wanyama wote kwamba niogopi mwanadamu, basi kama wendio mwanadamu. Mie nakutafuta kwa siku nyingi sana. Kwa hivyo haja yangu tupigane." Amwambia: "A! Ama wee simba ni mbuzi sana, wewe kushajirekebisha mwaka wangapi huu?"

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M "Ebu niambie mwaka wangapi huu kushajirekebisha tangu ulipoambiwa kwamba uogopi mwanadamu. Mwaka wangapi?" "Sasa leo walikuja hapa mie hivyo tuna kazi zangu sijajirekebisha unaniambia tupigane." "Ama nakubali tupigane wala sirudi nyuma."

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M "Lakini mpaka nami nipate silaha zangu nijirekebisha. Tena nkupe masharti yangu kama utayoweza, ndio tutapigana, kama si hivyo mie sitaweza(?) kupigana na mtu mwoga." Simba aliangalia: "Ka!

Ama masharti gani?" Amwambie: "Mie masharti yangu nitakayo, ntaka unisubiri papa hapa, nendeni nyumbani nkachukue zana zangu." Amwambia: "Tayari." Amwambia: "Siamini utakuja kimbia."

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M "Nkufunge." (Kicheko) Amwambia: "Unifunge", amwambia:"Ehe", amwambia: "Tayari." Wanyama kule wapiga makofi wasema: "Hilo simba akamkwisha leo, simba hatoki leo."

Ki ML M Ehe.

Pe BH1 M Ambiwa: "Unakwisha leo simba." Asema: "Haya nifunga." Aliwambia: "Haya. Sasa ngoja nitafute kamba." Alikwenda kutafuta mbungo ambao hawezi kukata. Alikuwa akingunga nguu wa kwanza, amwambia: "Bado." Akingunga nawa pili, amwambia: "Bado." Akingunga yote minne. Akishafunga yote minne kisha akingunga na hii singo kisha akenda akingunga na nti ambao ukuwa hawezi kwanza haliwezi kumuka alishafunga.

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M ... keshamwambia kama: "Hodari ngoja papapa, nenda nyumbani na kuchukua zana zangu ... onyesha tupiganavyo." Ata kiuka binaadamu walikwenda wanyama. Aliambiwa: "Nkongwe simba tulikuambiaje."

Ki ML M (Kicheko)

Pe BH1 M "Katika ulimwengu ogopa mwanadamu, umekwishaa." Amwambia: "Ah! Nimekwisha wapi namgojea upumbavu wako, hebu jiangalie Amwambia: "Si kaniambia nimgoje ... kwisha, kwisha fungwa pole pole haji tena na utaoza papa utaoza papapa umung'nyuke(?)."

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M "Ah! Amaka simba alipokuja jifanya hivi wapi." Atoka. Amwambia: "Nasi hatuna mikono ya kukufungulia."

Ki ML M Mhh.

Pe BH1 M Tulikuambiaje."Ogopa mwanadamu kiumbe kidogo kile, fanya ya hodari fanya zunguwe(?) zao. Ilibakia kilio tu simba pale "iiiiiii" (Kicheko) mpaka likifa pale, paka likioza papo hivyo ... Tulikuambia vipi. Nayo hadithi hapo ilifika mwisho.

AA M Asante sana.

(NOTE! Some sentences are not complete because the interviewer is laughing while the interviewee is talking.)

Ki ML M ... na jina.

Pe WS M Jina Wahabi Sheami Jaa.

Ki ML M Wahabi?

Pe WS M Sheami.

Ki ML M Sheami Jaa.

Pe WS M Jaa.

Ki ML M Mhh.

Pe WS M Wa Shumba mjini sokoni.

Ki ML M Aha asante. Naam mzee, labda ungetupa tu historia fupi ya Shumba, kwamba Shumba-- ni wakazi wake ni Wapemba au ni Waunguja au ni watu gani wameanzaje mpaka ikafika waitwa Shumba mpaka mkaishi, mpaka hivi leo. Kwa ufupi unavyoweza.

Pe WS M Aa.

Ki ML M Naam.

Pe WS M Ngoja kidogo, mtafunyi hanaa hanaa-- ana wasiwasi kwanza.

Ki ML M Mhh. (A break.)

Pe WS M Asili ya Shumba hii ni watu wanatoka Tangani hii ya Tanga-

Ki ML M Ahaa.

Pe WS M -ambayo walitoka wakaja wakahamia wengine hapo Chwaka.

Ki ML M Chwaka ni mbali na hapa?

Pe WS M Ni kivuko tu.

Ki ML M Mhh.

Pe WS M Hapo tu mji ulipoondoka Chwaka wakaja mababu na mababu wakahamia hapa ili kuchunga, kuchunga mifugo. Makulima ikawa ni hapa. Sasa wakahama tena wote kule Chwaka wakaita hii Shumba ili shamba.

Ki ML M Ahaa.

Pe WS M Hiyo ndiyo ninayoilewa stori-- stori hiyo ndiyo-

Ki ML M Mhh. Hivyo kwa asili watu wametokea Tanga?

Pe WS M Ehee, Pangani.

Ki ML M Pangani?

Pe WS M Ehee.

Ki ML M Mhh. Hivyo kidogo unayo ... ndigo au siyo?

Pe WS M Siwezi kuelewa ... ndigo au vipi lakini wanatoka Pangani.

Ki ML M Pangani.

Pe WS M Ehee. Wakaja wakajenga.

Ki ML M Baadhi ya ote, wote hawawezi kuwa wanatoka Pangani, haiwezekani.

Pe WS M Baadhi yao. Hapo wakaja Chwaka wakajenga halafu wakaleta mifugo yao huku.

Ki ML M Mhh.

Pe WS M Halafu wakafanya ni shamba yao waye waki-- na mifugo wakina wakiendelea mashamba.

Ki ML M Mhh.

Pe WS M Sasa kule walitoka wote, mababu sasa, wakajahamia hapa wakaita Shumba.

Ki ML M Shumba.

Pe WS M Tafsiri shamba.

Ki ML M Shamba. Ahaa. Na ingawa neno hilo Shumba kwa maana ya shamba mmeliacha siku hizi?

Pe WS M Ehee, tunatumia Shumba tu.

Ki ML M Kwa maana ya shamba mpaka sasa?

Pe WS M A'a, kwa maana ya Shumba-

Ki ML M Kwa maana ya mji.

Pe WS M Kwa maana ya mji ehe.

Ki ML M Shamba mnatumia shamba?

Pe WS M Tunatumia shamba. Kwa maana ya mji Shumba.

Ki ML M Ahaa. Na baada ya hapo kuna wengine walikuja wageni wengine walikuja wakakaa hapa? Au mlibaki wenyewe tu? Kundi hilo hilo tu?

Pe WS M Walibakia mababu tu, sasa tu, mwisho wake tena walikuja wageni hapa wa mataifa sasa.

Ki ML M Mhh.

Pe WS M Wagunja, Wahigo, Washihiri ehe.

Ki ML M Mpaka sasa ni machanganyiko.

Pe WS M Ni machanganyiko.

Ki ML M Hivi kwa kweli wakazi wa hapa ni wale ambao toka mwanzo wameishi hapa ni mmechanganyika hivyo hivyo?

Pe WS M Wakazi wa hapa wengi wengi ni hawatu-

Ki ML M Kutoka hukoo Pangani.

Pe WS M Pangani.

Ki ML M Mhh.

Pe WS M Sasa wale waliochanganyika kidoogo, kidoogo.

Ki ML M Sawa. Lakini lugha yenu ni tofauti na zingine?

Pe WS M Lugha yetu ni moja. Pasipokuwa kojani, kojani lugha ni moja lakini yale matamshi, tefeuti. Siye hii twasema keanwa wao wasema kanwa.

Ki ML M Mhh.

Pe WS M Mhh. Sasa natafunika wao wasema anaumia.

Ki ML M Ahaa. Lakini wakizungumza mnaelewa?

Pe WS M Sawa sawa.

Ki ML M Na nyinyi mkiongea wanaelewa?

Pe WS M Wanaelewa sawa sawa.

Ki ML M Na wale wa kusini kule mwamba wakiongea mnaelewa?

Pe WS M Tunaelewa.

Ki ML M Watumbatu wale.

Pe WS M Watumbatu wale.

XX M ... maneno, siyo wazee.

Ki ML M Ehe, ehe.

Ki ML M Nanyie vile vile.

Pe WS M Ehe.

Ki ML M Ahaa.

Pe WS M Basi hapa waliingia mataifa, ... Watumbatu hapa wapo.

Ki ML M Mhh. Lakini watu kama Wareno hawakuacha asili yoyote misingi yoyote hapa. Wa zamaani hawa Wazungu Wazungu.

Pe WS M Si watambui.(?)

Ki ML M Mhh. Sawa.

Pe WS M Lakini Watumbatu, Wadigo wapo-

XX M Hawakufika huko ...

Ki ML M Ahaa, hawakufika huko kabisa.

Pe WS M Hawakufika.

Ki ML M Sawa. Na bandari ilikuwa wapi hapa, bandari yenu?

Pe WS M Bandari mpaka sasa ipo hapo.

Ki ML M Ndiyo toka zamani waliyovukia toka hapo nani(?) kuja hapa?

Pe WS M Waliotokea huko walikatiza hapa..kutua hapa wakiingia moja kwa moja Mnarani.

Ki ML M Mnarani ni kijiji-?

Pe WS M Kigomacha.

Ki ML M Ki?

Pe WS M Kigomacha.

Ki ML M Kigomacha ni kijiji kingine?

Pe WS M Ehe.

Ki ML M Lo! Mmepata maneno mengi. (Kicheko)

Pe WS M Ah jamaa, jamaa zetu-- ndugu zetu wa kibara wengi ndio waliopo wafanya kazi ya ukulima.

Ki ML M Huko Kigomacha?

Pe WS M Ee, jamaa wa bara wote wapo hapa.

Ki ML M Ahaa.

Pe WS M Na mazao yao yote tunakichukua tuleta hapa.

Ki ML M Mnaleta huku?

Pe WS M Ehe.

XX M ... usikia kuna mwito wa makangale huko.

Ki ML M Mwito wa?

Pe WS M Makangale.

XX M Makangale.

Ki ML M Makangale.

Pe WS M Ehe.

X1 M ... wasikia kuna mnara...mwisho wa kiziwa cha Pemba.

Ki ML M Na huu mnara wa kitu gani?

XX M Huo ni mnara mkubwa-

Ki ML M -wanaonyesho-

XX M -mataifa hasa-

XX M Katika "Africa" hakuna.

Ki ML M Mnara wa namna hiyo?

Pe WS M Mhh. Kama huko baharini huko unaleta kivyo ndio nayojuu-

XX M Mpaka Mombasa huko Mombasa-

Pe WS M U-- Mnara kwa ajili ya meli siyo?

X1 M Mhh. Ndiyo

XX M ... watu waweza kushitakiwa babo waweza kupata hasara ... hata chombo yoyote kama mnara hauwaki ikiwa ni wasafiri, wasafiri kuwa kupotea.

Ki ML M "Okey", ndio ndio. Naelewa, naelewa. Ahaa.

XX M Hivi sasa kwenda hapo bandarini hapo huo uko mbali sana uko lakini utauona wuuuuu mwanga wake, maana hauwaki vile pva-

Ki ML M Mhh.

XX M -pva-

X1 M -zile zinitwa-

XX M -una zuguka tu kama nini ya kio wuuuu...halafu moto mwekundu.

Ki ML M Hapo kuna kisiwa?

XX M Ni rasi tu. Mwisho wa bahara huko tena, sasa mwisho wa kisiwa itakuja bahari, na huko juu penye buta sana-

Pe WS M Sisi hapa tulipo na wao walipo ni hizi, hii bahari, inaingia mpaka msituni kule, mwituni kule.

Ki ML M Kwenye msitu tuliopita?

Pe WS M Tuliopita.

Ki ML M Mhh.

Pe WS M Sasa hii inachukua moja kwa moja mpaka huko.

Ki ML M Mhh. Nanyi mko?

Pe WS M Tuko huku. Kivuko kidogo tu lakini tukitaka twaingia gari mpaka twazunguka huko.

Ki ML M Vinginevyo mnavuka wenyewe?

Pe WS M Ehee.

Ki ML M Hivi kuna uhusiano fulani wa kishughuli kama biashara?

Pe WS M Naam, tunaleta mitumbwi tunapelekani mitumbwi twachukua twaleta hapa.

Ki ML M Sawa asante.

XX M Lakini mbali kidogo.

Ki ML M Ee?

XX M Kwa miguu mwendo saa sita kamili, kabisa.

Ki ML M Ndo! Mbali. Hiyo sio mbali kidogo, mbali sana! (Kicheko)

XX M Kwa mtumbwi kiasi ya masaa manne ndiyo.

Ki ML M E! Mtumbwi vile masaa manne.

XX M Tena zile za kutuweka zile zakuanzia ndogo kama ngarao.

Ki ML M Aa, basi ...

Pe WS M Hiyo ndiyo stori tunayojua.

Ki ML M Asante sana. Au ulikuwa na nyingine ee?

Pe WS M A'a.

Ki ML M Asante sana.

Ki ML M Labda utueleze jina lako--

Pe AJ1 M Jina langu naitwa Alhaji Juma.

Ki ML M Alhaji Juma?

Pe AJ1 M Ehe.

Ki ML M Una umri miaka mingapi?

Pe AJ1 M Miaka yangu-- nafika miaka arobaini.

Ki ML M Arobaini. Umzaliwa na mkulia wa hapa hapa?

Pe AJ1 M Nimezaliwa wa hapa hapa na nimekulia hapa hapa.

Ki ML M Na shughuli zako?

Pe AJ1 M Shughuli zangu ni hivyo kilimo kilimo.

Ki ML M Mhh. Sio mvuvi?

Pe AJ1 M Ni mvuvi mvuvi.

Ki ML M Mhh.

(Transcription of about five minutes is missing.)

Pe AJ1 M Ehee, ilikuwa ni huyo huyo simba na fisi na sungura.

Ki ML M Naam.

Pe AJ1 M Fisi anamwona simba anakwenda na njia zake na safari zake. Na sungura fuata ile fisi huku nyuma. Halafu mpaka akawauliza: "Nyinyi hasa mnakusudia nini, kunifuata mie mimi hapa?" Anasema: "Hata, sisi tunakufuata kumbe wanafuata kwa tamaa, kama yule simba ni mtu mwenye nguvu." Sasa yeye awinja yule simba akikuta nyama anaweza kumpiga. Sasa wale watapata ile mifupa watakao-- watakula wao. Atakule yale ya ndani akisha mifupa anawaacha sungura na-

XX M Fisi.

Pe AJ1 M -fisi wanakula. Sasa ikabidi mpaka ika..wake sasa hawezi akawaacha.

Ki ML M Mhh.

Pe AJ1 M Sasa wanakwenda zao weee, wanakwenda zao weee hata kafika siku hiyo. Akamwona ikawa ule rafiki umengia sana. Sasa ikiwa sasa wataka wamfanya mpumbavu. Yule simba aone kuwa mpumbavu sasa. Alikwenda zakee akifika akimwona mnyama mkubwa. ML Mhh.

Pe AJ1 M Alipiga teke moja amwangusha. Kumwangusha pale pale akinkata kichwa kisha(?)atuambia: "Fanyeni kazi, wanchune wale sasa." Sasa wale fisi na sungura walinchuna, wakinchuna simba akalala pale mfanyakazi huyo, kankaa pale kanlala watizama. Wao wanchuna wale, yee kashafanya zile nguvuze sasa wafanyakazi wao wanchune akawakisha nyama wakieka hii. Chungu nzima yu kubwa.

Ki ML M Naam.

Pe AJ1 M Wakieka sasa, walitoa zile za moyo mafigo yale na kila kitu kile kizuri kizuri zile maini wakieka hapo. Sasa na ile mifupafupa wakieka wakichanganywa wakieka huko. Na zile za matumbo tumbo nyingine mbaya mbaya zile nyama nyekundu wakieka huku, akigawa mafungu matatu.

Ki ML M Mhh.

Pe AJ1 M Alipogawa mafungu matatu. Sasa yule fisi ndiye mgawanyi akimpa yakwe simba akimpa ile inayo mifupafupa. Sasa yule fisi akijieka ile ya nzuri nzuri ya mafigo na yule simba kumbe ndio itakayo ile ndie atumiayo sana ile nzuri ile.

Ki ML M Mhh.

Pe AJ1 M Na yule sungura akipewa hile mwenye kugawa ni yule fisi. Sasa alikaa yule simba watizama tutakisha akawambia: "Haya mzee hiyo yako, yako nyama." Akimwuliza yule simba akimwuliza: "Hii yangu?" Hiyo akimwambia "Hii ya kwangu mimi." Yule fisi asema: "Hii ya kwangu mimi." (Kicheko) Ni nzuri ee. Sasa sungura, sungura yako hiyo--

Ki ML M Mhh.

Pe AJ1 M Haya sawa sawa. (Says this to someone else) Basi nisongezea maana nachoka hapa. Yule fisi akiichukua ile mifupafupa. Kwanja amwona na meno ya sasa mbele(?) ile mifupafupa, akenda pale kumwekea. Alinrukia alimpiga kofi moja kubwa sana.

Ki ML M Mhh.

Pe AJ1 M Akinlenga kule akigaagaa kipapatika(?)

Ki ML M Mhh.

Pe AJ1 M Sasa simba akimwambia sungura: "Changanya nyama yote changanye kwa pamoja." Akisha tayari sungura atetemeka pale, aki-- akichanganya ashawambia: "Gawanya mafungu matatu." Sasa yule agaagaa kwa lile kofi. Sasa sungura akigawa akichukua ile nzuri akieka ile mafigo na ile ... akieka nzuri pakwe kama vile alivyogawa yule. Na yule alieka-- sasa akichukua ile nzuri akenda akimwekea simba. Akimwambia: "Hii nzee yako."

Ki ML M (Kicheko)

Pe AJ1 M Sasa hiyo ya nani amwambia: "Hii ile mifupafupa, hii yangu na hiyo na ile mifupafupa mingine", akimwambia hii ya fisi. Sasa simba alintizama sungura alimwuliza: "Ulifundishwa na nani kugawa

Ki ML M Mhh.

Pe AJ1 M Amwambia: "Kofi la fisi" (Kicheko) "Kofi la fisi ndio lilonifundisha mie sungura kugawa nyama. Kwa sababu lile kofi unalompiga, naona kagawa vibaya ile kwa sababu wewe ndio mfanyakazi bwana. (Kicheko) Uliyefanya kazi...kupa mifupa bwana. Amwambia: "Asante sana." Sasa akichukua nyama ya akila yule ka--

yu-- taabani kwa kofi. Sasa wakichukua ile mifupafupa, ... ataka mfanye mpumbavu atakashamwona yeye kashajifanya na akili. Sasa kampiga kofi moja. Sasa yule kuchanganya ... kashachanganya akitakisha igawanya aliweka ile mzuri ya mafuta akampa yule, simba. Sasa hata kushakugawanya alimwuliza: "Ulifundishwa nani kugawa wanyama hivyo?" Alimwambia: " (Kicheko)... twafundishwa lile kofi ulilompiga. Kofi la fisi ndio lilonifundisha mimi kugawa nyama." Amwambia: "Asante sana."

Ki ML M Nami nashukuru sana, nashukuru sana.

(Transcription of the rest on side A is missing.)

XX M Ilikuwa bwana mkubwa mmoja, alikuwa, ana shida ya matatizo ya nyumbani.

Ki ML M Mhh.

XX M Ana jibwa wake, ana sifa kama binaadamu ana akili kama binaadamu.

Ki ML M Naam.

XX M Hapo bwana mkubwa alifikuwa na matatizo ya kinyumbani, alikwenda kwa mtajiri, kwa tajiri mmoja. Akimwambia: "Ee bwana mpaka sasa hivi nimefikwa matatizo ndani ya nyumba yangu, kwa hivyo namwika jibwa wangu rahani, kwa hivyo nipate kaondoe matati-- matatizo yangu."

Ki ML M Naam.

XX M Hapo yule tajiri alimwuliza: "Jibwa huyu ana sifa gani?"

Ki ML M Mhh.

XX M Alimwambia: "Kama utakavyoo, utakavyo mwamrisha yuko tayari atakutumikie." Amwambia: "Hewala." Aliingia ndani, yule tajiri akimpa yule mzee m-- haja anayotakia.

Ki ML M Naam.

XX M Akimpa fedha, akiondoka. Akimwambia:"Haya jibwa wangu, wee jibwa nimekuika hapa utamtumikia huyu mzee kama atakayo kutuma."

Ki ML M Mhh.

XX M Sasa yule alilala tajiri yule siku ya kwanza, siku ya pili walikuja majambazi.

Ki ML M Mhh.

XX M Majambazi kuja pale walivunja nyumba, wakaichukua mali yote. Jibwa alifuata tu, hakufanya jambo lolote. Alifuata mpaka akenda iona mali inamotiwa. Halafu alirudia akija kika kule kule kule tajiri.

Ki ML M Mhh.

XX M Sasa tajiri asubuhi kuamka nyumba imeshavunjwa, mali yote imechukuliwa. Hapo tajiri yule alisema: "Jibwa huyu nilipewa kwa sifa. Kumbe si chochote yule bwana ilikuwa, anifanyia hadaa."

Ki ML M Mhh.

XX M "Kunichukulia fedha yangu, lakini kwa hivyo mimi siwezi nkakubali nitamfuatia mwenyewe." Yule jibwa alimwona hangaika, yule tajiri amwona jibwa hangaika, kusikia maneno yale.

Ki ML M Mhh.

XX M Hapo kila akitaka ondoka yule tajiri jibwa afuata njia hio. Halafu yule tajiri aliona kuwa eh, "hebu nimfuate huyu jibwa". Alifuata jibwa yulee, akamfuata jibwa, akamfuata jibwa ata akifika kule, mali inamotiwa mote yule jibwa akaingia mle.

Ki ML M Mhh.

XX M Kumwonyesha yule tajiri kuwa mali yako hii.

Ki ML M Mhh.

XX M Yule tajiri aliririka saa hile hile. Alisema: "Ama jibwa huyu kwa siku tulizoikiana ahadi ya kuwa aridishwe kwao." Haitafika, kwa hisani anyonifanyia.

Ki ML M Naam.

XX M Hapo aliandika barua yule jibwa alimfunga hapa. Kuwa ende zake kwao ile barua ilieleza kuwa jibwa amesharu-- amesharudi kwao.

Ki ML M Naam.

XX M Na hakuna tena ujira, ujira wake ulimaliza jana tu kwa kazi aliyoitekeleza.

Ki ML M Mhh.

XX M Basi yule bwana mwenye kumwika yule jibwa wake kule kwa tajiri, kumwona yule jibwa atokezea, aliona ama jibwa ameni-

Ki ML M Angusha.

XX M -ameni angusha. Hapo kaingia ndani, kuingia ndani alimtupia bunduki kabla hajafika-

Ki ML M Alla alalalalaa!

XX M Hapo akija akifika pale akija akitizama ile barua nayo-

Ki ML M Aa t-t-t!

XX M Akija-- akiyasoma yanayoandikwa mule, sasa ilikuwa faleki, ndio maana ya kuwa utajuta kama mwenye mbwa alivyojuta. Ndiyo hiyo mwisho wake.

Ki ML M Ahsante sana.

XX M Ehee.

Ki ML M Naam. Labda ungetueleza tu-

Pe SS2 M Tayari?

Ki ML M Ee, tayari.

Pe SS2 M Kwanza jina langu ni bwana Shame Said.

Ki ML M Naam.

Pe SS2 M Nikiwa na umri wa miaka thelathini na mbili.

Ki ML M Aha.

Pe SS2 M Ni mkazi wa hapa kwale Micheweni.

Ki ML M Umezaliwa hapa hapa kwale Micheweni?

Pe SS2 M Nimezaliwa hapa hapa nimekulia hapa hapa.

Ki ML M Hivyo na baba na babu wako walikuwa wanaishi hapa-

Pe SS2 M Na mpaka leo hii wanaishi hapa hapa.

Ki ML M Naam. Sasa kuna sehemu ya historia ya Micheweni tumeelezwa inavyoelekea una maneno mengine ambayo unataka kutu...-

Pe SS2 M Kidogo.

Ki ML M Ndio.

Pe SS2 M Nahisi kama wanakiacha historia ya Micheweni.

Ki ML M Mhh.

Pe SS2 M ... baada ya wale Masharifu wanne wale, walipokuja, wanawake wawili na wanaume wawili.

Ki ML M Naam.

Pe SS2 M Sasa kutokana na shughuli zao walizokuwa wakifanya.

Ki ML M Ahaa.

Pe SS2 M Baada-- kwa sababu kama walivyoeleza kama walikuja watu sabini na nne.

Ki ML M Mhh.

Pe SS2 M Miongoni wa watu sabini na nne, wanne walikuwa ni Masharifu.

Ki ML M Naam. Endelea tu, endelea.

Pe SS2 M Miongoni wa watu sabini na nne waliokuja pamoja.

Ki ML M Mhh.

Pe SS2 M Sasa wanne walikuwa ni wale Masharifu wawili wa kike na wawili wa kiume.

Ki ML M Aha.

Pe SS2 M Sasa kutokana na shughuli zao zile na elimu(?) walivyokitumia. Ilibidi wa kiwana wakitumia njia ya wana kiholela.

Ki ML M Aha.

Pe SS2 M Wale watu wale wale-

Ki ML M Wale sabini na nne.

Pe SS2 M Ehee, sasa wakiwana kiholela.

Ki ML M Lakini nikuulize hapo tu kwanza. Walikuwa Masharifu wanne, hao wengine walikuwa watu gani?

Pe SS2 M Ni watu wa kawaida ambo walihama kutoka sehemu hii-- ... sehemu za bara kuja huku.

Ki ML M Mhh.

Pe SS2 M Na wakapita kwanza huko walikokuta tangu(?) ya mwanzo kule alikoizungumza sijui kama-

Ki ML M Ehee.Mhh.

Pe SS2 M -halafu wakapita Panga Mariamu, halafu ndio-

Ki ML M Wakaja panga ya wafu.

Pe SS2 M -ya wafu, ile ya mwanzo ile. Sasa baada ya kuja huku, sasa baadhi waligawanyika kidogo. Sasa walibakia katika mji ule wa Micheweni, sasa...na hatua hiyo ikawa sasa wana wana-

Ki ML M Wenyewe kwa wenyewe.

Pe SS2 M -wenyewe kwa wenyewe. Sasa ndio waliokuwa mbali nao kidogo ndio sasa wakasema huko ni hakwendeki ni Michawini, kwa sababu huyo kutokana wanatumia kitu uchawi. Kwa kuwa(?) mara kwa mara.

Ki ML M Mhh.

Pe SS2 M Kwa hiyo ndio lile jina likapatikana Michawini lakini likabadilisha nakuwa.

Ki ML M Michaweni.

Pe SS2 M -Michaweni. Sasa alafu na ile asili ya kiuyu nikuwa baada ya yule bibi kuona matatizo yale, ya pale Michawini.

Ki ML M Ndio.

Pe SS2 M Yeye alisubiri wenzake wakalala. Mara tu walipolala yeye alikimbia, akarudi kule kwenye Panga ambako-

Ki ML M Ile Mariamu, Panga Mariamu?

Pe SS2 M Ehe, ambako kulikuwa pana na mbuyu.

Ki ML M Mhh.

Pe SS2 M Sasa asubuhi walipoamka yule bibi hayupo. Sasa ikabidi wamtafute, "Yu wapi yu wapi", hawajui ... kwa sa-- mmoja akatoa rai hata nenda aka-- angalie kule tuliko toka kule kwenye Panga, pengine huwenda ikawa kanarudi.

Ki ML M Mhh.

Pe SS2 M Sasa walipokwenda walimkuta yule bibi, yuko.

Ki ML M Naam.

Pe SS2 M Kwa hivyo ndio akaja akatoa taarifa, kwamba kile kibibi, kiuyu wapi? Kule mbuyuni.

Ki ML M Mhh.

Pe SS2 M Sasa ndio likapatikana jina la asili kiuyu mbuyuni na mpaka leo wanakuita hivyo hivyo kiuyu mbuyuni.

Ki ML M Kiuyu ikiwa na maana gani?

Pe SS2 M Kiuyu kikiwa kile kibibi, ki-- maana kikiwa kilirudi.

Ki ML M Kiuyu-- kuuyu ni kurudi?

Pe SS2 M Uu-- maana yake ... kuhusu ni kurudi.

Ki ML M Kuuyu?

Pe SS2 M Ehe.

Ki ML M Hivyo kiuyu mbuyuni ni kwamba karudi kibuyuni.

Pe SS2 M Karudi kwenye mbuyu-

Ki ML M Kwenye mbuyu.

Pe SS2 M Kiuyu ni kurudi. ... jina kiuyu mbuyuni na mpaka leo hii inaitwa hivyo hivyo kibuyu mbuyuni.

Ki ML M Sawa.

Pe SS2 M Kwa sababu hivi viuyu vilikuwa viwili kuna hicho kiuyu mbuyuni na kuna hapa na vitatu kuna kiuyu cha ngezi halafu kuna kiuyu mirungwi.

Ki ML M Hicho cha ngezi na cha mirungwi vina u-- historia yoyote?

Pe SS2 M Hivyo-- japo kama vina historia lakini sijui kwa sababu ni mbali kidogo kwa sababu kiuyu cha ngezi ni konde mbele, halafu na kiuyu mirungwini ni sehemu za chaki.

Ki ML M Ngezi manaake nini?

Pe SS2 M Ee?

Ki ML M Ngezi?

Pe SS2 M Kiuyu cha ngezi?

Ki ML M Mhh.

Pe SS2 M Ama hata hiyo ngezi, ingenishinda kabisa kueleza kwa maana waliokusudia mpaka wakakita kama ni kiuyu cha ngezi.

Ki ML M Mhh. Na nikuulize suali jingine. Unasema kuwa Masharifu wanne sio saba?

Pe SS2 M Masharifu walikuwa ni wanne watu wote walikuwa ni sabini na nne. Masharifu walikuwa ni wanne-

Ki ML M Walikuwa wanne.

Pe SS2 M -wanawake wawili na wanaume wawili.

Ki ML M Hivyo sio saba?

Pe SS2 M Ata. Nani(?) alisema saba?

Ki ML M Ndio nilikuwa nataka tu kusisha na watu wengine walionipa hadithi ya watu saba, Washirazi saba waliokuja sehemu za huku sasa ... Micheweni.

Pe SS2 M Hata. Hata hapa skuli pale pana, pale peke-- peke yake pale pana jina maalum paitwa Pashamemata.

Ki ML M Ee, Shamemata ndio nini?

Pe SS2 M Shamemata ni jina la mtu.

Ki ML M Ehe. Alikuwa nani?

Pe SS2 M Yeye ni mtu kutoka sehemu hizi hizi za bara.

Ki ML M Mhh.

Pe SS2 M Ambaye yeye alikuja lakini hakufika huku mjini, yeye alikuja mji tayari, ushakuwa tayari huku Michawini.

Ki ML M Mhh.

Pe SS2 M Na mas-- maskani yeshakuwa tayari. Lakini sasa yeye ikawa ni mtu si mashuhuri sana, kwa hiyo akabakia pale.

Ki ML M Akajenga mji wake?

Pe SS2 M Akajenga mji wake peke yake. Na ikawa ni mtu shughuli za-- anajishughulisha, ana maswala ya ugang'ugang' wa kinyeji.

Ki ML M Mhh.

Pe SS2 M Sasa yee maskani yake yakawani ni pale.

Ki ML M Ahaa.

Pe SS2 M Sasa watu walipoondoka huko vijini, "Ah, wenda wapi?", "Endapo Pashamemata".

Ki ML M Mhh.

Pe SS2 M Kwa maana ya lile jina la yule mtu, na hapopa eshamemata(?), nyumba ni Peshamemata.

Ki ML M Ndio.

Pe SS2 M Sasa mtu yule akendelea kuishi pale mpaka muda aliondoka. Na kwenda zake. Lakini eneo hilo mpaka leo hii-

Ki ML M Inaitwa Pashamemata.

Pe SS2 M Inaitwa Pashamemata.

Ki ML M Ahaa. Sasa bwana ... simuliwa wewe kuhusu wale wanawake wawili na wanaume wawili.

Pe SS2 M Masharifu wanne.

Ki ML M Masharifu wanne.

Pe SS2 M Ehe.

Ki ML M Sharifu moja wa kike ndie alirudi?

Pe SS2 M Ndie, alirudi kiuyu baada ya kuona ile hali mbaya ambayo waendelea wenzake naye alikuwa haipendi. Maana ile kuwa na kiholela.

Ki ML M Mhh. Kule alipokwenda hakuolewa? Au aliendelea kuishi mwenyewe?

Pe SS2 M Sasa kwanza alianza kukaa peke yake na baadaye wale jamii nyingine au wale baadhi ya watu wengine kuona vile, kama pana mauaji(?) ya kiholela, baadhi ... fuata yule-

Ki ML M Kumfuata.

Pe SS2 M Sasa kule wakenda wakaanzisha mji mpya mji wa kiuyu mbuyuni. ... unaendelea na baadhi ya watu wengine kutoka sehemu mbali mbali wanaingia kidogo kidogo.

Ki ML M Hivyo haijulikani aliolewa na nani?

Pe SS2 M Hata.

Ki ML M Haijulikani.

Pe SS2 M Haijulikani aliolewa na nani.

Ki ML M Na katika watu sabini na nne ufikiri kwamba ongea kuwa watumwa hawa sabini.

Pe SS2 M Kuwa watumwa, mwanzoni walikuja kama sio watumwa. Sasa hatujui huko kwao walikotoka. Kwamba walikuwa watumwa.

Ki ML M Na mwenyewe wako(?) Warabu kwa asili?

Pe SS2 M Ehe, asili yao walikuwa Warabu na hivyo yule kasema kama walikuwa ni Washirazi, lakini walikuwa ni Warabu. Kwa kweli.

Ki ML M Mhh. Sawa kabisa.

Pe SS2 M Na sasa ile kwenda na kurudi ile kwao wanakurudi walikuwa wanakwenda mmoja wakirudi wanarudi ... watatu wanne sasa jamii inakuwa ina... kuwa kubwa.

Ki ML M Halafu kuna lile kaburi pale. Huna habari nalo kuwa ni la nani haswa?

Pe SS2 M Kaburi lipi?

Ki ML M Karibu na msikiti. Sasa katikati ya msikiti na pango lile pango la wafu kuna kaburi.

Pe SS2 M Sikumbuki la nani.

Ki ML M Mhh.

Pe SS2 M Kabisa.

Ki ML M Wakasema la zamani wamelikuta hapo-

Pe SS2 M Hata nami silikumbuki.

Ki ML M Haya asante. Asante sana.

Edited by TR, November 1996

Proofread by MY

DAHE 104

Place: Mtwara, Chuno

Time: 12.10.1990

Interviewee(s): 1. (BM5), 2. (HS2), 3. (AM9), Anonymes (XX), (X1), etc

Interviewer(s): 1. T. Sengo (TS), 2. David Massamba (DM)

Recorder: Sony Professional

Language: Standard Swahili (Ki)

Topic: 1. History of Chuno, 2. Meaning of names Chuno and Mtwara, 3. About the life during the colonial period, 4. Marriage customs in the old days, 5. Co-operation among citizens, 6. Value of money

Pw XX M Mzee bwana Masudi nianze mimi. Anza wewe.

Ki TS M Naam. Kwanza tueleze jina, jina lako.

Pw BM5 M Nitaeleza jina kwanza, maanake kuna tofauti jambo moja, lugha zinazotakiwa hapa, ni zile lugha za kizamani za Kimakonde. Si ndiyo?

Ki TS M Hapana, ni Kiswahili.

Pw XX M Kiswahili cha pwani.

Ki TS M Cha pwani.

Pw BM5 M Kiswahili cha pwani?

Ki TS M Naam.

Pw XX M Ehee. Watu wa Mwambao natulikuwana Kiswahili chetu.

Pw BM5 M Kuna kifungu hivi yaani inafuata sehemu mtu ulikokulia.

Ki TS M Naam.

Pw BM5 M Unasikia?

Ki TS M Naam.

Pw BM5 M Mimi Kiswahili cha mbao. Umesikia? Itakuwa sikielewi.

Ki TS M Naam.

Pw BM5 M Kwa sababu nimeondoka hapa nimeishi mji mwingine.

Ki TS M Naam.

Pw BM5 M Unguja. Sasa Kiswahili cha, cha Kimwambao hakikunijaa sana isipokuwa Kiswahili cha Kiunguja, unasikia, kule nilikokulia ninacho sana.

Ki TS M Basi, wewe utatusaidia katika kiwango chingine tutakapokuja kulinganisha. Ehee, wewe utatusaidia.

Pw BM5 M Basi haifai kuanza miye.

Ki TS M Bora anze mwingine.

Pw BM5 M Mimi nimalizie.

Ki TS M Hewallah, asante, asante. Baba?

Pw HS2 M Mimi ni mzaliwa wa humu.

Ki TS M Naam. Taji jina?

Pw HS2 M Hassani Selem.

Ki TS M Hewallah, bwana. Umri wako waweza kupata miaka mingapi sasa?

Pw HS2 M Waweza kupata kama miaka hamsini na tano au sitini, basi.

Ki TS M Hewallah, bwana. Naam, je, umesoma Korani?

Pw HS2 M Sikusoma.

Ki TS M Shule?

Pw HS2 M Sikusoma.

Ki TS M Kazi zako katika maisha?

Pw HS2 M Kazi zangu ni mvuvi.

Ki TS M Naam. Na makulima unalima?

Pw HS2 M Nalima.

Ki TS M Hewallah. Basi tunaomba utueleze kiasi unachojua kwa kutumia lugha ya Kiswahili cha mji huu cha zamani, historia ya mji huu. Chuno imetokatoka wapi? Na la jiji maana yake nini na watu wa hapo wametokea wapi na hivi?

Pw HS2 M Aah. Mimi Kiswahili chetu tunachosema sikuzote ni kama hivi ninavyosema. Hakina tofauti. Kama nitachukua Kiunguja aidha Kimakonde zaidi, hapana. Lakini kama hivi ninavyosema ndio tunavyosema. Mnanisikia?

Ki TS M Naam. Tueleze basi historia ya kiasi.

Pw HS2 M Historia yangu katika mchi huu wa Chuno. Sisi twalikuwa na mchi ukiitwa Ntwala kule bondeni.

Ki TS M Naam.

Pw HS2 M Tulipokuwa tumekaa walikuja Wazungu ili kwa sababu tunataka kuitoa hapa hii Ntwala, mchague mahala pa kwenda. Unanipata lakin...?

Ki TS M Naam, bila shaka.

Pw HS2 M Sisi tulipotoka kule Wazungu wakasema ya kwamba kama sisi tumeshapima hapo mahala. Katika kupima hapo mahala ninyi chagueni kwanza mahala gani mnapotaka. Sisi tukataka kule... nani hapa Magomeni. Wengine wazee wengine wasema, sisi hatutaki kukaa Magomeni. Tukikosekana kupata hapo Chuno, basi kwanza tunataka twende tukaone. Tukaingia ndani ya gari. Lakini hadi nchi yote iliko kulekule Ntwala. Mpaka tumefika sisi hapa humu, humu, humu, humu. Hapo itakuwa soko. Hapa patakuwa msikiti. Baada ya kupima wale Wazungu mpaka tukapata na majumba yetu haya. Tukasema, basi, kama ikiwa si kukaa kule mitumbwi yetu kukaa hapa, ni hapahapa tu. Maana ya Chuno ni 'hapahapa'. Lakini hii Chuno haiko hapa. Iko nyuma huko. Pale machinjioni wanapochinja nyama. Kama waliwahi kukwenda ndivyo pale ile inaitwa Chuno. Lakini tukachanganyisha sisi kwamba panatufaa hapahapa, maana ni karibu.

Ki TS M Na Chuno maana yake nini?

Pw HS2 M Chuno? Hao watu wa zamani hawakunipa tafasiri hii.

Ki TS M Na Ntwara maana yake nini? Ntwara? Twalikuwa na nchi ikiitwa Shangani. Kule hoteli ya... alikuwepo Mzungu mmoja akiitwa Overdeiki kule. Palikuwa majumba hapo. Kwa bahati nzuri walipokuja hawa Wazungu wasema, 'Hapa nataka mtoke hapa. Maana yake hii Chuno, mara hii ni mara ya... ya pili, inavunjwa.' Ikenda ikavunjwa ile, Shangani ile. Wakapeleka Ntwala. Wale watu wa zamani wakasema kwamba hii ni Ntwala. Madhali wale wamechukua kule. Na sisi tutachukua hapa. Ndio wakasema, 'Hii Ntwala, maana wanitwala, Wazungu.'

Ki TS M 'Wanitwala', maana yake wamechukua?

Pw HS2 M Wamechukua, ee. Kama hivi.

Ki TS M Haya asante, umemaliza?

Pw HS2 M Nimemaliza.

Ki TS M Hewallah bwana,

Pw AM9 M Sasa pamoja na wazee wenzangu waliotangulia.

Ki TS M Taji jina.

Pw AM9 M Jina langu ni Athumani Mussa Mfaume, Mshaweji. Na elimu yangu elimu ya watu wazima, hatua ya nne na tano.

Ki TS M Naam.

Pw AM9 M Nimezaliwa kijiji cha Ntwara. Na nimechukua nafasi ya jina sasa hivi kuwa mkoa wa Ntwala, nilipozaliwa kijiji cha Ntwala, kama mzee mwenzangu alivyosema, chini ya nyumba ya RC. Ni kweli mzee alivyosema. Chuno ime... imepata nafasi kuingia kama mara moja mbili tatu. Kulikuwa upande huu wa Shangani. Kuna Shangani hii ya Mangoila ni Shangani. Ikahama ikienda Chuno. Kule Chuno baharini kwake katika bahari ya Hindi, kulikuwa na miti mitatu minne, michu ile, Chuno mitu. Miti ile, pana Chuno hapa. Kitu ambacho nimeambiwa. Miti ile ilipata nafasi ya kuingia Chuno. Kuingia kwenye jina hilo. Kitu kama hivi nimeambiwa. Waliishi wazee pale. Bahati nzuri wakati ule ni utafiti tu. Sehemu gani ntu anaweza akakaa akakidhi haja zake? Kwa uvuvi, kwa kuwinda samaki, na bandari ambayo ina hoba. Unaweza kuweka ngalawa? Halafu ya Bahari ya Hindi isipige, isiharibu ngalawa zile. Kuna amani wakati wa kwenda nje na kuingia ndani. Unaingia ndani. Wakaona basi, ni lazima kuingia ndani zaidi. Kuingia ndani zaidi kwenye mfereji wa maji, kuingia kule ambako ni Mtwara kule. Ile Ntwala yenyewe kutoka Chuno, kulikuwa na sababu ambayo imewahamisha. Kulikuwa na Litwala pale, Litwala.

Ki DM M Ndio nini?

Pw AM9 M Litwala ni kufumania ... ya shangazi yangu, mafumanisi. Waligombana watu pale mafumanisi. Ukawa upone. Ule ugoni ulipochukuliwa pale, mahala gani tunakwenda kuzungumzia, ni pale ndani Ntwala. Wakakaa kuzungumza, 'Kwa nini wewe umemchukua nke wa mwenzio? Umetwala nke wa mwenzio. Mbona uninyakula njawe fulani yuno ninyakula? Wepo vena haya? Wewe huna haya? Watu wana ndugu na kuchukuliana wanawake.' Wazee pale wakasema, 'Ametwala nke wa huyu, kafanya kosa, kutwala.' Wazee watafanyaje sasa? Na wakati ule binadamu ni binadamu wa namna yake tu. Wanavaani? Nguo za kasuba, za miti, mibuyu. Wanafanyaje? Hakuna vibiriti. Kuna miti, mpaka leo ipo. Unapekecha tu moto, moto unatoka. Kabla kiberiti hakijaundwa wale waundaji wa viberiti hawajazaliwa vilevile. Lakini watu walikuwa na hii. Imekaa kichwani. Kwamba anakulaje, anafanyaje? Walivuka pale Ntwala, walipotwala pale, wakenda

ng'ambo ya pili. Kuna kijiji kinaitwa Msemo. Wakenda wakafanya bunge lao pale. Tukafanya masemo. Kiswahili cha zamani hicho. Maneno ya kutafuta musili ya ule ugoni. Twende tukakutane pale. Tufanye masemo. Masemo ni kujadili kama tulivyokaa hapa. Kujadili amani, 'yalitwala juu ya nkewe'. Wazee wakakaa pale na mambende yao. Kulikuwa na miti inavaliwa. Lakini kulikuwa na mambende vilevile.

Ki DM M Ndio nini mambende?

Pw AM9 M Mambende ni nguo ambayo lilelile gogo lililochongwa na kupigwapigwa. Inapigwa na kuwa laini kabisa. Halafu unavuta huku kama wanaume. Umetupia huku, na huku unatupia huku. Wanawake kama dhabu ileile mbuyu.

Pw XX F Wanaita likongoti.

Ki DM M Likongoti, ee?

Pw AM9 M Ileile, wakenda wakakaa pale wakafanya masemo. Basi kama ni masemo, na hapa tulipo, jina lake ni Nsemo. Kile kijiji cha namba ya pili, mpaka lao ni Nsemo. Kama nilitwala, maneno yamezungumzwa katika Litwala. Pale tulipotokea Ntwala ni Ntwala. Halafu palepale Ntwala pale palikuwa na, palikuwa na mnyama huyu... ndogoro inaitwaje Kiswahili? Huwezi, unampeleka katika nyati yule. Kule nyumbani ni ndogoro, laini, nzuri kama kongoni, nzuri sana, mkubwa, ni mtamu. Akakimbizwa na mawinzi, mbwa mmitu, karibu na nyumba ile ya RPC. Pana kibao pale, shule ya ufundi ile. Pana kibao. Sasa li kidogo. Zamani kilikuwa kikub... kikubwa sana. Kulikuwa na mabata pale, wanawinda, kwa mishale tu. Wanapiga vijana pale. Na sisi tumewahi kwa umri yetu kuyaona mabata pale. Likafukuzwa, ndogoro moja kubwa porini huko. Wakwangwala, yaani wangoni, wakwangwala, wangoni, ni ngoni kwelikweli. Ni ngoni ya mingoni.

Pw XX M Mikwangwala.

Pw AM9 M Mikwangwala. Na hilo jina walichukua mikwangwala hilo. Ni ngoni kabla ya Wangoni hawa. Akafukuzwa yule ndogoro akaja pale, akaingia katika bwawa lile la kiyangu. Pana mtaa wa Ntwala pia yangu vilevile. Umegandana na huo. Akatumbukia kwenye mafuti yake yakazama kwenye matope mpaka kwenye mapaja. Hawezi kutoka. Hawezi kutoka, mpaka pale achinjwe palepale. Wale wazee wa Ntwala wale wakapata habari. Kuna nyama wenu, ni wenu ninyi wenyewe nyama yule. Ametumbukia katika bwawa gani? La Kiyangu. Na Kiyangu mpaka leo ipo. Wakwangwala wametokea wapi? Hakukuwa na miji, watu wanapita tu na wanawinda tu, kutafuta nyama tu. Watu wa Ntwala wakawagomea wale. Nyama si wenu, yangu-yangu, yangu-yangu. Ndilo lile bwawa pale likaitwa piyangu, kwa kugombania huyo nyama huyo. Sasa historia iliendelea. Maana takriba dunia hii haikuwa na ntu mahala gani anaishi. Kama nilivyosema awali ni kutafuta tu windaji. Watu wanavuka katika makongwa. Hakuna ngalawa, hakuna mitumbwi.

Ki DM M Magongwa ndio?

Pw AM9 M Ndio, magongwa ni mtu mmoja, umepigwa tu gozi la mti. Limepanikwa na vila vyake vile, kufungwa huku na huku. Hakuna ngalawa ya kuchonga, huna cha kuchongea. Halafu wamekaa pale ndani, anavuka. Nalikongwa mpaka upande wa pili. Watu wanafariki sana. Maana maji yanapita rasha lakini lazima haja yake ya kidhi afike ng'ambo ya pili. Ende katika masemo. Atoke katika mitwala. Dunia inakwenda. Na watu haohao kwa kuongeza yangu nadhani walizunguka zunguka wakafika kijiji cha Msandawe. Kule walipokwenda wanatafuta tu sehemu tu. Tunaishi namna gani? Tutakaaje? Wakakuta ule mchanga uleule. Una namna yake ni mchanga mnene kidogo, ee. Ndani yake mna changarawe nene nene hivi. Kuna nchugu nyingi tu, mpaka leo upo. Akauzoa, akautazama akamwambia, mzee mwenziwe, 'Unaona nyanga nkulu? Unaona nyanga nkulu?' Asema, 'nauona'. Nyanga nkulu kwa maneno ya kisasa Kiswahili chenu, wale walisema ni mchanga mkubwa. Kwa maneno ya kisasa ndio ile inaitwa 'mchanga mkuu'. Kwa sababu kutokana na ardhi yake nene kila jambo lilikuwa na maneno yenye maana yake. Nyanga mkulu, ikawa hivyo... kwa sababu ya mchanga huo. Bibi tia maji. Kwaji kumwuika kulikuwa na nini? Wazee tu ntu amekaa

pale. Amekuja peke yake. Amevamia masimba, majoka makubwa. Akawa Sugu tu. Akakaa kule Ntepwei. Dibumwike, dibumwike, maana dibumwike ni jitu kubwa kubwa ili liliweza... Watoto wadogo hawapiti pale. Wakipita hata kama amepotea sema, amepotea kwa nzee.

Ki TS M Inaelekea yule nkuu ni ngumwike (kicheko).

Ki DM M Ni ngumwike (kicheko).

Pw AM9 M Nikumwike.

Ki TS M Nikumwike, naam.

Pw AM9 M Nikumwike. Kwa hiyo hawa watu walifanya kazi hiyo. Hawajakua, utafiti wao sehemu gani tutakaa. Na halafu vile huwezi ukaishi kwa ulimwengu huo. Mimi nimewahi roho yao kabisa, na hawa wazee wangu, kaka zangu hawa wamenipita hapo. Lakini kilichofanyika kwa wakati ule kila sehemu ilikuwa mbali. Hata sisi tulipotoka kuitaka Dar-es-Salaam, ni siku karibuni tu, thelathini na nane. Hatuna akili sana, thelathini na tisa, ee. Basi ni mwezi mmoja kutembea. Dar-es-Salama ilikuwa mbali sana. Lindi ilikuwa mbali sana. Kutoka Mtwara kwenye masemo, kwenye Litwala pale, kwenda Mikindani, mji mkuu wa zamani, ilikuwa mbali sana. Na hata sisi kwa wakati wetu, ukikutana na watu wengi sana, kama unakwenda Mikindani. Basi ni watu watatu ama wanne. Watu watatu ama wanne. Kwa hiyo, nyongeza ya mzee Bwana Azani hapa, ni kwamba shamba la katani halijakuwa bado. Watu wa Ntwala wameshajenga huko Ntwala, hapo chini kwao hao. Na wazazi na sisi tuliobakiabakia. Kujulikana kama litakuja shamba la katani hakujulikana. Shamba la katani lilikuja baadaye. Mzungu nani? Linda, dada, mama, jama... Nani Linda yule? Linda, Mjerumani mmoja, kuanzisha shamba la katani.

Pw AH M Ilikuwa lini?

Pw AM9 M Eee?

Pw AH M Mwaka gani?

Pw AM9 M Nadhani hapa mimi nyuma yangu, kama... ishirini nadhani, ishirini au kumi na tano, ishirini au kumi na tano. Vita vya pili, baada ya vita vya pili... vita vya kwanza. Vita vya kwanza vita vya kumi na nne. Na mimi sikuzaliwa Mjerumani. Nimezaliwa Mwingereza tu. Mwana Hassan vile Mwingereza tu, vita vya kumi na nne. Shamba la katani. Shamba la katani wenyeji wake waliowakuta pale watu wa Ntwala, ni hao babu zetu sisi, na mashangazi zetu. Na mwisho ndio hao miliki ya Hamedi yuko hapa. Kina usemi gani ha...? Kinaharibu na... jina? Nani mzee?... Kina Ali Muhammad. Ee, kina nzee Riteka, kina Ninganya. Watu wafupi wenye nguvu, kina Nasari. Wao kazi yao, amari yao kubwa sana, lazima wampate kasesher.

Ki TS M Naam.

Pw AM9 M Kama hakuna kasa, sisi tunaingia katika ngozi la kasa lile, ndani mule, tunaparata. Mimi na mwenzangu hao. Ndipo unajua kama lao nimekula samaki nzuri zaidi. Na hiyo mpaka leo ipo. Kwetu kasa, shehe pamoja na Chuo Kikuu. Ukikuta kipengere cha haramu basi usi... utuambie vizuri. Tunamula mpaka lao. (kicheko) Unasikia? Halafu shamba la katani limekuja baadaye. Halafu Linda anataka kupanda katani, ardhi ya Ntwala. Na vitongoji vyake mpaka Ntepwesi, mpaka kule Likonde, mpaka Nchikongola yote, katani tupu, mpaka Madukanda, katani tupu. Lakini Waamerika, nadhani watu kama hao, elfu tisa mia arobaini na tano walikuja vijana kidogo kama Wanegros, na Waamerika fulani, kuja kupima. Kina, kina kile cha bahari ya Mtwara. Pima, mdomo wote, mfereji wote, moja kwa moja mpaka nje. Kuna majina yake kule. Kuna vipa vyake kule, kipa kile cha mwisho ni Ntwalo kutoka bandarini.

Pw XX M Kwa nani... na Maganga.

Pw AN M Na Maganga. Unasikia? Kupima wakapima, wakapima, wakapima, arobaini na tano, arobaini na sita, arobaini na saba... kupima tu. Na wakati ule Wazungu ni hadimu. Na halafu hawezi kukaa na hivi kama bwana mdogo tulivyokaa. Ni hadimu sana. Kumwona unakwenda mbio. Na unaacha vyako vyote. Huji pale.

Pw XX M Upwa kabisa.

Pw AN M Upwa kabisa. Lakini kulikuwa na ujanja wake, watu kama sisi, ee. Shauri hawajui elimu, ni ujanja wa macho tu. Unaonekana machoni mtu ujanja. Zamani ustaarabu ni ujanja tu. Na elimu imetokana na watu kutoka kichwani ku... na elimu. Haikuzuka hivihivi tu. Elimu haikuzuka hivihivi. Elimu imetoka katika matamshi ya watu, na mambo ya watu. Wakapima, wakapima, wakapima, wakapima, wakapima. Wakati wa Waingereza arobaini na saba, arobaini na nane, arobaini na tisa... arobaini na saba, arobaini na nane, arobaini na tisa, arobaini na nane na arobaini na sita hivi imekamilika bandari. Tukaambiwa sisi pale tutoke.

Pw AM9 M Tutoke, ee... kwa ajili gani? Pale pa Ntwala pale. Yote hii ni ardhi moja, lakini tutoke pale kwa ajili gati ikiishakamilika, na halafu huko juu ee, ufalme wa ukoloni tena, kutakaa watu wenye hadhi yao. Sisi tumewahi kukaa pale, Mzungu wa shamba tu, shipliman, Mzungu wa shamba tu. Tuko kijijini pale. Mzungu anatisha. Unalia, mama anachukua kitambaa na kuziba mdomo. Kauli yako isitoke, unapiga kelele bwana asisikie vile. Mmh? Wakasema, hapana, uhuru unasogea. Sasa hivi kiliopo... na kwa bahati mbaya ama nzuri... wale kupima ile bahari na nini ikasema, haiwezekani, hatuwezi kwenda nje ya watu. Lazima tuwachukue watu waliozaliwa Ntwala. Waifanye kazi pale ya kupima bahari na kukata koko na kufanya ka... kila kazi. Kazi hii ni matunda yao. Hata baadaye waanzie na wao, zuri hizi. Sisi tunarakai nyavu.

Ki DM M Unafanya nini?

Pw AM9 M Tunarakai, kushono matundu samaki sio wanaharibu.

Ki DM M Ndio.

Pw AM9 M Raka ile unadaris, hm? Unarakai. Tundu nyingine unafuatilia, unarakai. Na unasuka nyarfi, nyavu. Ikakatwa na samaki, unarakai. Na kwa maneno ya zamani unawanja. Sio uwanja huu wa wasige. Unawanja nyavu. Unawanja, eeh, unawanja, unatega madema. Papi la dema zuri. Tumbo lake lililokwenda kwake mbaya. Kivua kimeoza. Kile kinachombabaisha samaki kuingia ndani ya nani... ndani ya ndema, halafu hasugui alikoingilia. Ni kivua, kimeoza, unatengeneza kivua chengine, unarisha kama ki... kwake. Sasa dema, madema mengi, dema moja, madema mengi, manema, ndio lugha ya zamani. Malema, lilema moja, malema mengi. Lilema moja, malema mengi. Upondo mmoja, mipondo mingi. Kasi moja, makasi mengi. Kasia moja, makasia mengi.

Ki DM M Iko tofauti baina ya kasia na kafi?

Pw AM9 M Iko. Ndiyo. Kasia... lina fimbo ndefu. Kasia lina fimbo ndefu sana. Mmh? Unaona hii fimbo. Kasia kitu kama hichi. Halafu ni lefu. Na yako mengi. Kwenye dau au mashua. Yanaweza yakapachikwa, upande mmoja matatu, upande mmoja matatu. Vuta kasia wanaosema kule. Yanainuka kwa amri, chap, chap! Mnalala nyote pamoja. Chombo kinakwenda mbele. Kama kasi yenu ni ngumu zaidi ni kazi sana. Anakuambia, pinga maji, zuia. Pinga. Watu sio wanapingana katika maswala mbalimbali. Na yale maji unaweza kuyapinga chombo chako kikafunga bleki. Si vyombo vya moto, sio boti ile. Pinga maji, mnayatosa yote makasia yenu. Inavuti kinuvi. Haja ya kuangalia kina cha maji, kwa sababu ya kusimamisha wale watu. Hata kama kuna wimbwi, kuna rafu, kuna nini. Na kafi ni fupi.

Pw AM9 M Na anayevuta yuko nyuma mmoja. Na ikizidi sana watakuwa wawili. Lakini lazima akae nyuma huko. Na mmoja akae mbele. Ama zaidi, mtu wa kafi ni mmoja tu. Kwa mtumbwi mmoja mmoja, wa ntu mtu mmoja, watu wawili. Kwa hiyo kutolewa kwa katani na kupima bahari, kadhalika bati kupimwa na kuna

nini. Ikawa tena tumeambiwa sisi tufanye hiyo kazi. Lakini miji hii yote ni moja. Ni seti hapa, Mangoila, Ntwala, Ntwepesi, Msanga Mkuu, watu wa jinsi moja, tabia zao, mila zao na dasturi.

Ki TS M Watu hawa kutokana na maelezo yako inaelekea kwamba ni wa jadi toka sehemu mbalimbali. Ndivyo, sivyo? Kama ndivyo, wametokea pande zipi mpaka walipokusanyana katika hii miji ya leo mpaka mka... mkajiita na kuitwa Wamalaba?

Pw AM9 M Kwanza, sijui ndio... mwasemaje? Lakini sisi kiasili ni wa Mwamba, Wamakonde wa Mwamba, wa Mwambani, ee. Na mtu wa humu ukimwita Mmalaba kama anakuelewa wewe, hataki kukujibu kwa ustarabu wake kwa kweli. Lakini sisi ni Wamakonde wa Mwamba. Makonde hizi zina tabaka nyingi sana hizi. Ama si sawasawa?

Pw XX M Sawasawa.

Pw AM9 M Makonde zina... Lakini sote Wamakonde. Lakini Wamwamba, Mwambao, hii Mwambao sio imekuja sasa, kwa kutungana na umamba. Sisi watu wa Mwambani. Ni jitu ambayo kazi yetu sisi kulakula vitu vya baharini tu. Hakuna haramu haramu hii. Heh? (kicheko) Vitu vyote manyankumi manyankumi, masale, manini... kazi yetu ni kupondeapondea tu. Na ntu ukintoa kule, huyo Mmakonde kabisa, ukaja ukampa pesa, anakula sasa. Zamani angekimbia tu. Lakini sisi tunaochukua pesa, ameshajifinga. Unajua kujifinga? Ni kukusanya mawe. Akajiziba, anatoa pumzi tu. Ukamtoa mawe yote, yeye amekusanya. Ukantekenya, unamchukunua, akatoka. Akaingia mikononi, akaja na mikono hii, yake minane, akatia ndani ya pua. Bado unastarehe tu. Mwamba huyu. Bado anastarehe, hajapata matatizo yo yote. Anaona raha. Halafu kuna madudu humu ndani nma masumu yake. Kuna yule taa, umemwona kama taa, samaki. Kuna nyenga, mbaya sana, miguu yote sisi tuna alama zetu. Anakukita huko, huku anakwenda. Kuna nononduni, kanyata samaki kama huyu mbaya sana. Miezi sita wanakuuza. Zamani miaka miwili mitatu na nguu unapotea. Lakini unapona.

Pw XX M Safari bahari.

Pw AM9 M Kuhamishwa kwetu, wakoloni wakasema, kwanza tukaambiwa tukate... tukate koko, kapa hii, mangololo. Nini ile? Kapa hizi. Mikoko.

Ki DM M Ndio.

Pw AM9 M Mikoko. Iliziba sana. Watu wa Ntopesi na watu wa Ntwala tunakata mahala pamoja. Halafu ikawa ni kesi, kwa sababu kitu kimoja nkoloni, kama anataka kufanya kazi, anafanya kazi pale, amri tupu. Amri tupu. Fanyeni kazi, fanyeni kazi. Pale tunawawekea nyavu, tunakataa kufanya kazi. Hatukukwenda tukachukuliwa shule. Na huyu bwana niliyekuwa naye mimi na nini... kwenda kule. Kwenda kule hawa mahala tulipokaa usiku wakanichagua mimi kama ndio mzungumzi wao. Kwenda kule juu. Kwenda kule juu nikazungumza kijana mmoja wa Kimarekani. Hajui Kiswahili. Hajui Kiswahili. Na mimi najua Kiswahili kama ninavyosema. Lakini wakati ule ilikuwa kazi za kujitolea zipo vilevile nkoloni. Tumewahi kulima barabara, kwa kodi, ama kwa hivihivi tu. Kwa mazingira ya leo wanakuja DC na nini ukasafishe.

Pw AM9 M Imetoka zamani. Kilichofanyika siku ile, mvuvi kum... unaona sasa hivi, maana yake mamba atafanya kazi yo yote. Ataingia katika uinjania baada ya kusoma. Lakini amari yetu ya zamani ni ku... kila utakachokifanya cha juu ni cha bara tu, na anafanya ntu ya bara. Hata kule kutumwa kwenu ninyi. Mimi nimechopoka kidogo, si siku nyingi kufanyafanya kazi tu za nini.

SIDE B

Ki TS M Kazi kubwa ya wavuvi?

Pw AM9 M Kazi kubwa ni wavuvi tu, wa Makonde. Hilo lisitoke. Lakini wa Mwamba, wa Mwambao.

Ki TS M Ebu nieleze kidogo lile neno la Malaba mmepata wapi? Na kwa nini linaudhi katika masikio yao?

Pw AM9 M A-aa, lisichukuliwe kama maudhi, maana Wamalaba tupo hapa wengi. Lifutwe hilo. Lakini mimi nilikuwa ninaeleza tu.

Ki TS M Naam.

Pw AM9 M Kwamba zile kanda namna ziwe kama maake sasa hivi sisi sote ni Wamalaba. Ukiwaambia watu kama kipengele hicho... itaudhi watu wengi sana. Sisi sote ni Wamalaba, sote sisi ni Wamalaba. Lakini kwa mgawanyo wa zamani hawa wazee, ukishatokea huku, anakuambia, unatoka... unatoka pahala, unatoka Malaba. Maana Malaba haikuwa mbali, hapa pwani. Mulipe. Mpaka na Nyamba tu. Sansubansu wakati ule ni mbaya sana. Wanakuuliza, 'Uma kwachi wepo?' Sasa yule naye Kimakonde chake ni tofauti na wewe. Wewe unasema, 'Uma kwachi' kwa lugha ya hii nyepesi ya hapa. Wale kule unasema una... ni 'uma kuna ni', anatoka wapi. Anatoka na Nyamba. Kwa hiyo kwa Makonde kabila kubwa sana sisi sote ni Wamakonde. Lakini kwa mgawanyo wa maisha ni Wamakonde lakini Wamwamba, wa Mwambao.

Ki TS M Je, una mchango wo wote kuhusu neno Chuno, maana yake katika kilugha? Maana gani?

Pw AM9 M Mchango wa Chuno...?

Ki TS M Neno lenyewe, maana yake.

Pw AM9 M Neno lenyewe maana yake Chuno ni kwa kweli ni ile miti. Mimi nakumbuka hilo jambo. Kwa sababu wao wamezunguka, wamekuta ile, miti ile, michu, ya michu, michu, michu. Mpaka sasa ipo ile miti katika miti michu. Michuno, michu ile. Ile kwa wale wa zamani, kabla za ndoa wamashangazi zetu hao walikuwa wana... wanavumbikwa... hawaonani na wanaume. Halafu wanachukua ule mchu ule, unakatwa, unasaga. Anasafisha siku zote, anakuwa mweupe tu. Mpaka siku ya kufanya harusi, ndio anafungua uso wake. Anaona macho, lakini yote nini kutafuta ndio poda za wakati ule. Anakuja pale mama mwari, amependeza, amechubuka. Mashavu kama embe dodo. Siku hii anakabidhiwa kwa mumewe. Ile michu, michu, michu. Halafu miti hii ya michu unaweza kufanya kipini cha jembe, vipini vya mashoka, vya kuchongea ngalawa, chongea vitanda, hiyo michi.

Ki TS M Sasa twende kwenye kipengele kingine cha desturi na tabia, ambazo hapa mjini mnazo, pengine hazipo sehemu nyingine. Maisha yenu mnayaendeshaendesha vipi?

Pw AM9 M Main... Maisha yetu sisi toka zamani ya ujamaa sana. Toka zamani maisha ya watu wa mwambao ni ya ujamaa mno. Kwanza dasturi zetu ndio wazee hatutoki nje. Ila sasa tunaasi. Sasa unasikia ntu amekwenda wapi huko, Moshi. Watoto wetu sisi.

Pw MA M Nilitaka kuomba radhi, kwa sababu mimi nina shughuli kule Nchiwa na mambo yote ninayo nina... Sasa wale kule kwenye taim zao ni saa tisa. Sasa ikiwa mimi nitakuwepo hapa, kule wengi watanisubiri kunitafuta. Na hili jambo, ambalo nilikuwa mimi ni... tu, sikulielewa. Kwa hivyo...

Pw XX M Tumsamehe mzee, maana yake yeye anatutangulia tu. Ndio hayo tunayosema hapahapa.

Pw MA M Au kama kuna maelezo mengine naweza kueleza nikapata kuondoka. Historia yangu mimi ni kuondoka hapa mpaka kwenda Unguja.

Ki TS M Naam, dokeza tu kidogo.

Pw MA M Mimi jina langu Masusi bin Ali. Na sababu mimi nimezaliwa wakati vita vya Mjerumani na Mwingereza. Ndipo nilipozaliwa. Na vimemalizika vita na fahamu yangu ya kuweza kufanya kazi nikapata hela ya jermani.

Ki TS M Naam.

Pw MA M Halafu baba yangu alinitia chuoni kusoma. Yule anonisomesha ni shemeji yake. Sasa nyumba ya vivi yangu, yaani kwa kizamani vivi, vivi anaitwa vivi, yule aliyemzaa mama au baba, unamwita vivi.

Ki TS M Naam.

Pw MA M Unasikia? Sasa mimi pale chuoni nyumba ya vivi yangu hii na chuo. Sasa mwalimu yule akitoa ukali wakati wananisomesha, anakuja vivi yangu yule, kuja kuniondoa pale chuoni. Baba yangu ikawa ameshangaa. Hawezi kugombana na mama yake kwa sababu yangu mimi. Akaja akatoa malalamiko kwa shemeji zake, kwa jomba zangu mimi. Kuwa huyu mtoto nataka kumsomesha, lakini mapenzi ya bibi yake hasomi huyu. Nifanyeje? Wale shemji zake wakanijibu, kwa kuwa huyo mtoto. Ukitupa sisi naweza kumchukua tu kampeleka sehemu nyingine. Baba akawapa ruhusa, 'Mchukueni'. Nikachukuliwa mimi. Wakti huu nilipoondoka hapa kwenda Unguja inatumika hela ileile ya Jerumani kabla Mwingereza hajaleta zake. Nikatoka mimi hapa nikapakiwa ndani ya jahazi hizi za mbao hizi. Yaluwali mmoja zamani akiitwa Nammeta. Nikapakiwa hapa nikapelekwa Unguja. Sasa nilipofika Unguja nimekikuta Kiswahili kilekile cha Kiunguja. Kitu... mchele-mchele, sukari-sukari, chumvi-chumvi, yaani kilekile. Sasa kati ya matembezi, nikikaa pale ninapoishi, nikienda shamba, ninakuta lugha nyingine. Unasikia? Pale ninapoishi, yaani mimi najua huyu ni mtoto. Anaitwa mtoto. Sasa nikienda shamba kule, yuleyule mtoto nitakuta jina jingine, anaitwa mwanakele. Kwa lugha ya kule, ya mashamba kule.

Ki TS M Naam.

Ki DM M Hukohuko?

Pw MA M Kulekule Unguja. Mwanakele ni mtoto mdogo.

Ki TS M Naam.

Pw MA M Lakini pale nilipofikia mimi ninajua ni mtoto tu. Ehee, basi ikawa lugha zile nilizosisikia kule ninazozifahamu, ni kawaida kama wanavyosema watu Unguja, unasikia. Bin fulani, bin fulani au hivi. Yale najua, isipokuwa ya nje. Ninapoondoka petu kama kuondoka hapa nikienda Nanyamba utakuta lugha nyingine.

Ki TS M Naam.

Pw MA M Ehee. Lakini kwa pale nilipokulia nimekulia kikiswahili tu, cha kawaida kama Unguja.

Ki TS M Ulikulia Unguja mjini?

Pw MA M Nimekulia Unguja Chukwani.

Ki TS M Chukwani.

Pw MA M Eee.

Ki TS M Ewallah, ewallah.

Pw MA M Basi, sina namna nyingine, isipokuwa nilipotoka Unguja nimefika kabla Saidi Halifi hajatawala. Yuko Said Ali bin Hamudi. Unasikia? Amejihudhuru, mimi niko Unguja, mimi nimehudhuru kwa Ulaya. Kuja kutawala ndugu yake. Unasikia? Sasa yule ndugu yake ni mke wa Saidi Halifa. Ikawa baada ya kuwa yule

mwanamke hawezi kutawala, ndio ule utawala kupewa Saidi... Saidi... Saidi Halifa. Lakini utawala ulikuwa Bi Matuka, binti Albin Mahmud. Mnasikia?

Ki TS M Na umerudi mwaka gani?

Pw MA M Mimi nimerudi zamani sasa kuliko miaka ishirini inapata tangu kurudi.

Ki TS M Uliwahi kuo kule?

Pw MA M Nimewahi kuo Dar-es-Salaam. Unguja sikuo, lakini nimewahi kuo Dar-es-Salama, katika matembezi yangu ya kikazi tena. Baada ya kufika hapa, halafu ikawa tena Unguja. Dar-es-Salama nimeishi kwa matembezi ya kikazi. Nimeishi Tanga kwa matembezi ya kikazi. Nimeishi Pemba ya Unguja kwa maisha... kwa matembezi ya kikazi. Nimeishi Mombasa kwa matembezi ya kikazi. Lakini wakati huo mahistakwimu yangu ilikuwa pale Dar-es-Salaam.

Ki TS M Asante, ewallah, nashukuru, marehemu.

Pw AM9 M Ninachoamini ni kwamba ndoa zetu za kizamani... hasa Kimwambao. Kwanza sisi kwa jadi mwananke kwetu sisi ni kitu ashaf sana. Nke, nke, ni asilmali kubwa hiyo hata kwa matangazo tunaweza tukasema. Ni kitu kikubwa kwa heshima yetu sisi mwananke. Kuliko mali yako, kuliko nini. Maana yake ni chimbuko la kuweza kupata wajukuu na watu. Njia kuu ya kupitia ni hiyo. Unawezaje kuondoa hizo, hata mimi nimeziwai. Hazipatikani ninyi wenyewe kwanza, msichana na mvulana. Humwoni. Humwoni kwa namna yo yote. Isipokuwa wakati wa mavuno. Unachokoa kumbwa. Msichana... msichana anachokoa kumbwa, na pweza, na ngisyu na kadhalika. Kuna vitu ashaf sana. Makome yale yanachanganywa na unga wa... wa... wa... wa matambo. Unanyunyiza. Hujawahi kula katika hoteli yo yote? Kitu cha namna hii. Mawazo yako ya fahamu yote yanaharibika. Unawekewa pale chumba (kicheko). Unawekewa kando, yamelala mle kama mjongoo. Yamenyunyuso ule unga. Chota kidogo.

Ki TS M Halafu kutupa na kuangusha.

Pw AM9 M Halafu kutupa na kuangusha. Sasa hii, wewe unaanza kusema kwamba mimi nataka kumchumba huyu. Kazi inayofanyika pale ni ya usomo tu, kama kuna shangazi. Mawasiliano. Hamwonani. Mawasiliano, shangazi anapita huko na huko. Huyu bwana anakwenda. Huyu bwana anakwenda mpaka unafika wakati wa ndakika. Eeh, wewe umeishaiva kidogo. Wanasema Kiswahili cha Tanga, mdakik... wakati wa mdakika. Kwa kufikia jambo lile la wakati wake. Sasa wazee wanakwenda kwa mzee mwingine, kwa mzee fulani mwingine, kumtaka binti... kumtakia binti kwa mtoto wao, hasa wa kiume, anakwenda kumpata mzee wake, anazungumza. Ndoa itaanzia pale. Sherehe zake za harusi kutokana na pale. Jambo la kwanza kabisa anawekwa mfungati. Maana Kiswahili cha zamani hicho. Mfungati kwa sasa ni nini? Mfungati... anaka mfungati, si kuzabaa.

Ki TS M Sasa hifi mfungati inarahisisha.

Pw AM9 M Mfungati? Mfu bwana. Kama uweke mfu nani ataelewa? Na ndio maana Kiswahili chengine sehemu zingine zimeharibika sana. Haitoi maana. Mfu, umefungwa pale. Nataka nipanue zaidi. Umefungwa pale. Si kama umefungwa jela. Umefungwa katika mapenzi. Wewe unataka ukae pale siku saba. Wakwezo wanakuweka. Hapana kutoka ndani. Pweza inaliwa ndani humuhumu. Makome yanatafunwa ndani humo. Huna ruhusa kutoka ndani. Na yule binti katika umri wake kwanza ndoa zilikuwa za, labda kipengele hicho. Lazima kijana akomae. Sio sasa hivi. Watoto wanazaa, sababu hata wao wenyewe hawawezi kusaidia. Wanapigwa visu tu. Kwa sababu watoto wadogo. Ndio mazazi ya majila. Unapata nafasi tena. Unakabidhiwa nke. Unakula starehe. Unakula ndani. Sasa changu analiwa kule, changu wa kubanika, changu wa kupaka. Mchuzi wa rojorojo, mchuzi wa... wa... wa ukwani tu. Wali unatiwa nazi, mchuzi

chukuchuku. Ukisalti kukusanya mahala pamoja mawazo yako yote hayapo pale. Wali wa nini ashaf huo? Sio mchele, ni ntama tu.

Pw AM9 M Ntama tu. Ntama, were, mahindi al ghasi. Ni wali mwepesi, lakini mahindi... siku nyingine unataka mahindi. Inapikwa mikate mle ndani kwa bwana arusi ya mofa. Kuna mofa waachana na kitumbua. Yungu kubwa hivi, yungu kubwa la udongo, wanafanya slesi ya mikate, iliyotwangwa na mitama. Kama thelathini, arobaini, hamsini. Unabandika ndani ya vyambasa, unabandika, unakoka moto. Ndio hii imatenga sasa hii. Anakwenda kutanudi, anakwenda kwa nini? Ee. Imetoka zamani. Ndio asili ya mikate ikaja hiyo. Bahati nzuri imetokana na mofu. Ile inabanduliwa moyo. Upande mmoja umeiva sana, hasa kule unakokaa kwenye udongo. Utapenda, maana yake kule kidogo kuna harufu ya udongoudongo ule. Inapatana na ile, ndio unabandua ile, unatiwa na sahani, unapelekewa kule. Changu yuko pale, wa kuchemsha, wa kulegeza, na pamoja unakula. Unakula na nini? Uji. Uji wa asubuhi ama uji wa mapande? Uji wa mapande asili yake nini? Ni mchele wa mpunga. Mpunga gani? Mpunga wa vilimani. Ngwindimba, jina langu ni ... sasa. Andika hii. Jina la ngwindimba alipo.

Ki TS M Maana yake ndio mchele, sio?

Pw AM9 M Ni mchele, lakini mchele ule wa vilimani. Ndio huo sasa. Na tena unakwenda katika mitumbua.

Ki TS M Milimani, yaani unalima milimani?

Pw MA M Hawalimi bondeni. Huu ni speshel. Zamani wazee kupata uji katika vitumbua na uji wa mapande. Umenyooka vilevile kama ulivyo, katika uji wa mapande. Punje tatu tu umeshashiba, pamoja na huu. Mtu anaanza kunenepa toka vidole mpaka kichwa. Sasa ntu ananepa... Nitaharibu hii?

Ki TS M Hapana.

Ki DM M Hapana.

Pw MA M Sasa ntu ananepa kitumbo, kwa ajili ya mambo fulanifulani. Siwezi nikaeleza, ee, kama yule mtoto. Na watu wana afya nzuri tu. Afya nzuri tu. Hio ndio inafanyika. Halafu anakwenda baba nzazi ama mama na mashangazi zake, anakwenda. Lazima ahakikishe kwamba upwawa upo kumhamisha huyo mama kumpeleka kwa mumewe. Upwawa. Mwiko upo. Kisu cha kusaranga. Wewe unasema 'kuchonga' au kufanya... kusaranga miyai, miyai, kusaranga, kusaranga, si inatoka mikeke hii. Kule kunaitwa kusaranga. Na ina maana tu, sar, sar, unasaranga.

Ki DM M Mmm.

Pw MA M Kipo. Halafu je, mkeka upo? Mkeka ni ashaf sana. Hawezi kwenda bibi arusi kama hana nkeka. Kiwambaza kile pale, shuka itawekwa wapi? Lazima shuka ipachikwe pale kwenye chango. Kuna miti chango. Hakuna besela huko. Chango, jiti moja bao kubwa. Imewekwa vijiti, vijiti, vijiti. Unapachika, visokoti, kanzu. Unasikia, bwana njoo, unapache... Halafu unajua kama kweli nyumba hii ina bwana arusi na bibi arusi. Mkeka, kuna mkeka wa kulia chakula chini. Na kuna nkeka vilevile hule, na mkeka mwingine, wa malasi.

Ki DM M Namna tofauti?

Pw MA M Namna tofauti. Unawiza. Wiza ni rangi ya ile, mkeka... Ee, halafu kuna kama darizi vile. Kuna vyungu nene, ee, nyepesi. Na wao unawiza, unaita mkeka. Halafu hawashoni tu. Wanashona na wao kama watu wa dars. Ana kibao cha kusugua katika laini ile. Ili zile balabala zilane, isije bwana akapata taabu tena, analala, mgongoni kumegondania. Kuna alama kwamba alilala kwenye nkeka. Si ruksa ... za zamani. Hiyo ndoa inakwenda. Mnakwenda sasa hivi, mnaanza kutunga riziki huko ndani kwenu. Unapigwa maswali kila mahali. Watu wanaishi kwa namna gani? Mwulizeni. Unafanyaje? Na ndoa zetu hakuna kupotea, sasa

inapotea. Huyu ni ntoto wa binamu yangu mimi. Ameoa hapohapo. Mimi nimeoa hapohapo. Nyumba kuzunguka tu. Hutoki nje. Sasa mimi niliozaa mimi sina hapo watanichukua. Wengine wako huko Arusha, wanaoa pale. Ya zamani hakuna, sisi tu. Sasa sisi ndio wa mwisho. Mimi na ndugu zangu pale.

Pw MA M Hutoki. Maana yake nini? Ujamaa umeanza zamani sana. Leo kuna msiba pale. Watu wote hakuna ruksa ya kwenda mahali po pote, ni pale. Siku tatu mzima mnakula pale. Siku za neema, vitu vyote mnakula pale. Wavuvi wote wanaleta samaki, hapana hapo hasala. Hakuna neno hasala mbona mnapeleka, mnapeleka pale? Kama kuna unyago, siku saba mnangurumana mnakula vyakula tu. Sasa cha kufanyia hatuna, lakini nia iko palepale. Tutafanya nini na nini? Ni mila na desturi. Ndio tunapunguzapunguza. Kwa hiyo unaangaliwa hata kisasi chako. Unapopata ntoto wa kwanza, na kule shangazi yake mkewe anamhoji. Unaishije na mwanamume? Na anaangalia. Kama mwanamume anamwona mbaya mbaya mwanaume ni ntunzi. Sasa thubutu, mwanamume yule ntunzi anakushinda tu. Na wewe uko. Unaambiwa na mjomba wako. Ni ntoto wa watu, mtizame vizuri. Hakukuona jambo lo lote ni kaniki pande mbili tu. Hm? Zile kaniki pande mbili tu.

Pw MA M Ziwepo. Zile pande mbili kwa pamoja inaitwa nini...? (kicheko). Pande mbili tu. Nakwenda, nakwenda mpaka unapata ntoto wa kwanza, ntoto wa kwanza, basi. Pale ndipo ilipokuja sisi kuona kwamba Wamakonde, Wamwambao, mila na desturi. Kwamba kwa vyo vyote vile ameshazaa nkewe amejifungua. Utawekwa miaka mitatu. Humwoni nkeo. Na nke ataambiwa: aoge maji, lakini awe mbaya sana, asipendezwe kwa mumewe. Maana yake iko hatari.

Ki DM M Upangaji wa majira ule.

Pw MA M Upangaji wa majira ule sasa. Wanachotaka nini watu wale wa zamani mpaka tumezaliwa sisi? Mwanja ule, mama ntu, afanye kazi, apate pumu. Awe na afya. Sio unabandika hapa kichwani mmoja, huku mwingine yuko, mwingine yuko pembeni, mwingine yuko vichochoroni huko. (kicheko) Huwezi. Huwezi kuzalisha. Anataka nguvu. Mimi mwenyewe binafsi, maana yake mimi nilikuwa si mbaharia baharia tu, seamen tu. Ee? Kijana wangu wa kwanza hawa hawa wanikabidhia. Kijana wangu wa kwanza kabisa. Na yuko hapo Dar-es-Salaam. Kijana wangu wa kwanza kabisa. Niliambiwa kwamba unaweza kufanya mambo mawili. Kaa hapa na adhabu zako. Ama ukishindwa, safiri. Minka ikatokea. Miaka inasogea mimi narudi. Kuja kuzalisha mali tena. Ikiwa hivyo, mimi napeni. Na wale waliokuwa wanasikia wenzangu wanaambiwa, hapana. Miaka mitatu, miaka miwili na nusu hasa. Mitatu ntoto ananyonyeshwa kabisa, ananyonyeshwa na maziwa ya mama yake. Kitu cha kwanza hicho.

Pw MA M Hata homa zilikuwa zinapungua kwa watoto. Hata magonjwa madogomadogo ilikuwa hakuna. Hm? Maziwa ya mama. Miaka miwili mitatu ilitimia tayari, halafu tena, basi, unaambiwa. Haya, kama uko wapi, urudi. Sasa umekaa mabaharia, rudi, mimi ninarudi. Unakuja kuzalisha tena. Hivyo tu. Nini? Ntoto anatofautiana, yule wa kwanza na wa pili wanatofautiana sana. Anasaidia mtoto mwenziwe pale. Mama anakwenda shamba na kwenda kutanda dagaa huko. Wanaitana huko, chimelelo huko. Wanaitana, 'lichelemelelo'. Lichemelelo, yaani kuita, 'twende'. Kuna jiwe moja pale pwani linaitwa Lichemelelo. Kuchema. Unawachema wenzio. Wako mbali. Lakini pale ndio senta ya kukutana. Panaitwa Lichemelelo.

Pw MA M Kwa hiyo ndugu wakienda vile wakati ule. Kwa sasa hivi kama zilivyo sitakueleza, ninyi wenyewe mnazo. Mnazijua zilivyo. Halafu, nataka kumalizia. Ujamaa umeanza siku nyingi. Kwa namna gani? Wavuvi, kazi yao ni mafungu. Kwanza kila dao na kila ngalawa na kila ntumbwi. Kazi yao, bia. Wanavua, bia. Shirika, bia, wanagawana mafungu, bia. Na wanaonza kuwapa wazee wasiojimudu, kwa ridha yao wenyewe. Pelekeni nzee fulani, pelekeni nzee fulani, lakini bia.

Ki DM M Mpaka leo hii.

Pw MA M Imepotea, imepotea. Haipo. Wakati ngumu. Bia, halafu wanavua, wanavua, sisi tumewahi, na mzee wangu hapa amewahi. Wanavua kwa kuwa pamoja. Wanavua tu, wanavua tu kama wanakwenda wapi, wanavua, mpaka mwisho wa uvuvi wao wanakutana tena, wanajua nini walichopata. Wanapanga gharama, wanapanga zana, wanapanga nyuzi za kurakai, wanapanga kununua mitego mingine, hivi. Hata kwa amana, kwa sababu mzee mmoja anachaguliwa kama huyu ni mzee wa kijiji. Lazima ajulikane ana amana pale. Lazima awe angalau shilingi thelathini. Elfu tisa mia thelathini na nane shilingi thelathini ni nyingi. Ni baisikeli, nimenunua kwa shilingi thelathini. Mimi nimeona machoni. Shilingi thelathini. Ope, na jina lake. Nimenunua baisikeli, shilingi thelathini. Awe na shilingi thelathini. Kinachofanyika ni nzee mwenye nguvu, inachukuliwa amana kwake. Kununua sanda ya makafani. Gharama zikiisha, mkishachanga, mnarudisha haki yake. Hakuna kusimulia.

Pw MA M Simulizi, kumsimulia kwamba tazama alivyokuja kughorofa, hapana. Anatoa kwa itikadi safi. Anatoa kwa moyo mzuri, anatoa kama ndukuzi. Kwa hiyo, mimi nimesema mengi, na bibi amekuja hapa, lakini namna yenyewe ndio hio. Mnagawana yale mafungu, mnasema kwamba tumegawana safi. Nimefanya mahesabu yenu, safi. Kitu safi ni kitu ambacho hakina mwishki. Wewe fungu lako hili, safi, unamwambia. Kwa sababu ni kizuri. Na fungu lako hili safi. Kama kuna samaki pale ghafya ghafya, ambao hawana vichwa wana nini, ee, mnakusanya nkauza kwa bei ile ya kulipua mara moja. Imetokana na mali gani? Safi. Sasa mimi nadhani nilifikia hapo. Halafu walikuwa wanasema, 'Mali isiyo na daftari inaghibu bila habari'. Hakukuwa na msomi. Nimu yao imefungwa tu. Mmepata shilingi tatu leo. Basi zitafungwafungwa tatu. Mzee anaweka. Mpaka mmemaliza majimana, majimana. Sio bamvua, maji yamekufa. Hayavuti, tait. Majimana. Maji chalu, maji yanaanza kuvuta chalu.

Pw MA M Maji bamvua ni taiti kabisa. Mlangoni hapa pana vipande vya, vya miti hii ya mtama, selewa zile, zinazotokana na mtama zile. Saizi hii vimefungwa vipandethelathini, viko pale. Kila kukicha, anavuta, mwezi huu. Anasema leo mwezi mosi. Na akili yake iko pale tu. Hata mama atavuta pale ya pakia pale. Ikifika mwezi thelathini anajua mwezi thelathini. Kama ni mpungufu anajua ni mwezi thelathini mpungufu. Iko pale. Hakuna mwenye saa nkono, kwamba anatazama wakati... Ni jua tu. Vukuti tayari, na itakuwa vukuti tayari vilevile. Kwa hiyo baadaye vitu hivi vimekuja, vikaja vinaletwa huku. Watu wanachonga vitanda pale ka-ka-ka. Mtu anapita. Unakwenda wapi huku anachonga kitanda. Ndio barua yenyewe. Wakienda Mikindani mwambie mzee Azani, huku kumepata faradhi kama hio. Hawana habari kumpita faradhi. Barua inakwenda, lakini kwa imani. Atakwenda kubali hata kama ana kazi gani, mpaka akatoe maagizo yale. Maana ndio barua yenyewe.

Pw MA M Maagizo mkuja? Ndio. Sasa barua zinaweza wakati mwingine. Sasa mimi nimesema sana. Bibi amekuja hapa. Na yetu ameleta na, au walikuwa wanacheza mabega, ngoma za kiasili... kede-kede-kede, kiasili na nini, na mengi. Hao ndio waliotuzaa. Kama ana moja mawili, na yeye ameshajua hali hii.

Proofread by MP

Edited by TR in October, 1996

DAHE 106

Place: Mtwara, Mikindani

Time: 13.10.1990

Interviewee(s): 1. (HB1), 2. (SH2), 3. (MC1), 4. (AY1), 5. (YS), 6. (RA2), 7. (MK2), 8. Unknown (XX), 9. Several unknown (X1)

Interviewer(s): 1. Arvi Hurskainen (AH), 2. David Massamba (DM), 3. T. Sengo (TS)

Recorder: Sony Professional

Language: Standard Swahili (Ki), Kimakonde (Ma)

Topic: 1. Tradition and habits of the people in Makonde, 2. Slavery, 3. The origin of the people in Makonde, 4. Circumcision rites, 5. Getting married in the past and today, 6. Sexual moral, 7. Story about a rabbit and a turtle, 8. Story about a Sultan, 9. Story about a lion and a rabbit, 10. Story about Tipitii and a lion

Ma HB1 M Nisimulie mpaka saa 12 hapa?

Ma XX M Usiseme peke yako mpaka hapa.

Ki AH M Ongeza tena jina lako.

Ma HB1 M Mimi Hamis Bakari, ni mwenyeji wa hapa Mikindani, Magengeni. Sasa nakuja katika historia ya mashamba. Historia ya mashamba yote mnayoona ya... ya minazi.

Ki DM M Naomba mzee kidogo, kabla hujaendelea, kukurejesha nyuma kidogo. Yaani jibu swali langu la maana ya Mikindani.

Ma HB1 M Ee, ndio, kweli nilisahau. Ewallah. Hapo nilikwama mimi hapo. Maana ya Mikindani hii kuita Mikindani ni naji yale. Kama nilivyozungumza kwamba pale maji ilikuwa hayafiki. Yalikuwa huko nje. Watu walitoka huko kwenda kuchokoa kumbwa. Kumbwa umezikua?

Ki DM M Hapana.

Ma HB1 M Chakula, kitoweo. Kwenda hukoo... Miambani, Mwambani, unaitwa Mwambani kule nje, kufuata maji. Sasa kubomoka lile jiwe lile pale na mvua imenyeshwa, ndio maji sasa yale yamekuja huku ya mvua mengi kabisa. Ndio sasa maji yakijaa, yanakuja, yanakuja, na miaka inakwenda. Mpaka sasa bahari ime... imekuwa mengi zaidi. Sasa ndio kuita maan... maana ya Mikindani. Sasa kwa maana hiyo kuita Mikindani yote jumla. Lakini kila sehemu na jina lake. Hapa tun... panaitwa Kimbuli. Kimbuli, Mmakonde mmoja kutoka bala anaitwa Kimbuli, kutoka bala Mmakonde huyu akiitwa Kimbuli, jina lake. Ndio kujenga kulekule alikojenga, alikofikia Livingstone, kule. Yeye akaitwa Kimbuli. Mmakonde huyo, ndio kuitwa Kimbuli.

Ma XX M Sio Chimbuli?

Ma HB1 M Chimbuli.

Ma X1 M Chimbuli.

Ma HB1 M Sasa historia ya mashamba haya yote mnayoyaona, watu wamegawanagawana sasa. Zamani alikuwa na mtu mmoja akawa na mashamba kumi na mbili ya minazi. Sasa katika kufa ntu yule midhamumijaa.

Ki TS M Akiitwa nani huyu?

Ma HB1 M Akiitwa Shikololo.

Ma X1 M A-a, a-a.

Ma XX M Penye minazi mingi Abdalla Rashidi.

Ma HB1 M Aa, Abdalla Rashidi kwa upande huu. Lakini kwa sehemu hii mpaka kufikia Mbuo, Ndumbwe, yeye akiitwa Chikolo kwa sababu alikuwa na mashamba 12. Kuanzia Mchuchu moja kwa moja na kuendelea mpaka Ndumbwe, ntu mmoja tu, mashamba 12. Na maji baridi haya tunayokunywa sisi hapa Mikindani, maji baridi. Yanatoka katika chini, yaani yamechimbuka chini. Ilikuwa ikatoka kidogokidogo, kidogokidogo. Hata tulipojitawala sisi, watu wakayafuma maji hayo. Ndio kujenga mashine kuvuta maji hayo. Sasa wataalamu ndio wamejenga mashine kabisa ya kuvuta mpaka wametoboa chini ya bahari. Na maji haya yanatokatoka zamani. Yanatoka chini, lakini juu ya mlima. Lakini haya maji yanatoka chini. Yanaitwa chemchem, mchushwa hapo.

Ma SH2 M Mimi Saidi Hamisi, mkazi wa Mikindani, Kisungule.

Ki TS M Sauti, sauti, sauti kubwa kidogo.

Ma SH2 M Mimi Saidi Hamisi, mkazi wa Mikindani, Kisungule. Narudi pale katika utumwa. Hii habari ya kununuliwa watumwa, walikuwa watu wa kabila mbili, au tatu, Ngoni, Mnyao, Mwera. Mmakonde hakuna aliyonunuliwa utumwa.

Ki DM M Kwa nini?

Ma SH2 M Wala Mwela. Ilikuwa hawataki kabisa kitu hicho.

Ki DM M Yaani wao wenyewe walikuwa hawataki, au Waarabu hawataki?

Ma SH2 M Wamakonde wenyewe ilikuwa hawataki kitu hicho cha kununuliwa. Na Mwera vilevile. Kabila ya utumwa ni Ngoni, Nyao, Mwela. Basi, Makonde hakuna ntumwa. Wala Mwela hakuna ntumwa. Nhyao, Ngoni, Makua, Bazao.

Ki DM M Ebu kidogo. Sasa Wamwera umetaja mara mbili. Kwa hiyo ni Makonde... ni Ngoni, Mnyao, na Mmakua.

Ma SH2 M Mwera hakununuliwa. Wale Mmakonde hakununuliwa. Kabisa, utatembea sehemu hizi zote huku, hukuti mahala... anaambiwa huyu ni Mmakonde mtupu, hamna.

Ma MM M Nikitaka kutoa historia ya...

Ki TS M Unaongezea hapo au?

Ma MM M Naongezea hapa.

Ma XX M Sio inakwenda huko sasa?

Ma MC1 M Mimi Dadi Mohammedi Chihinde. Yaani ni mwenyekiti wa Mitengo wa CCM. Mimi ninarudi katika sehemu ya Umakonde katika utumwa. Kwa kweli mimi nilikuwa ananieleza mjomba kama mimi Mmakonde. Mimi ni Mmakonde wa sehemu moja inaitwa Nanyanga, iliyo inakwenda Newala.

Ki DM M Inaitwa nini tena?

Ma MC1 M Nanyanga, ile inayokwenda Newala. Sisi ni... kabila letu ni Wamihiulu, lakini ni Mmakonde. Ilikuwa inanieleza kwamba Mmakonde hakuweza kupata utumwa, kwa sababu Mmakonde hakuwa na mwenye. Yaani sehemu za Ngoni ilikuwa na mwenye. Sehemu za Nhyao ilikuwa na mwenye. Sehemu za Makua ilikuwa na mwenye. Sasa wale mwenye, anapofanya ekstent, au kukaa tu akakusanya watu wake, basi akawakusanya watu 10, 15, wasema wachukue hao, wapeleke Mikindani, ukawauze. Na walikuwa wakikubali, kwa sababu ni mwenye. Akitoa amri ametoa. Harudishiwi na mtu mwingine tena. Lakini sisi Wamakonde hakuna hata mmoja aliyeweza kufanya hivyo, kwa sababu hatukutaka kutawaliwa na mtu mmoja. Ilikuwa sisi tumejiweka tu namna ya kipeke yetu.

Ma MC1 M Sasa ndio asili kuwa utamkuta mwingine anajihesabu hapa kusema kwamba mimi Mwarabu. Lakini ana kosa hilo. Mama yake amekuja Mwarabu hapa akannunua, akamfanya sulia. Akazaliwa ntoto. Sasa yule mtoto anajihesabu, kwamba mimi baba Mwarabu. Lakini kwa upande wa mama kuna kasoro. Kwa sababu Waarabu wakati tumetoka kule wamekuja bila mwananke hapa. Hawakuja na wanawake. Wamekuja wao na wanaume wao tu. Ufuasa wanawake wataowakuta huku. Historia ilikuwa inaniambia mjomba. Basi ikabidi wanawanunua na wengine wanawapeleka mbali. Wanewa wanaopendezapendeza kidogo, basi wanawaingilia, wanaofanya, kutokea ntoto mle ndani. Ndio Waarabu Newa una hapa, Mikindani nzima hii. Historia yao imekaa hivyo. Mwingine utansikia, huyu Mwarabu. Lakini baba Mhyao. Mwarabu huyu ilikuwakuwaje amepata mwananke Nhyao? Ndio sababu. Lakini huwezi kumwona Mmakonde. Kwa hivi narudishia kwamba kisa cha Mmakonde asipatikanake na utumwa, sababu zenyewe ndio hizo. Nilizopata historia kidogo kwa mjomba wangu, mzazi wa...

Ki TS M Sasa nikudokezeni kidogo wenzenu walivyotuambia pahala pengine. Halafu tuliache, maana tumelipata kwa faida. Mmakonde katika kujiletea kwamba asichukuliwe utumwa, aah... walivyotueleza wazee wenzenu wa Mtwara njini. Ndio kisa au ndio sababu ya ndonya na machale yale. Ulikuwa ule ni utetezi wa kumtisha Mwarabu asimtamani mwanamke wa Kimakonde na wala asimtamani kijana wa Kimakonde. Sasa sijui kama ninyi hapa mmeipata hiyo au vipi?

Ma PM M Mimi ninavyofikili, sio kosa hilo. Kosa kubw... Kwa sababu huyo Nhyao ilikuwa na yeye ilikuwa, anaweka machale... Na ndonya ilikuwa nayo, Nhyao. Ya wastani.

Ma XX M Na Mmakua vilevile.

Ma MC1 M Na Mmakua vilevile. Ilikuwa inaweka ndonya hapa, na chanja wanazo humu. Sasa sio sababu hiyo. Sababu maalum ndio hii ninayokueleza kisa mimi. Pamoja ni mtoto mdogo, na umri mdogo sana. Lakini nimepata historia sana kwa mjomba. Kwamba wewe jihesabu mahali po pote, kwa sababu wewe Mmakonde. Hakuna hata kidosari. Sijui tumo watu sisi ilikuwa kufanya kosa kama huyu mjomba wangu. Mimi huyu mjomba. Akifanya kosa, akamwona ntoto mmoja tu kwenda kulipwa ugoni kule. Aiba kulipalitaka kule la nguo au bunduki, basi. Lakini sio namna hh... au matondo. Kunkuta ntu njiani anatembeatembea peke yake, basi akamvamia tu, akanchukua akampeleka nyumbani kwake. Akamfanya ntumwa. Sasa ukisikia wenyewe wakaenda pale kutaka shufaa, hata kwa kurudisha pesa au kitu cho chote, tunchukueni ntoto wetu. Ilikuwa inafanyika hivyo. Lakini sio sababu ya chare.

Ki TS M Sawa.

Ki DM M Sisi tulikuwa na chare, Wamakonde la wastani, lakini mboni wale wa Nhyao au Wamakua ilikuwa na chare na ndonya ipo wakichukuliwa utumwani.

Ki TS M Sasa sisi watafiti na ninyi pia wasikilizaji kwa hizi sababu zote mbili tunazichukua.

Ma MC1 M Sawa sawa.

Ki TS M Halafu tunapima uzito iko wapi. Mzee unataka kuongezea?

Ma AY1 M Nitakuongezea kwa ajili ya chai... (kelele).

Ma AY1 M Mimi ni Ali Yusufu. Kwa vile wazee wangu nilivyowasikia tumetokea Nyanda muda mrefu hapa, kuhusu chare na Wamakonde. Kwanza Makonde huyu ali... ametoka wapi? Huyu Makonde ametoka wapi? Mapokea ya wazee wangu Makonde hasa hawakuwa na chare na halafu ametoka Arabuni. Ni Mwarabu. Mmakonde hakukuwa na chare cho chote, Mmakonde ni Mwarabu kabisa, na kabila hii imetajwa huko Uarabuni. Lakini wakati wa siku ile za zile za zamani za wakati wa dini dini zamani, ndio Wamakonde

ambao... Waarabu waliotoka kule wakenda ng'ambo. Walipofika ng'ambo mfalme wa nani huku... wa Makka... akataka kuwafuata. Watu wake wametaka kuja huku wafuata huku. Alipofika huku katika wale walipokwenda ng'ambo ndio wale waka... wakatoka pale wakaenda kukaa bara.

Ma AY1 M Kukimbia kurudi Arabuni... kidogo haba... kidogo kidogo nashindwa kuzieleza lakini ni ndefu sana. Katika kukimbia kwao wale wao watachukuliwa tena kwenda huku. Wale wakakenda bara, kule bara ndio walipoanza kujiparuraparura kule, ili wasijulikane. Wasijulikane na mfalme, mfalme nani, sijui nani, sikui mfalme yule ya... maskini. Mfalme nani, sijui. Lakini sio huku. Maana yake Makonde ni Maarabu kabisa mtu... Maarabu kabisa, wawetoka huku wakaenda ng'ambo. Akapanda juu huko, ndio walipoanza kujichanjachanja kule, kwamba wasijulikane kwamba hao ni wale waliotoka Arabuni. (kelele, wengi hawakubaliani naye). Kuhusu habri ya Makonde, na zile chare, ndivyo zilivyokuwa zimetokea zile chare, walijichanja kwa sababu ya hivyo wasio wakachukuliwa kurudi.

Ki TS M Haya, hii tafsiri moja ya mzee, kusema kwamba Wamakonde ni Waarabu. Swali zito zaidi ni kwamba Waarabu wangapi kutoka Uarabuni wakahamia Msumbiji kwa jina la Umakonde, halafu wakaja...

Ma AY1 M Hawakuwa Wamakonde, walikimbia. Kule walikimbia Waarab...

Ma HB1 M Niongezee kidogo kuhusu Wamakonde. Mimi ni Hamisi Bakari, Mikindani, Makengenyeye. Nitatoa shauri ya chale. Mmakua ana chale. Mwera ana chale. Mmavia ana chale. Mimi nimeishi sana sisal estate kule Kabisela, na hawa Wamawiya wenye chale. Wanasema hivi. Maana yake nipata kuuliza mimi. Si mimi peke yangu. Mwingine ameuliza, ameuliza, ameuliza, lakini kila akiuliza jibu ni hili moja. Wanachanganyika pamoja hawa. Lakini ukimwona Mmawiya, Mwela, Ngoni, Nyasa, nani sijui, Wamawiya hawa hao. Wa... ukiwatazama kwa chare, chare zao tofauti. Tumwona mwingine chare sasa ujue huyu ana kabila fulani fulani huyu. Huyu kabila lake fulani fulani. Yaani haiingii katika Wamawiya wengine. Hivi chare zile ni alama ya kabila fulani fulani. Chare hizi hawezi akachanja yule. Hata siku moja. Watazame tu baba wa Mawiya wale, chale zao tofauti kabisa.

Ma XX M Lakini hilo kweli.

Ki DM M Swali ndogo.

Ma XX M Hilo kweli.

Ki DM M Ndio kweli, Wamawiya wale kila mmoja na chale yake, kila moja na chale yake, wale.

Ma XX M Niulize swali.

Ki DM M Huko tulikopita kwingine, na hata katika mwanzo wa mazungumzo yetu hapa, nafikiri kama sikusikia vibaya, ulitaja kwamba Wamawia hao ni Wamakonde. Ndio Wamakonde hawahawa. Sasa nachanganyikiwa kidogo. Huku unaniambia, ni Wamawia mengine, huhu ninaambiwa ni Wamakondwe hawa. Naomaba unitofautishe.

Ma HB1 M Ehee. Marhaba.

Ki TS M Endelea.

Ma HB1 M Kuna Wamakonde, Wamawia. Kuna Wamakonde wa leo, huku sisi tunaitwa Wamakonde wa leo. Ndio sisi hapa. Kuna Wamakonde wa Wamawia wale wa huko, wanaitwa Miteda, sijui huko, Miteda. Wamakonde sisi na wale kuna tofauti ya ulajiulaji wetu. Sisi, Wamakonde sisi hatukati kukatakata kwa kushonya, hapana. Lakini wale Wamakonde wa Miteda wanaitwa Wamawia, Wachacho wale ndio wanaitwa Wachacho. Maana yake Mmakonde hata akija hapa kwa kisiwa hii chake tu ukinsomesha wewe anaweza akaacha shule ambaye nani anasoma akataja sura yake anayeifahamu, kwa sababu ya kuchanjachanja kwake kwa meno yale.

Ma HB1 M Lakini sisi, sisi hivi, sisi kwa historia tu, tunaweza kwenda mahakamani sote, Wamawia, Mmakonde, Wamakonde sisi Mmakonde, anayejitambua pale kubadilisha dini labda kama anayezingizia Waarabu, anayezingizia Ungoni, anayezingizia Umwera, unaona hap... sasa vile vile kwenda sisi wa... sisi Wamakonde sisi. Tunaweza tuka... tukienda pale tukasema, 'Mimi Ngoni, mimi Nyasa'. Na wale Wamako... Wamakonde wale wa Mweda wale vilevile wana... wanakataa kuitwa Mmakonde wale, wanakataa.

Ma Pe SS M Kuitwa Mawia?

Ma HB1 M Kuitwa Mawia, hawataki. Wale Wamawiya, kisa kuitwa Wamawiya, kisa cha kuitwa Wamawiya wale, ni kujikatakata kule usoni, kuvihya. Maana kama ntu anankata hapa pa kuvimba pa kufanya hivi, pamevihya. Maana yake...

Ma XX M Kuvihya ni kuvimba kule.

Ma HB1 M Kuvimba kule. Ndio wakaitwa Wamavihya wale. Sasa ukiwatamkia Umawiya, wanakataa.

Ki TS M Sasa tuje kwenye swali jingine. Ninyi hapa Mikindani mnakubali kuitwa Wamalaba ama Wamwamba ama Wamwambao?

Ma HB1 M Kwa yote tu. Kwa yote sisi. Kwa yote tunayapokea.

Ki TS M Mnayapokea.

Ma HB1 M Kwanza sisi Wamwamba, halafu sisi... nini umesema?

Ma XX M Wamalaba.

Ma HB1 M Wamalaba, Wamalaba sisi. Nini nyingine umesema?

Ki TS M Basi. Wa Mwambao.

Ma HB1 M Mwambao ni sisi.

Ki TS M Lugha yenu ni lugha gani mnayozungumza sasa hivi?

Ma HB1 M Kiswahili.

Ki TS M Haya, sasa tume... tumefika hapa. Kwamba tumetoka huko tulikotoka. Wengine wamesema wao Waarabu kidogo, wengine hivi, ndio binadamu tulivyo.

Ma HB1 M Ndio, sawa.

Ki TS M Na kwa faida yenu Waafrika sisi katika shughuli shughuli hizi za utumwa hizi, baada ya kuchukuliwa chukuliwa vizazi, wengine tumefika mpaka Iraki ya leo... Persha ya leo.

Ma HB1 M Ndio.

Ki TS M Kuna mji mmoja unaoitwa Shirazi, eeh. Kuna mji mmoja unaoitwa Shirazi, na Waafrika wamefika huko. Katika karne ya 9. wamefanya fujo wale watumwa weusi wale, wakafanya fujo wakapindua serikali. Wakaongoza serikalini kwa miaka miwili. Mnasikia wazee?

Ma XX M Sawa. Insallah.

Ki TS M Wakati ule wanaongoza serikali miaka miwili... (kelele) wazee... mnaharibu rekodi. Ninyi msizungumze kabisa huko, tunarekodi hapa. Ni kwamba Waafrika wale baada ya kuwa wamepata uhuru wa namna fulani wameanza kuja na vyombo vya taabu taabu baharini. Kwa hiyo inawezekana mtu wa Ethiopia akafika hapa, mtu aliyotoka Nigeria akafika Kilwa na nini. Hawa wachache wachache waliokuja ndio

wakajitia Ushirazi, kwa sababu ni kweli wakatoka Ushirazi. Lakini si kwamba ni watu bora, kwa sababu ni vizazi vya utumwa uleule vimekwenda kule na vimerudi. Kila aliyerudi Afrika akaenda pahala na akapafanya pale. Kwa hiyo hii tuiache, haina thamani yo yote.

Ma XX M Sawa.

Ki TS M Na Mwarabu kama akaja Mwarabu hapa, atakuwa ameendelea kubaki Mwarabu kwa namna moja. Sasa kama akachanganyika akawa ndio sisi basi Wamakonde, Wamalaba leo, Wamwambao, tuishie pale. Sasa lugha yetu ni Kiswahili.

Ma XX M Sawa.

Ki TS M Kazi zenu haswa mnazozitegemea katika maisha yenu ni zipi?

Ma HB1 M Ukulima tu.

Ma MC1 M Ukulima na kuvua.

Ki TS M Kazi mbili: kulima na kuvua. Tayb. Mila na desturi zenu ambazo mnafikiri kwamba hizi ndizo zetu sisi tu zinatutofautisha na Wamakonde na Wamakua na Wangoni na Wanyasa ni zipi? Mmoja mmoja basi. Mila na desturi na tabia, yale mambo makubwa makubwa. Kwamba ndio wa zetu ziko namna kadha kadha kadha kadha, tunao wa hivi tunao wa hivi. Unyago wa watoto wa kike tunawafunza hivi na hivi. Nyando la watoto wa kiume tunafanya hivi na hivi na hivi. Vitu vyote hivyo mmoja mmoja kila mmoja aeleze.

Ma HB1 M Sawa.

Ki TS M Anayeanza ataje jina, aeleze.

Ma HB1 M Mimi nazungumza hivi kuhusu unyago.

Ki TS M Jina?

Ma HB1 M Jina tena?

Ki AH M Inatosha, tunajua tayari.

Ki TS M A-a, kwa sababu tunataka kila topic tupate nani anazungumza.

Ma HB1 M Mimi Hamisi Bakari, wa Mikindani, mtaa Makengeni. Mimi na mwanangu tunataka kuchezea leo. Ndugu zangu hao woote wanakaa mbalimbali ndio wapelekea habari kusema mwaka huu na mwezi huu mtoto wangu namchezea.

Ki TS M Kuchezea maana yake nini?

Ma HB1 M Kumtahiri. Kama nina ntoto wa kiume, kumtahiri. Wananiuliza jamaa zangu hawa, 'Lini?' Kila ndiye ninayemwendea anauliza 'Lini wewe una tamko yako ya kuchezea mtoto wako? Lini?' 'Jumamosi, ngoma'. Basi Jumamosi hiyo, wacha na mwaka huu, lakini kwa miaka iliyopita ilikuwa watanikuta nimetandika jamvi namna hii. Nimechukua mtama wangu, pishi tatu tunamwaga hapa. Basi huyu akija huyu na mtama wake, huyu na mtama wake, mtama wake, mtama wake, kumwaga palepale. Yaani uwe mwingi ule mtama... Usiku ule ngoma. Ngoma hiyo kwa lugha inaitwa 'ulimbondo... ulimbonjo'. Ngoma hiyo inaitwa 'ulimbonjo'. Sasa watu woote wengine wenyeji wangu, jirani zangu, wanasema, 'Leo Hamisi ananchezea mwanawe kumtahiri kesho asubuhi'. Sasa anamwaga kama mume, anamwaga nke, 'mimi nakwenda kwenye ulimbonjo kwa Hamisi'. Kama ni mke, anamwaga mumewe, 'Mimi nakwenda katika ulimbonjo kwa Hamisi'. Kuja, na che... sasa kuimba kwake sio kupigapiga magoma, hapana. Kuimba kwake wewe utaona raha kuliko ngoma. Unasikia bwana huyu ndiye mwenyeji yeye wa nini fidi, mafidi, mafidi ya kinanda. Haitoshi kitu

kuliko ngoma hizo za kuchezea ntoto huyu. Ee, wanapiga makofi namna hii (anapiga makofi)... mpaka asubuhi. Asubuhi ngariba ni huyu.

Ki DM M Imba kidogo basi. (kicheko) Ndio, ndio mfano.

Ma XX M Utajua?... Atajua.

Ki DM M Mfano.

Ma HB1 M Niimbe kidogo?

Ki DM M Ee.

Ma HB1 M Wamahe nna... (anaimba na kupiga makofi)

Ma XX M Mnapeana namna hii?

Ma HB1 M Namna hii, kucha. Sasa anasema kwa lugha, anasema, 'Wanawake wamelala usingizi, musiwaamche watakuja wenyewe hapahapa kwa kunoga ngoma, kwisha. Asubuhi anasema, wangeriba wale, wanaimba pale. 'Shoka usiache, moto usiache, kuku usiache, kisu usiache, mundu usiache'. Anahesabu, basi wanatapaka vitu vyote alivyohesabu ngariba yule anayekwenda kumtahiri mtoto kuchukuachukua vitu. Na mtoto wangu anawekwa mgongoni kutangulia moto na mtoto na wachen(?). Sasa kule sasa wakifika kule maulidi sasa. Zamani pale palikuwa kelele kelele 'woo-woo-woo-woo', hapana. Lakini sasa maulidi, kwa kitaalamu chetu kwa wakati huu. Sasa huyu maulidi, 'soma shadi mwalimu', ndio una.... kongwa pale. Mtoto analia lakini kusikia nje hawasikii.

Ki TS M Rudi nyuma kidogo tueleze ile jando tunayotaka sisi.

Ma HB1 M Jando?

Ki TS M Kule kumtahiri mtoto, kwa makusudi gani, na vinafanywa vitu gani, sio ya habari ya kile kitendo, kile tunakijua. Lakini makusudio haswa ya jando yalikuwa nini?

Ma HB1 M Asili ya jando ni ku.. ni kumrihimia mwana Mtume...

Ki TS M Hili tunalijua. Katika maisha ya yula Mmakonde yule katika maisha yake, kile kitendo kinamfunza nini?

Ma XX M Awe na adabu nzuri.

Ki TS M Tunataka mzee aseme.

Ma HB1 M Eee, ndio sasa hapo nikija hapo sasa kwa sababu hayo tunagonga hata mwananke ndani ya nyumba. Hapo yule mtoto anakaa kule jandoni. Anakuwa na kungu yake kama huyu, kumkaza yule mwali. Wewe ukenda mwgope mama yako na baba yako na watu wote. Wewe, mwali wewe. Unasikia? Mbukwa, kuitikia kwake mwali anasema, 'mbukwa'. Wewe unamfunza yeye mbugwa, unamfunza. Yeye anaitikia 'mbugwa'. Ukienda njini wewe ukinkuta mwananke amekaa kitandani usigongegonge huku, anatoka hezi. Hii ndio maana yake. Unaona? Wewe ukienda wewe usifunue funue wengi shafunua ntakula nini sijui. Unaona? Ukenda utamkuta mama yako amejifunikia hapo, wewe ukienda ndani ya nyumba humo usifunue chungu kile. Hii heshima, uwe na heshima wewe, na adabu, kuogopa watu na wazazi wako. Ndio. Kwisha hapo, ukipata siku ishirini thelathini mwali anatoka nje. Akitoka nje pale kuja kumfanyia sherehe pale, basi asubuhi kama ana... wote hawa watampa mkono wa halawa, halawa, halawa, hala... Mwenye sumuni, shilingi, anampa mwali huyu. Lo...

Ki TS M Hii inatosha sasa. Habari ya ndoa, ilikuwa mnaozwaozwa vipi?

Ma HB1 M Ndoa zamani haikuwepo.

Ma XX M Kuna kuongea bwana Hamisi, bwana.

Ma YS M Mimi ni Yusufu Hamedi Selemani. Nakaa hapa Mikindani. Mimi nitazungumza kile kinachoulizwa. Swala kuhusu ndoa. Ndoa tangu zamani ilikuwapo. Lakini tafauti. Tangu zamani watu walikuwa wanapeana wanawake kisheria zao kimila. Na ndoa zimekuja karibuni wakati za dini zetu hii ya Kiislamu huku. Ndio ikaanza ndoa kuwa na hutuba maalum na kuoana. Lakini ndoa tangu zamani kabla hata dini hazijafika huku ndoa zilikuwapo. Wakifunga ndoa wazee wakipeana kipagando kimila zao. Huwezi kumchukua mtoto wa ntu bila hizi ya mienzazi. Mpaka mienzazi amekubali ndio mpate mke. Na mpaka sasa hivi ndio dini imetufunza watu kuoana kisheria maalum, kihotuba.

Ki TS M Ebu tueleze mchumba alikuwa akipatikana vipi katika hizo siku za jadi. Na mpaka leo mambo yamegeukageuka kwa kiasi gani?

Ma YS M Siku za zamani mchumba akipatikana mzazi wa mwenye mtoto mwanamume anakwenda kwa mzazi mwenzie mwenye mtoto wa kike, kwenda kumposa. Kuwa mimi ninamposa ntoto wako na namposa ntoto wangu.

Ki TS M Bila ya wale watoto ku...

Ma YS M Hapana, bila kuonana watoto, hapana.

Ki TS M Na leo hii?

Ma YS M Hivi sasa wanaweza kuwa... kuonana wenyewe watoto wanawake wanakutana na shauri yao wanakwenda kunani... Lakini zamani walikuwa wale nke na mtoto huyu hawaonani. Mashauri yao wanafanya wazazi ili kuwatafutia ndoa. Walikuwa hawatafuti wenyewe wale watoto wanawake, wazazi wenyewe.

Ki DM M Lakini kwa nini walikuwa wanachukua ile dhima. Kulikuwa na sababu maalum?

Ma YS M Ipo. Sababu watoto walikuwa wanatawishi walikaa nyumbani mwao. Wale watoto wa kike walikuwa wanatawishi, wanakaa nyumbani mwao.

Ma XX M Ilikuwa zamani...

Ki TS M Usisahau kutaja jina.

Ma DC M Mimi jina langu Dadi Muhammedi Chihinde. Mi mwenyekiti wa Mitengo. Jinsi nilivyoona ndoa zamani, baada ya kuchazwa yule mtoto wa kike, basi ilikuwa anadhimitiwa ndani, hatoki nje. Yeye anakaa humo ndani kunsabiri aje nchumba. Sasa ndipo anapopanganyika nzazi wa kiume kuja kukuposa wewe mimi. Namposea mwanangu, binti yako. Asante. Sasa hapakuwepo na hotuba. Isipokuwa ilikuwa kutoa kitamwo tu.

Ki DM M Kitamwo ndio nini?

Ma DC M Kitamwo ni kile ambapo kitangulizi kya matamko yako yale. Unanieleza kwamba nataka ngitakali moja hapa la nguo, au bunduki. Basi nachukua mimi napangulika na kuja nakupa, wewe unaniruhusu kuja kui... kunchukua mwanao, kumpeleka nyumbani kwangu. Basi. Hapakuwepo na ndoa. Ndoa imekuja kiutalamu siku hizihizi baada ya kuingiaingia Waarabu wa kutufundisha masomo na kutuondoa kizani tulikokawa. Ndivyo ilivyo.

Ki TS M Na kitu tusichanganye. Ndoa kuna maana mbili. Maana ya kwanza ya ndoa ndio hio, kwamba mtoto wa kike hatoki mjini kwake kwenda nyumbani kwa mtoto wa kiume. Sharti kwa idhini ya wazazi wake. Hio

ndoa. Maana yake si sisi kama mbwa. Ukiwa na haja unaruka tu. Kwa hiyo ni ndoa. Na ndoa ya pili ndio hii ynayoeleza kwamba kuna hotuba na nini. Lakini tunachokitaka haswa ni ule msingi kwamba ninyi katika maisha yenu ili kupata uadhilifu wa jamii yenu, ee, tumeshaupata huu kwamba walikuwa hawatoki mabinti huku kuchezewachezewa tu hivihivi barabarani kama wanyama. Lakini kulikuwa na utaratibu maalum. Na swali la mwalimu hapa kusema kwamba kwa nini wazee ndio waliokuwa wanajihusisha kuchagua wake wa watoto wao. Pamoja na jibu lililotolewa lakini ni kwamba wazee ninyi mnazijua akili za vijana wenu vizuri zaidi kuliko vijana wanavyojua akili zao katika jambo la ndoa.

SIDE B

Ma DC M Ilikuwa nimezungumzia habari zile za ndoa kusema kwamba ilikuwa mwanangu namwona huyu sasa ameshafikia hatua ya kufikia makamu ya kuweza kuntaka nke. Basi ndipo ninapokuja kwa bwana huyu kumweleza nantaka binti yako, nimpe mwanangu. Na kumwogopa atazambaa katika mji akaharibu taratibu za nji mzima. Maana pale watahika ugoni, pale watahika ugoni. Sasa afadhali nimpe nke awe naye ili taabu zile zisitokee. Ndio maana kabisa ya wazee kufanya hivyo zamani.

Ki TS M Naam, nani anataka kuongeza? Samahani kidogo, taja jina na mtaa unaokaa, halafu tueleze.

Ma RA2 M Mimi jina langu Rashidi Muhamed Ali Maaruf Mwema. Ni... ninakaa kijiji cha Magengeni hapa. Nilikohama Milumba nikahamia Magengeni. Mimi narejea katika kipindi kimoja, ambacho umekigusagusa, lakini umeshindwa, ingawa hukuendelea, lakini umeshindwa. Lakini mimi nakukumbusha. Kipindi cha mila, maana yake wewe hapo umeuliza sana mila, hata mtu aliyetaja mila. Na mimi naitaja mila. Hio ndoa iliyogusiwa kabla ya wakati uliopita wa zama za zamani, ndoa haikuwepo. Na hii ilikuwa ndio mila yetu Wamakonde. Kumchukua mtoto wangu kumpelekea mzee mwenzangu yule kama hongo au kama mila yetu kutafuta ujamaa. Maana yake hii ndio ilikuwa mila zama hiyo. Ndio maana ndoa haikuwepo. Sasa yule alikuwa jamaa yangu milele, kwa mwanawe. Maana amekwenda kumpa mwanawe aje amwoe wangu, wangu aache kumwoa, ni kupa... maana yake wanasema Wamakonde 'kupalikwa', kupalikwa, yaani kufunganisha. Hapakuwepo ndoa.

Ma RA2 M Hii ilikuwa ndio mila yetu sisi Wamakonde wa pwani mpaka bara. Kwa sababu tulikwishachukua mila yetu. Maana yake sisi hatukuwa na sultani, Wamakonde hatukuwa na sultani. Alikuwa na sultani Mwela, yaani mfalme fulani, Ngoni mfalme fulani, huyu Songea... Mnyao. Lakini Mmakonde hakutawaliwa. Hakuwa na sultani wala hakuwa na mkuu, hapana. Ila isipokuwa tulikuwa wenyewe, tuakubaliana kwa utu uzima wetu na uungwana, tulipenda sana uungwana, zamani, tulipenda sana. Basi ndio ulikuwa ndio usultani wetu. Sasa tukaiweka mila ya kuwa sisi mila yetu lazima tukae mtoto wako wewe aje amchukue mwanangu mimi huyu kuja kukaa naye na kwako watazaa watoto. Sasa watoto wale katika mila yetu huyu ana nduguye, anaitwa mjomba. Sasa mjomba ndio watakaorithi watoto wale, mila yetu ya zamani. Sasa ikawa ndio mambo yamekuwa yamekaa vizuri, kwa sababu ya mila, iliyokuwepo katika nchi nzima hii ya pwani yote, kupandia bara hii ya Makonde. Ndio maana ya kuita 'kupalikwa' kwa nyumba mbili, kwako na kwangu.

Ki TS M Niulize swali. Katika mila hiyo mlikuwa mkiruhusu uzinzi?

Ma RA2 M Ndio, hatukujua la akhera wala la dunia wala la Mungu.

Ma XX M Hatukuruhusu uzinzi.

Ki TS M Mlikuwa mnaona fahari mtoto wa kike achukuliwe na kijana usiyemjua?

Ma RA2 M Hatukujua kitu wakati huu.

Ki TS M Aa, jibu, nasema ulikuwa unaruhusu wakati huo baba wa nyumba alikuwa anaruhusu binti yake achukuliwe na kijana wa kiume vyo vyote vile?

Ma RA2 M Ndio sisi... alikuwa anapelekewa...

Ma SN M Aa, haikuwa hivyo bwana.

Ma RA2 M Zipi?

Ki TS M Mzee Barua anataka kujibu.

Ki DM M Ni hivi, labda tuweke mambo sawa. Ningependa kitu kimoja tuki... tukiweke wazi na tukitofautishe. Ee, sisi hatufikiri kwamba huko nyuma tulikuwa washenzi. Hatufikiri hivyo. Ili ningependa tuliondoe katika fikira zetu. Hatufikiri kwamba tulikuwa katika kiza, hapana. Sisi kama Waafrika, kama Wamakonde tulikuwa na taratibu zetu zilizokuwa zinakubalika wakati huo. Hazikuwa za kipuuzi, hazikuwa za kishenzi, hazikuwa za gizani, hapana. Ila kibinadamu anavyozidi kuendelea na kupata mabadiliko mengine.

Ma XX M Ewallah.

Ki DM M Sasa hilo ningependa liwe wazi.

Ma XX M Sawasawa.

Ma RA2 M Sasa katika kuwa wazi, mwalimu, ni ndio maana mimi nikatoa nasaba ya kitu tulichoanzia chini. Sasa wenzangu hawakielewi, kwa sababu hawakukiona. Na kama wangelikiona, wangalielewa mimi nimetoka wapi. Mpaka sasa tumeendelea, tumekuwa watu wa namna hizo. Ndio maana mimi nikazungumzia kwamba mila, mila ilikuwa lazima iwe hivi. Sasa mwalimu mwingine wako ameniuliza wakiruhusiana ku... katika uzinzi. Hii imekuwa katika nasisa ya mambo ya Kurani, mambo ya dini.

Ki TS M Basi sio hivyo. Kama alivyoeleza mwalimu ni hivi. Maake sisi tunajaribu kupata misingi ya maisha yetu ya Kiafrika. Nilipokuja mara ya mwanzo mwezi wa saba niliulizauliza wazee. Na wakanambia, kwamba katika Umakonde lilikuwa ni jambo la aibu kubwa sana msichana yo yote kuonekana amevunja miiko. Na mwiko si mwingine, ni kwenda kulala na mwanamme nje ya taratibu. Nafikiri tunakubaliana hapo.

Ma XX M Ndio.

Ki TS M Nje ya taratibu, bila ya kuwa na taratibu za Korani au taratibu za nini. Lakini taratibu za wazee walizoziweka wakati ule. Sasa ndio pale nikasema, lengo la maisha ya ndoa ni lipi. Mzee akanieleza kwa namna nyingine kwamba mimi namchukua mtoto wangu na kwenda kumkabidhi mtoto wa mwenzangu, ili waishi pamoja, na kutumia neno ulilotumia, 'kupalikwa'. Na hii ndio ndoa. Ama siku zile ama leo, lengo haswa ni hilo. Na katika ndoa yo yote mume kutoka kwenda kulala na mwanamke mwingine, mke kwenda kulala na mume mwingine, ni udhaifu wa kibinadamu tu. Lakini katika jamii sijui kama zipo ambazo zinasema, 'sasa wewe fanyeni hivi', watu wakaona fahari. Hilo ndilo tulitaka tuliweke sawasawa. Naam, mzee uongeze.

Ma RA2 M Na mimi katika tamko langu zaidi naendelea kwamba haikuruhusu kwamba wale watu wafaye uzinzi, hapana. Isipokuwa mimi na baba yule tulikuwa tunashirikiana katika upande wetu wa ileile mila, tukakubaliana. Unafahamu? Sasa watoto yule wako wamekua, wangu wamekua. Sasa tutafanya nini? Wewe unatoa kitu maalum kama alivyosema mzee mwenzangu wa kwanza, kwamba taka la Japani. Maana yake uka... mimi unakuja kunipa kama mtu umekuja kushika amana ile ya kuwa ndiyo ndoa yetu. Hapakuwepo walimu, hapakuwepo nini. Tukakubaliana kwamba sisi... unafahamu, mwanangu kaolewa na

mtu... mtoto wa fulani. Na fulani ni mke wangu. Tukafanya furaha, tukafanya nini kwa zama zilizopita katika njia za uzee uliopita wa zamani. Maana haya yote yamekuja sasa. Hata miaka ishirini, siku thelathini haizidi, kati ya kuja. Sasa kujua katika kiza kama ulivyosema mwalimu kuiondoa kiza na kuiweka uwangaza. Ndiyo njia ambayo katikati hapo huyo mtoto wako ndio umeweka ndani ya nyumba. Baada ya kumweka ndani ya nyumba haji mtu kumwona ila mzazi, kama shangazi, ndugu wako wewe kumtazama yule mwanangu mimi. Antazame, amjue mzuri. Halafu ndio anakuja kum... mtoto wa huyu, anakuja kumtazama, kwamba mtoto nimemwona mzuri sana. Kwa hivi afadhali tukampose. Inaanza kutoka ile kiza. Ndio ikafanywa mapatano na kuendesha mambo ya posa. Mpaka ukafikia katika kukubaliana kufanya harusi. Huwezi kumwona, wala yule hamwoni, wala hampatanishi pamoja, yaani katika kukatika zile mila. Zimekatwa mila, lakini zama zilizopita ndio mila yetu. Hakuna njia nyingine ya Umakonde, hata kidogo, isipokuwa hii. Sasa ndicho kitu kilichoendelea, tukawa tunakwenda, tunakwenda, mpaka tukawa tuna...pata elimu za kuweza kuwasomesha watoto, mpaka tukawapa sisi wenyewe tukawa... tumesoma zaidi, na tunaweka njia za kuoana. Tukawa tumeoana.

Ki TS M Tayb, sasa tuje kwenye mila zenu za vilio. Na tukiuliza swali kama hili maana yake mnatueleza nyuma ilikuwaje na leo mnafanyaje. Pakitokea kifo mjini mlikuwa mkifanyaje na sasa mnafanyaje?

Ma RA2 M Toka zamani katika kifo... zinaendelea lile... kifo tulikuwa tunafanya masikitiko kama kama ya kawaida. Tunakaa siku tatu baada ya kuzika. Tunafa... tunakaa siku tatu.

Ki TS M Kabla ya kuzika, maana yake kilio kimetokea, mtu amefariki.

Ma RA2 M Ndio, mzee wa zamani, nitarudia pale. Mzee wa zamani ilikuwa kama amekufa, amerukwa pale, siku tatu mtu hazikwi. Inapigwa ngoma, jina lake 'ngula ntwe', ngoma ile imesoma.

Ki TS M Itamke tena tulipate neno.

Ma RA2 M Ngoma hii ni 'ngula ntwe'. Unasikia inapigwa 'kuwa kuno, kuwa kuno', siku tatu. Huyo ni mtu, mtu mzima, au mzee wa pale. Yaani anajua Mitengo, anajua pale Pemba, anajua Mikindani hii, kwamba pale pamekufa mtu. Mpaka siku ya tatu wanakusanyika wazee wote.

Ki DM M Swali, kabla hujaendelea.

Ma RA2 M Ndio.

Ki DM M Aa, siku tatu si siku chache binadamu amekwishakufa. Je, ya miili kuna taratibu ya kumhifadhi marehemu mpaka hapa...

Ma RA2 M Sana. Hifadhi zake za kumtabaduni ule wa kumwosha na kumnyoosha, na kumpaka mafuta na sabuni wa kumtunza sana bila kuharibika. Bila kuharibika kwa vizuri sana, maana paliwekwa watu maalum wa kumwanguka yule marehemu, yule ma... ile maiti. Unafahamu? Basi, wanakutana kufanya shauri ya kuzika na wakateuliwa watu wa kuzika. Baada ya kuzika ndio tunarudi kufanya shauri ya kuwa tufanye tatu, yaani tanda, kulala siku tatu. Siku ya tatu wanamaliza na kupiga sadaka zao na kumaliza. Hii ilikuwa mila zama za zamani, toka nyuma. Mpaka tumeendelea sasa ndio tunaanza ku... kupata labda elimu zaidi sijui. Ndio tunakwenda hata siku moja ileile baada ya kufa leo, kesho akizikwa, kesho palepale unaweza kusoma tukamaliza kila mmoja akaenda kwao. Lakini hii ni mambo wanayosema ya utaalim. Lakini jadi ilivyotoka na zamani ilivyokuwa, kama unataka mila ndio hizi ninazosema mimi, wengine kwa sababu hawazilelewi mimi nitakuwa mjinga sana.

Ki TS M Sawa. Sadaka, nani anachangia sadaka?

Ma RA2 M Vema. Zamani ilikuwa umoja wa baraza. Wana ndugu wale wote waliofika pale wanalichangia lile baraza. Sio wewe mwenyewe peke yako. Kama alivyosema nzee wa kwanza, kwamba unaweka pale

kama ile mambo ya jando. Unaweka pale pishi mbili, yule analeta pishi mbili, yule, yule, yule, zinakusanyika pale. Halafu, wakati ule mbuzi hakuwa ghali. Kiasi shilingi sita saba unapata mbuzi. Sasa zinatolewa pesa, unaona zinawekwa pale kwa sababu ya kitoweo. Ikapikwa chakula kama kawaida kufanya sadaka zake. Hio mila ilikuwa zamani. Mila, mimi niko katika mila.

Ki DM M Sawa.

Ki TS M Je kuna la kuongeza wazee, ambalo tumeliacha, ambalo mnafikiri muhimu kwa mji wenu sisi tulijue? ... Wazee, tunataka kufunga...

Ma XX M Msafara.

Ki TS M tufanye mambo mengine.

Ma RA2 M Haya, labda ninyi mtakalo tena ulizeni tu.

(kicheko)

Ma HB1 M Mimi jina langu Hamisi Bakari wa Mikindani Makengeni. Asili ya utajiri, asili ya utajiri za mane, za mani. Palikuwepo kobe. Mnamfahamu kobe? Sungura. Mnafahamu sungura? Na... aah... huyu nalwihu nini Kiswahili?

Ma XX M Kinyonga.

Ma HB1 M Kinyonga. Hawa tatu.

Ki TS M Taja hilo jina lingine lakini.

Ma SN M Nalwihu.

Ki TS M Sawa.

Ma HB1 M Asili ya utajiri hiyo. Wamekaa watu watatu hao wakasema, sisi hapa mbona hata tukienda porini kuvunja kuni tukija hapa tukiuzwa hakitoshelezi kitu, hatushibi. Sababu gani? Sehemu za Bazala kuna sultani mmoja, yeye ni tajili wa kanda. Tajili mkubwa mno. Akatoka sungula akasema, 'Sehemu hii huku mimi nasikia kuna tajili. Hata hatushirikiani sisi, twende, tukamkope'. Kobe akasema, 'Aa, lakini hata tukienda tukikopa, tutapata?' Alisema, 'Tutapata'. Aah, kinyonga anasema kwamba, 'Wewe sungula, wewe kobe, sisi, mimi na kobe huyu, mwenendo wetu huu kutoka hapa tu mpaka maili moja, mwendo wa siku mbili tatu, huko tutafika?'

Ma HB1 M Akasema, 'Tutafika. Hata kwa miezi sita tutakwenda. Tutafika tu.' 'Je, tukienda kule, kutuona sisi mwenendo wetu yule tajiri yule anaweza akatuamini sisi?' Asema, 'Atatuamini, lakini tushirikiane, tuzungumze kitu kimoja'. 'Vyema'. 'Tunapokwenda kule akim... maana yule tajiri yeye lazima amluhusu mtu mmoja aondoke. Wabaki wawili hawa. Sasa wawili wale watakaobaki washirikiane wale. Haya, ataanza nani?' 'Nitaanza mimi sungura'. 'Hapana. Aanze huyu, kobe huyu'. 'Akitoka kobe aanze nani?' 'Kinyonga'.

Ma XX M Nalwihu huyo.

Ma HB1 M Ehe, ehe, basi. Kwenda pale katakatakatakakata siku tatu nne tano wamemfika kwa tajiri yule. Kufika 'salaam aleikum', wameitikia. Basi, haya, waita watumishi wake ndani ya nyumba watengenezee vyakula wageni wamekuja. Tandiko jamvi kama hili, wamekaa pale. Wamekaa pale, sungura anaanza, 'Bwana tajiri, sisi tumefika, sisi ni wageni wako. Kwa hiyo sasa sisi tuna njaa, tunaomba utusaidie. ...tupatie kitu cho chote cha kuweza tupate... tufanye staftahi majumbani kwetu.' Haya. Anaanza kinyonga sasa. Anasema, 'Mimi jamaa nimeshikwa na haja'. Kinyonga kutoka pale tu njia iko sawa ya kwenda kufanya haja yake. Tajiri anantazama... yule, yule, ninyi kutoka kwenu kuja hapa siku ngapi? Anasema, 'Leo tunafika

siku ya tano'. Aah, nyinyi shughuli hii hapa mmekuja ku... kama ninazo senti mimi ninaweza nikupeni. Mimi kweli tajiri. Mnaona jumba yangu hili limejaa fedha hili. Ninatafuta watu niwakopeshe. Yule anaweza akalipa yule? Mbona anakwenda vile? Sasa hawa wawili ...(matangazo kuhusu ziara ya rais Mwinyi kuja kugombea urais Mtwara kesho yake yanasikika kutoka gari inayopita)... waliobaki, sungula, na kobe anamwambia tajiri kusema, 'Sisi tumekuja, kwa ahadi yetu tuliyowepo, lakini sisi tulikuwa matajiri wakubwa kabisa. Wazazi wetu wametujaa, watajiri sana. Walipotuzaa wazazi wetu, mzazi wa huyu aliacha mali yake nimetoweka, mzazi wa huyu ameacha mali nimetoweka, mzazi wa yule, yule ndio alikuwa zaidi utajiri wake. Lakini mitoweka Mwenyazi Mungu ametunyang'anya. Basi, ndio tumekuja kwako. Yule tajiri sana yule. Basi, amefanya haja yake, amerudi pale. Akija pale, haya, amekaa kidogo. Kobe sasa, anakwenda, kakacha kakacha, kakacha. Tajiri amuliza, aah, lakini hata yule nikimkopesha fedha yangu itarudi ndio? Mbona anakwenda vile? (watu wanacheka). Anasema, 'Allahu akbar, hapa nimekuambia nini bwana?' Kilio moja wa tajiri... na yule vilevile, tajiri mkubwa sio unamwona vile. Kwenda kobe amerudi pale, amekaa, anaanza sungura sasa. Anaanza sungura, 'Mimi, aa, na mimi tumbo sijui tu... nini sijui, aah... si nini yule togwa ile tuliyokunywa pale njiani ndio maana yake'. Basi sungula alipogunduka hapa hata yule tajiri hakumwona amefanya kama kuruka vile. Aah, yule bwana yuko wapi? Loo, yule katika kuja mpaka akatia njia, huyu kobe alikuwa... alikuwa yule ndio farasi wetu wa kutuchukua sisi. Huyu bwana alikuwa nyuma, mimi nilikuwa mbele. Ndio yule unayemwona yule. Yule ana hatari yule. Hapa bwana wewe ukifanya ziyaka.

Ma XX M Kule kwetu yule tunamtisharifu.

Ma HB1 M Hapa ukifanya ziyaka kama hukutupa fedha hapa ni hatari yule bwana. Atamkwenda kule sungura. Dakika tano kumi amerudi pale. Tajiri yule. Haya akawaita watumishi wake. Toa mabusati haya, toa masanduku ya fedha. Sasa atakwendaje masanduku haya sio tuazime watu watuchukulie mpaka makwetu. Haya, akakubali. Akikubali watu watatu, wanne akawapa mabusati, akawapa vyakula, akawapa na fedha wachukulie hawa mpaka kwao. Basi, wale... kufika kwao. Wale jamaa kulala asubuhi wamerudi. 'Je, sasa tufanyeje fedha hii?' 'Sasa tugawane gawane, kila ntu ajitumilie tumilie fedha yake'. Ndio maana wa utajiri hivi hata watajiri hawa wote sisi watu weusi sisi utajiri wetu tumepatia kwa hivyo, kwenda kumdanganya ntu. Sasa wewe bwana, mtu wa Dar-es-Salama, wankubwa wa Dar-es-Salama, bwana huyu sijui wapi, Ulaya gani sijui. Sasa katika sisi, sisi, sisi tumekwisha, lakini katika hawa vijana vijana hawa pengine wanaweza wakamwona hawa huko Dar-es-Salama huko. Wanakizungumza hawa Kimombo hawa. Basi msione ajabu. Ee, basi hadithi yangu imekwisha hapo.

Ki TS M Asante, asante.

Ma DC M Mimi jina langu naitwa Dadi Muhammedi Chihinde, mwenyekiti wa Mitengo. Hadithi yangu mimi sio ndefu. Ni hadithi ndogo sana, lakini ina maana yake mazuri zaidi. Yaani kuliwepo sultani mmoja. Huyu sultani ana binti yake. Lakini haolewi mpaka ampate ntu, ambaye atakayeweza kuzuia upepo. Kigoma kimepigwa, watu wamejaa, ametoa amri. Ndani humu juu ya ghorofa kuna binti yangu. Lakini hawezi akampata ntu kama sikuzuia upepo. Asante. Watu wakajitahidi watu wanene wanene ndovu, suki na simba. Nyama wa aina yote yote, hata wa baharini kina nini... papa wakubwa wakubwa wale kina hamlani nini. Wakashindwa kabisa. Sungura akasema, 'Mimi nakwenda kujaribu'. Aah, wewe utaweza wapi? Wameshindwa watu wakubwa wakubwa, utaweza wewe? Akasema, 'Mwenyewe Mwenyazi Mungu atajiadhimisha'. Akaenda zake.

Ma DC M Mimi nimekuja, najiandikisha jina langu. Akaandikisha kutenda haya. Akamwambia, 'Lakini mimi nna lazima moja. Lazima yangu nnapoondoka hapa nipowazane na huyo mwali pamoja na watumwa wakanitazame kazi ninayofanya kule'. Sawa. Ameenda zake. Na wale...Amefanya kazi siku ile. Ametega ntego. Amempata keleng'ende. Yaani kuna ndege mmoja anayeitwa keleng'ende. Akaambia, 'Nchukulie huyu nyama, uende ukawape huko mjini, nyama yote, watafune. Lakini mimi ninachotaka wanibanikie nchuzi. Ndio ninayotaka mimi, nitaporudi huku katika shughuli zangu huku, nikute tayari mambo hayo yako

tayari. Nna... mimi niko... nn... nimekufanya kazi zangu za kumvia upepo. Lakini kesho natumai itakuwa tayari tu. Nimeshazungumza nao tayari, upepo utakubali tu, lazima. Haya, wampeleka. Wamemweleza yule bwana nkubwa yule. Haya, wamepika keleng'ende, amekwisha ametiwa chuzwi nini nini, hali mzuri. Nyama imetafunwa. Wameba... wamepasua nti. Wameu... wameutengeneza vizuri. Kila wakitia maji hayakai. Kila wakitia maji hayakai.

Ma DC M Ala. Huyu amenimpuzi, bwana ee. Hii lazima uliyetupa kuweza kuweka maji ndani ya mbano hayakai mboni. Hayakai sasa ndio... Aah hii imenikatotoa shiraiti za namna hii. Maana yake nini?' Sungura huyo, yuko huko. Basi, jioni anarudi. Akirudi amekaa pale tungu. Kazi kubwa anayofanya kule. Haya, tayari kazi zangu mimi nilizo... nilizotumwa kunifanyia sasa mimi sianzi kula kitu kingine kama si kitu hicho nilicholazimisha nibanikwe. Sasa ndipo anatoka mwenyewe sema ah, 'Wewe umekuwaje bwana?' Eeh, umetulazimisha tubanike ma... nchuzi, yaani ni maji yanaweza yakakaa katika mbano kwa... ' Sungula akacheka. 'Nasikitika sana mzee. Yaani wewe unatukosesha binti yako kwa sababu ya upepo kuzuia. Upepo na maji si sawasawa? Nani ataweza kuzuia upepo? Sasa imekuwa jambo hili basi na mimi nimetumwa kitu hichi nikitengeshwe, mimi nipate kutafuna kitu hicho na mimi nikazuie upepo. Na upepo nimeshazungumza nao. Kusho hautavuma kabisa'. 'Aa, basi imekuwa jambo hili jambo gani basi?' Basi akapiga kigoma. Huyu amenishinda kwa ghele basi nikabidhi binti yake... binti yangu. Akankabidhi akampata nke. Hadithi imekwisha.

Ki TS M Naam mzee Mbaruk.

Ma MK2 M Mimi Mbaruk Ahmadi hapa bin Hassani Kimbeta, mkalbi maarufu. Mimi ninatoa kihadithi kidogo tu. Cha... Bunuwasi sungura. Yaani tunasema sungura na simba. Sungura alitoka porini akasema, 'Mimi nakwenda kukaa jangwani'. Akakaa jangwani kilimani juu huku. Na huku juu ya kilima kuna jiwe, limeinama hivi. Amekaa chini pale. Hewa yote inamjia pale. Sasa simba ametoka huko, anasema, 'Namtafuta njaa huyu njaa kila siku utasikia mtu amekufa kwa njaa, mtu amekufa kwa njaa. Basi mimi nitamtafuta huyu njaa nikamtafunilia mbali. Sasa anapita jangwani, kule anakwenda, anakwenda, anakwenda anatazama huko, anakwenda. Sungura akasema, 'Yule anakuja yule, makusudi akiniona mimi atanitafuna'. Basi akaja mpaka karibu. Sungura akalikamata jiwe. Kwa nguvu sana ametoa mabavu yake. Sasa akamwuliza, 'Babu, babu?' Akaitikia, 'Ee, mbona unakuja huku, unakwenda wapi?' Anasema, 'Ninamtafuta njaa'. 'Unamtafuta njaa?' 'Ee, tena leo nikimwona atashika adhabu yake. Akampa... akapita sasa hivi hapa, njoo. Amepita sasa hivi, njoo, unikatatie mimi nikavutie'.

Ma MK2 M Akasema, 'Nikatie mjukuu wangu'. Akaja pale akamwambia, 'Kaa hapa uzuie jiwe hili kama nilivyozuia mimi.' Basi akaja, 'Mimi sija... upesi'. Akakamatia na yeye akatoa nguvu zake. Simba akamwambia, 'Mimi sasa ninaliacha, naliacha, naliacha'. Simba anazidi... analiacha akatoka. Sungura akatoka akaenda zake. Maji yako moja akapita akila humo siku ya kwanza, siku ya pili, siku ya tatu. Akaja akamchungulia. Anamwona simba ameanza kutoa kibyongo. (kicheko) Ametoa kibyongo. Akamwita, 'Babu'. 'Eeh'. 'Namna gani? Amepita hapa njaa?' 'Sijamwona bado.' Asema, 'Aah, sasa hivi mimi nimekutana naye ebu kwanza. Usi... usiniache mbona linatikisika'. Amekazana tena. Akatoka akaenda zake. Siku ya kwanza, siku ya pili, siku ya tatu alipokuja anamkuta jiwe limemwangukia na yeye akajizame. Alipoanguka jiwe limeota bwana.

Ma XX M Jiwe limeota palepale.

Ma MK2 M Ee, nimamaliza hadithi yangu, imekwisha hapo.

Ki TS M Hadithi ya mwisho sasa.

Ma HB1 M Ya mwisho, naam, ni tamu kidogo. Tipitii mnamfahamu?

Ki TS M Tipitii?

Ma XX M Dudumizi, dudumizi.

Ma HB1 M Aa, tipitipitipi.

Ma XX M Ni litipitila.

Ma HB1 M Wanaitwa tipitipi hawa. Na simba, simba akiweza kuzungumza hakuna kukaa hapo. Sawa. Sasa walishindana hawa. Walikaa pamoja. Wakafanya kamfisi yao. Wewe tipitipi, akamwuliza simba, kwamba wewe...

Ma XX M Aaaaa, hapana.

Ma HB1 M Tipitii akamwuliza simba, 'Babu wewe, mbona una sauti kubwa, kwa nini?' Simba akamwuliza tipitila kusema, 'Aah sauti kubwa ndio mimi nina sauti kubwa nikizungumza nchi itatetema na watu kukimbia.' Tipitila akasema, 'Ndio, wewe una sauti kubwa tu, lakini wewe watu hawakutambui zaidi kuliko mimi.' 'Sasa tushindane vipi?' Simba anasema, 'Tushindane vipi? Utambue, ndio. Mimi nnaweza nikasema Newala.' Tipitii anasema, 'Mimi ninaweza nikasema Newala, lakini Mikindani hii Mtwala.' Watu wakafahamu tipitila huyo. Simba akasema, 'Na mimi ninaweza nikasema Newala'. Hapa Mikindani, Mtwala watu wakafahamu kusema, 'Hapana, twende wakashindane'. Na kumbe kweli tipitila unavyofahamu majogoo na tipitila sawasawa.

Ma HB1 M Wa Newala wakisema kati hapo kati hapo mpaka hapa utamwona yule yule, na saa zao zilezile, nongo. Matipitii hawa... tipitipitipitipi... Basi anajibiwa huyo. Anajibu huyo, anajibu huyo, mpaka mwisho wake. Haya, wakaenda zao Newala. Kwanza simba kusema uuh, uuh, hata mtu wa Nyamba hasikii. 'Umemaliza ...' 'Nimemaliza'. Wakaweka watu wao wawili. Wewe nenda ukasimame na nyamba, usikie sauti ya... Utasikia sauti ya nani? Haya, sauti ya simba na nyamba haikufika. Anaanza tipitii tipitipitipi, tipitipitipi, wanapokeana pokeana mpaka kufika hapa Ntwala Mikindani. Aah, haya turudi sasa kurudi kuulizauliza. Asema mimi sikusikia sauti ya simba, nimesikia sauti yako wewe tu, tipitila. Kumbe ni yeye yule. Simba akifikiri huyu sauti yake mbona ndogo na kadudu haka kadogo kufika Mikindani kweli haka. Hadithi imekwisha. (kicheko)

Edited by TR in October, 1996

DAHE 107

Place: Msimbati, Mtwara

Time: 15.10.1990

Interviewee(s): 1. (SA2), 2. (ST), 3. (SW), 4. (LA), 5. (PS), 6. Unknown (XX)

Interviewer(s): Arvi Hurskainen (AH)

Recorder: Sony Professional

Language: Standard Swahili (Ki), Makonde (Ma)

Topic: 1. Language situation in the district, 2. Differences in the speech of men and women, 3. Explanation why Swahili is spoken in the district, 4. History of the district (Arabs, Portuguese), 5. Building the road, 6. Fishing as an occupation, 6. Personal history of PS, 7. Is Swahili spoken in Mosambique

SIDE A

Ma SA2 M Mimi naitwa Salim Saidi bin Alawi, wa hapa Msimbati.

Ki AH M Umezaliwa wapi?

Ma SA2 M Nimezaliwa hapahapa Msimbati, nimezaliwa mwaka na ishirini na mbili.

Ki AH M Haya, na wewe una... unajiitaje?

Ma SA2 M Mimi?

Ki AH M Ndio.

Ma SA2 M Mimi na... najiita kwa...kwa jina?

Ki AH M Hapana, sio kwa jina, lakini ki... kilugha kwa mfano.

Ma SA2 M Kilugha mimi Makonde.

Ki AH M Makonde. Unasema Makonde tu?

Ma SA2 M Makonde tu.

Ki AH M Haya, ndio, sawasawa. Na wazazi wako wamezaliwa wapi?

Ma SA2 M Wazazi wangu wamezaliwa.. Madimba. Baba yangu amezaliwa Madimba.

Ki AH M Kweli, ndio. Na mama?

Ma SA2 M Mama amezaliwa hapahapa.

Ki AH M Ndio.

Ma SA2 M Msimbati.

Ki AH M Na wote ni Wamakonde?

Ma SA2 M Wote ni Wamakonde.

Ki AH M Je, unajua juu ya historia ya eneo hili, kijiji hiki, kwa jumla? Mambo yale ya zamani kabla ya hata Wajerumani kuingia hapa? Unajua lo lote kuhusu eneo...wakati ule?

Ma SA2 M Navyojua kidogo, kabla ya nani... npata kwa wazee kijiji hiki kilikuwa peke yake, kabla haija... hakijakaliwa na ntu yo yote. Kijiji hiki kilikuwa peke yake kabla haijakaliwa na mtu yo yote. Hawa waliokuja kutoka katika sehemu mablimali kwa makabila, sisi tunakuwa na kabila. Huyu nani Mnyao, huyu kabila nying... huyu labda Mpambe, huyu Mhumbo, katika makabila ya Matumbo. Sasa baada ya kufika hapa kila ntu alichagua sehemu yake akakaa.

Ki AH M Hm, yaani katika kijiji hiki?

Ma SA2 M Katika kijiji hiki. Huyu kaka sehemu yake, ntu wa Pamwe kaka sehemu yake, ntu wa Lihumba akakaa sehemu yake, ntu wa na Marama alikaa sehemu yake, ntu wa Nyang'are alikaa sehemu yake, ntu wa Lwariare alikaa sehemu yake. Hawakukaa pamoja namna hiyo, walikaa mbalimali. Halafu katika kuendelea kuoana na vizazi vilivyoendelea ndio ukapatikanika upanusi nkubwa katika watu kuwa wengi. Kijiji ndio

kikachanganyika tena kuwa kimoja. Lakini walikaa watu mbalimbali. Unapita pori, unafika mahali pa mzee fulani na watoto wake. Unapita pori, unafika mahali pa mzee fulani na watoto wake.

Ki AH M Na pia waliweza kutumia lugha tofauti?

Ma SA2 M Walitumia lugha tafauti. Unasikia? Wengine walikuwa wanasema Kimakonde kidogo hicho hicho. Wewe chanu wepo. Wepo. Ntemachu tongwa cho. Tungachani. Wengine waliofika hapa wamefika Kiswahili kimeshatawala. Wengine wanasema, Ndio... Hao wamesema nini? Mbona si... sisikii? Lakini wale wanaosema 'Utongo wa chani', nao wanasema kuwa wanasema nini, wanasikiana.

Ki AH M Yaani walipozungumza pamoja wale ambao lugha zao za asili zilikuwa tofauti walitumia lugha gani pale walipoonana?

Ma SA2 M Walitumia lugha ya Kimakonde, kwa sababu wote walikuwa ni Wamakonde.

Ki AH M Wote walikuwa Wamakonde. Na wakati ule Kiswahili hawakutumia, au?

Ma SA2 M Wakati ule walikikutia Kiswahili lakini kabla hakijapanuka ni neno moja moja tu. Lakini Swahili pengine kutwa maneno matatu au manne anachanganyisha.

Ki AH M Na katika eneo hili Waswahili wa asili kabisa, je wapo?

Ma SA2 M Waswahili wa asili kabisa?

Ki AH M Ndio, yaani katika maana ile kwamba hawana lugha nyingine kabisa kama ya Kimakonde au lugha nyingine ile, isipokuwa Kiswahili tu?

Ma SA2 M Hakuna lugha nyingine, lugha nyingine, kwa sababu Kimakonde ndio kilileta. Kuna Kimakonde cha wenzetu huko bara. Wanayezungumza mpaka sasa sisi hatusikii. Lakini tunayesema Wamakonde kutokana na lugha lugha walikozaliwa wazazi wetu huko, lakini sisi hapa tuje kizoeni Kiswahili.

Ki AH M Na sasa wakati huo sasa ninyi mkizungumza pamoja, mnatumia lugha gani?

Ma SA2 M Kwa sasa, au?

Ki AH M Ndio.

Ma SA2 M Tunatumia Kiswahili.

Ki AH M Kiswahili. Yaani huko vijijini mnatumia Kiswahili sasa?

Ma SA2 M Ndio.

Ma SA2 M Kuna makundi mawili. Kundi la wanaume tunatumia Kiswahili. Na kundi la... upande wakina mama wanatumia Kimaraba, tunaita Kimaraba.

Ki AH M Sawasawa, swasawa.

Ma SA2 M Lakini wengi wanaume tunatumia Kiswahili. Lakini kinamama wengi wanatumia Kimaraba.

Ki AH M Sasa unaonaje, ni sababu gani kwa nini mnatumia, wanaume wanatumia Kiswahili na wakina mama Kimaraba?

Ma SA2 M Sababu Kiswahili kinakuja kule kukamilisha zaidi katika njia za kusoma.

Ki AH M Hm.

Ma SA2 M Kwa vile siku zile za nyuma hizo watu hawakusoma Kiarabu wala kusoma Kizungu. Kwa hivi ilikuwa ni vigumu. Sasa vitoto vya sasa hivi, kwa makamu nani hii, wengi wote wanaume na wanawake wanatumia Kiswahili. Yaani wakati ule ilikuwa hawakutaka kusoma, basi ilikuwa vigumu kuweza kujua kutumia Kiswahili.

Ki AH M Bila shaka mambo yamebadilika sasa.

Ma SA2 M Ndio.

Ki AH M Na kidogo nimesikia kwamba kulikuwa na watu ambao walitokea kutoka upande wa Msumbiji kuja hapa.

Ma SA2 M Ndiyo, ndio.

Ki AH M Mababu zenu vilevile wametokea huko?

Ma SA2 M Ndio, wengine wametokea huko.

Ki AH M Ndio, ndio. Na kwa upade ule wa Msumbiji, je, wako watu wanaotumia Kiswahili?

Ma SA2 M Upande wa Msumbiji... hakuna wanaotumia Kiswahili. Isipokuwa kwa sasa huwa watakuja kuja huku, wanasikia tu. Lakini pengine kusema anashindwa. Lakini lugha zao tu kwamba kule kuna lugha Kimwani, Kimakua na Kizungu hiki, na kuendelea huko mbele huko, mnashangaa na nini kuendelea mbele. Lakini karibuni humu... na wanatumia zaidi nani wanaita Kimwani.

Ki AH M Sawasawa. Lakini Kimakonde vilevile wanajua?

Ma SA2 M Kimako... Kimakonde kule maana yake Makonde kule sisi hao watu tunaita kama Makonde. Sisisi watu tunaitwa Mawia, ndio Makondi. Wale ndio waliko wengi ndiko walikojua sana.

Ki AH M Ninyi mnaweza kuwasiliana, kwenda huko...

Ma SA2 M Ndio.

Ki AH M Na kuja hapa, hakuna kizuizi?

Ma SA2 M Hakuna kizuizi.

Ki AH M Haya. Mnahitaji kuwa na kitambulisho tu au?

Ma SA2 M Unahitaji kuwa na kiyambulisho, basi, unakwenda. Lugha nyingine kama nyingine sio ngumu sana, tunaweza tukasikilizana, kama wanaita Kimwani.

Ki AH M Ndio.

Ma SA2 M Ee. Mnataka kujaribia kidogo Mwani?

Ki AH M Ee, ndio. Sema kidogo (kicheko). Ndio.

Ma SA2 M Kimwani sisi Kiswahili tunaweza kusema sijui anaweza akasema 'siviji'. Sisi wengine nani... 'sitaki' anaweza kusema 'sisaka'. 'Mimi' anaweza kusema 'umi'. Ee. 'Usifanye hivyo' anasema 'usitende yavi'. 'Usitende yavi, omi sichaka', sasa 'usifanye hivyo, mimi sitaki'.

Ki AH M Tofauti kweli, ndio. Sijui kama ninyi wazee wengine mnapenda kuongeza hapo. Yaani kila mmoja ana... anaweza kuzungumza jinsi anavyotaka. Mnalo la kuongeza? Kwa mfano kuhusu historia. Tafadhali jina kwanza.

MaKi ST M Salim bin Aisam Tandika, Salim bin Aisam Tandika.

Ki AH M Vizuri.

MaKi ST M Fahamu yetu sisi tulimo kila boma au... lina matamko yake. Sisi watu wa huku sote usemaji wao sio wa Kilwa. Kilwa wanasema maneno wanaume na wanawake sawasawa. Nitakuja, nitakwenda, utakapokuja, atakapokuja... ukimwona, ukiniona, utapomwona, ukishamwona. Kilwa wanasema 'mke na mume'. Unasikia? Na sisi hapa 'sasa hivi' mwanamume, 'hambi yambi' mwanamke. Unasikia? Sisi wa huku, 'unatime', anasema mwanamke. Mwanamume 'usikawe'. Huku sisi, unasikia? 'Lyamba na mapema' anasema nke. 'Asubuhi mapema' mwanamume. Tamko letu sisi huku. Unasikia? Kuendelea boma hii ya Mikindani mpaka kufikia Lindi. Unasikia? Kadhalika sisi humu hatusemi Kiswahili. Hii lugha yetu sisi ni Kimwambao. Unasikia? Nitakuja, nitafika, utakuja, atakapokuja, nitakwenda, nitakupa, sikupi, mpe, usimpe, utakapompaa. Sisi, unasikia, yaani watu wa kanda hii, watu wa kanda hii tulio, maana yake sisi yaani tunaitwa Wamwambao. Unasikia?

Ma ST M Kile Kiswahili kama kwa sisi, watu wa Zanzibar tunaambiwa wale wanasema Kiunguja. Na wale watu wa Swahili kule Mombasa wale ndio wanaosema Kiswahili. Unasikia? Wale matamko yao tunasema Kiswahili. Lakini sisi humu hata kama ukamwona namna gani ujanja wake anasema lugha ya Kimwambao. Unasikia? Lakini wanawake 'Naidi hyambihyambi. Pa naida, akaida. Unanne yake.' Sasa wanaume tunasema 'Fuatana naye, usimwache'. Unasikia? Wanawake wanasema 'Hono uka twale'. Sisi wanaume sema 'katwahe'. Unasikia?

Ki AH M Lakini ninyi wanaume mnaposema, ni lugha ya Mwambao?

Ma ST M Ni lugha ya Mwambao. Na tunasikilizana na matamko yale ya wanawake, lakini lugha yetu ya Kimwambao tu. Ukipanda huko juu, hawawezi kusema haya, ni tofauti kuongoza kama tunavyoongoza sisi. Na sisi kadhalika. Tunapofika boma ya Naiwara, hatuwezi kusema kama wasemavyo.

Ki AH M Sawasawa.

Ma ST M Unasikia? Lakini wakisema tunasikia baadhi ya mengine. Na mengine yanatushinda.

Ki AH M Na ile lugha ya wanawake mnayosema ni lugha ipi? Mnaitaje ile lugha?

Ma ST M Ehe, lugha ya wanawake kwamba tunashirikiana nao, yote tunasema ni lugha ya Kimwambao.

Ki AH M Lakini hata hivyo ni tofauti?

Ma ST M Ni tofauti. Lakini tunashirikiana, kwa sababu kitu cha kushirikiana, 'usikawe' basi anajua kama ameniambia nisikawe, lakini yeye... wewe atakuambia 'unatime'. Hivi yule mwanamke wewe mwanamume atakuambia '...unatime', Mnasikia? Na wewe mwanamume yule bibi utamwambia 'usikawe uendako'. Atajua kama ananiambia 'yambiyambi', au 'nнатime'. Unasikia? Sasa tukirudi tena nyuma, 'hambi yambi' anasema nke. Sasa hivi anasema mwanamume.

Ki AH M Ngoja, anasema nini yule mke?

Ma ST M Mwanamke anasema 'ambiyambi unatime'.

Ki AH M Maana yake nini?

Ma ST M Anakuambia... mume ndiyo anasema 'sasa hivi, unakokwenda usikawe'. Nadhani tumeelewana hapo. Hii ndio lugha yetu sisi humu. Baki kulima, ni kama kulima tu vilevile, kutwanga ni kutwanga tu vilevile. Unasikia? Kwenda ni kwenda vilevi... Lakini mwanamke anasema 'kuhwena'. Mke atakuambia 'puhnayapuh' au 'kuhwenako'. Unasikia upesiupesi. Mwanamume anasema 'upesi, unakokwenda usikawe' au 'nenda upesiupesi'. Unasikia? Haya ni maneno yetu sisi humo.

Ki AH M Ndio. Sasa watoto watakulia katika nyumba moja, sio wanaume... wa kike na kiume, wanakaa pamoja. Sio wanajifunza lugha ileile moja?

Ma ST M Ileile moja. Kama tunavyosema sisi wanaume na wanavyosema wanawake. Walioko watoto wadogo wanasema vilevile.

Ki AH M Ndio.

Ma ST M Wakikua kidogo kupata kama miaka sita au saba, basi pale wanaanza kupangukana. Watoto wanawake wanafuatisha matamko ya wanawake. Na watoto wanaume na wanafuatisha matamko ya wanaume.

Ki AH M Kweli. Ni jambo la ajabu. Hili sijasikia mahali pengi. Yaani kama kuna lugha nyingine ambayo wanaweza kutumia kwamba ndio ndio lugha tofauti, wanatumia lugha ile ya asili, hii ndiyo inawezekana. Lakini kama ni lugha ileile, lakini matamshi tofauti.

Ma ST M Lugha ileile. Unasikia? Inatumika kwa kitu kimoja. Wanapokuwa Wamwela wanasema Kimwela tu, mume na nke. Wanapokuwa Wandonde wanasema Kindonde tu, mume na nke. Wanapokuwa Wanyamwezi wanasema Kinyamwezi tu, mume na nke. Wanapokuwa Wahyiao, wanasema Wahyiao tu, mume na nke, nkubwa na ndogo. Wamakua ni hivyo hivyo. Wanyasa ni hivyo hivyo, na kuendelea makabila mengine. Lakini kwa sisi humu Wamwambao, watoto wako namna hii maneno yao namna moja. Baada ya kupata miaka sita saba wanapangukana.

Ki AH M Na imekuwa hivi tangu zamani, au?

Ma ST M Tangu zamani.

Ki AH M Na vipi maeneo mengine hapo vijiji vingine, ni vilevile au ni hapa tu?

Ma ST M Kwa hii kanda ya pwani. Lakini ukifika boma ya Naiwara, utakuta msemo wao mmoja. Na leo, kama alivyosema huyu bwana, kwamba wanachukua usemaji wa pwani, unasogea kwao kama upepo. Wanatamka vivihivi, upesi, upesieupesi, usikawe, sikawi, uende haraka, nitakwenda, kachukue muhogo, atakwenda kuchukua muhogo, lete madafu, ataleta madafu, lete mchele, atakuletea mchele, lete nazi, atakuletea nazi. Mradi sasa haya na fuat.. mpaka kule sasa inafika. Isipokuwa ya wao wale sisi kusema kwa ufasaha wanavyosema wao, sisi hatujui. Kuanza Naiwara, maana yake boma la Naiwara ni la Wamakonde tu. Ukiingia Masasi Wamakua tu. Ukienda Tunduru ni Wahyiao tu.

Ki AH M Naiwara ni Makonde wa milimani, au?

Ma ST M Milimani.

Ki AH M Sio Malaba?

Ma ST M A-a, hapana. Malaba ni katikati hii. Na hii Malaba sio lugha maalum.

Ki AH M Ndio.

Ma ST M Ee.

Ki AH M Ndio, ndio. Sawasawa. Asante sana. Sijui mwenyekiti ungependelea sasa kuongeza?

Ma SW M Kwa kuongeza...

Ki AH M Taja jina.

Ma SW M Ah, asante. Mimi naitwa Salum Waziri.

Ki AH M Sema upya. Tafadhali sema upya.

Ma SM M Niseme upya?

Ma SM M Mimi Salum Waziri.

Ki AH M Endelea.

Ma SW M Naishi kijiji cha Msimbati. Ni mzaliwa wa Msimbati. Kutokana na historia hiyo waliyozungumza wazee hao hapa sawasawa mazungumzo waliyozungumza. Kutokana na maelezo yetu tuliyoelezana hapa, Kiswahili sisi ni lugha tuliyoipata, katika kihistoria tumeipata kutoka kwa watu wa zamani, tulimikutia. Sisi ... watu wanazungumza Kiswahili. Lakini mimi nipo sijasikiasikia tena nikasema hiki Kiswahili, kama alivyo... alivyozungumza mzee hapa. Anasema Kiswahili kimekuja kutokana Waswahili, watu wa Mombasa, ndio walioleta Kiswahili hiki. Sasa sisi... kihis...kihistoria, mara nyingi sana ilikuwa tunatumia lugha moja. Tulikuwa tunatumia lugha moja. Twala - twala...sote, cheka, nhyeka - hyeka. Unajua neno hili?

Ki AH M Sawa.

Ma SW M Hwena, hwena.

Ki AH M Na lugha hii ni lugha gani?

Ma SW M Ni lugha hii ya Kimakonde, Kimalaba hiki, tutakachotumia sisi katika... Unaona? Sasa katika kuishiishi walipofika wale Waswahili, maana yake ni Waswahili, walikuja wa kwanza ni Waarabu waliobadili Kiswahili, kutufanya sisi tukapepesuka. Walipofika Waarabu wametuambia 'Wewe chukua', lakini sisi tulikuwa tunasema 'Twala'. Tukikaa tumeelewana wanawake wanaume. Sasa wao walipofika asema 'Ah', Mmakonde mnaharibu Kiswahili. Hamjui Kiswahili, sema 'chukua'. Sasa sisi tukahama. Sasa wepesi kuhama ikawa na ume, kwa sababu sisi ndio tulikuwa tunatembea nao, Waarabu. Wanatuhamishahamisha kulee. Basi kwa lugha hii... imetuenea sisi sana...Lakini hawa wenzetu wanawake, kwa sababu tulikuwa tunawaacha hapa basi wale... lugha yet... ngh... lugha yetu ile tuliyokuwa nayo basi wanayo mpaka sasa hivi.

Ki AH M Je, ni vipi, wanawake zaidi wanakaaa hapahapa kijijini na ninyi wanaume mnatembeatembea baharini na mnakwenda hata vijiji vingine na mijini. Ni kweli? Ninyi mnasafiri sana?

Ma SW M Ee, tunasafiri sana.

Ki AH M Je, hii inaweza kuathiri lugha ile iwe tofauti kidogo, wanaume ndio wanakwendakwenda sana na wanawake wanakaa hapa zaidi?

Ma SW M Ee.

Ki AH M Unafikiri ni hivyo?

Ma SW M Ni kama kwa mfano kwa kuongeza, ni kama mimi hapo ninapotoka ninaweza kutoka na kwenda Uingereza, au nikienda Uitali, au nikienda huku Finland. Sasa mimi ninakuta wanazungumza Kiingereza kule. Sasa ninakaa mwa... mwaka mmoja, sasa nime... nimeshapata nini, nimeshapata Kiingereza, au nimepata Kifinland, au Kinorway, nimeshamchukua. Sasa mimi ninapofika hapa ninajiamini tu. Kama atakuja Mnor... Mnorway, Mnorway kuja hapa, mimi nitazungumza naye. Sasa ninapotoka pale nikienda kule kwa mama basi nitazungumza kilekile.

Ki AH M Ndio. Sawasawa.

Ma SW M Mke wangu ni yangu 'nipe'. Sasa ninamwambia kwa Kiswahili mke wangu 'nipe'. 'Hitaki', anasema, kwa Kiswahili 'sitaki'. Mnaona hapa. Lakini... toka zamani wanasema 'nipe', 'nipe', 'hitaki', 'hitaki'. Tulivyoanza huko.

Ki AH M Ndio, sawasawa.

Ma SW M Lakini nyakati za katikati hapa tulitaka kwenda ndio sisi tumepepesuka kwenda kule... Lakini lugha safi ni ile moja tunavyozungumza kama mnavyofahamu Makua, maana Wamakua wanasema 'Kinorwa'. Mwananke anasema 'Kinorwa'. Mwananke anasema 'Kin...' mume anasema 'Kinorwa' na nke anasema 'Kinorwa'.

Ki AH M Kinorwa ni nini?

Ma SW M 'Kinorwa' ni 'kwenda'.

Ki AH M Kwenda.

Ma SW M Wale wanasema namna moja tu. Unasikia? Mroe, mroe.

Ki AH M Mroe ni nini?

Ma SW M 'Mroe' Makua wanasema 'Njoo'.

Ki AH M Haya.

Ma SW M Na mwanamu... mwananke anasema 'Njoo'. Sawasawa vile na 'Mroe'. 'Mpani', mwananke; na mwanaume anasema vilevile 'mpani', yaani ni nyumbani. Kinorwa 'mpani'.

Ki AH M Ndio.

Ma SW M Twende nyumbani. Na mwananke... mwanaume anasema vilevile 'twende nyumbani'. Kama alivyozungumza mzee huyo kutokana na jamaa wa Msumbiji. Jamaa wa Msumbiji wanasema, 'Omi siyebu'. Na mwananke... mwanamume na mwananke wanasema 'omi siyebu', yaani 'sitaki'. Unakuta mwanamume anasema 'siyebu', na mwananke 'siyebu'. 'Kontaki nani', yaani wanasema 'kwa nini', mwanaume anasema 'kwa nini', 'kontaki nani'. Yaani kwa Kiswahili 'kwa nini'. Na mume alisema 'kwa nini'.

Ma SW M Sasa sisi hapa ikawa ndio tumepoteapotea, kwa maana Kiswahili chetu huku sisi sana tumepoteapotea katika kusafiri. Na hiki kimekuja na wale jamaa wa... una... baadhi ya watu walitoka hapa. Wamesafiri sehemu za huko Lamu, wengine Mombasa, wengine... Sasa katika kurudi kwao kuja huku basi walipata Kiswahili. Sasa sisi tulikuwa na lugha hii, kwa... lugha hii sio mzuri sisi kusema ya Kiswahili. Wapochani sasa tuko katika ni Wajuba. Sasa unakuta wao wanazungumza vizuri, wewe nini bwana Fallal, yahye nini bwana wewe bwana wewe. Sasa unaposema 'Wepochani unaoneka... aah.

Ki AH M Ndio.

Ma SW M Ee.

Ki AH M Lakini wana... kuna Kiswahili cha aina mbalimbali, na hiyo ndiyo mnayosema ni... ni lugha nzuri tu. Labda inatofautiana kidogo na lugha zile nyingine za Kiswahili, lakini ni lugha ya watu. Na mnasema mfululizo kama nini.

Ma SW M Ehee.

Ki AH M Hamna taabu yo yote.

Ma SW M Basi hii kwa sisi kwa kweli humu yetu ndio hii Wepochani. Lakini Kiswahili kwetu sisi kimekujakuja... kama mnavyofahamu, kama tuseme kama Kiingereza, maanake mtu anaweza kuzungumza kijana wa sasa... unaweza... Nenda Bwana ee. Sasa Mwingereza anasema 'Halo'. Unaona. 'I am coming now'. Sasa mimi, ah, mbona mimi nimesema Kiswahili wewe unanipa haya mimi sielewi. Unaona sasa? Sasa... mtu mwingine anakuta ni mtu wa sasa kama mzee huyu au mwingine au mimi, ukisema Kiswahili kuamwambia mtu wa zamani huyu, lakini sema Kiingereza. Ah, naspeak Kiingereza. Basi, sasa ime... hivi Kiswahili kinahama. Isipokuwa kama ulivyokuja wewe hapa ulivyokuja mwalimu kutafuta Kiswah... kutafuta lugha. Unaona? Lakini Kiswahili ujue sasa inahama kwetu. Ni haya waliyopata wazee hao lakini mbele utakwenda. Kama utakuja mwaka mwingine utakuja kimehama Kiswahili. Tuna watu wengi sana wanataka Kiingereza. Hivi kama unge...

Ki AH M Watu wa hapahapa?

Ma SW M Watu wa hapahapa, Kiingereza tu, basi.

Ki AH M Lakini Kiswahili si lugha ya taifa?

Ma SW M Lugha ya taifa hawaitaki, lugha hii mchafu.

Ki AH M Nani anasema hivi?

Ma SW M Watu wa sasa.

Ki AH M Wakina nani?

Ma SW M Wadogo wadogo, vijana vijana.

Ki AH M A-a, vijana hawa hawajui lo lote. Hawajui lo lote kabisa. Ujue bwana kwamba Kiswahili kitaenea, kitaimarika, kitakuwa lugha ambayo inatumiwa katika nchi nyingi za Afrika. Hujui hilo?

Ma SW M Sawasawa.

Ki AH M Unaona mimi ni mgeni labda, lakini nadhani kwamba hapo nitakuwa nabii, nitatabiri jambo hili.

Ma SW M Haya. Basi mimi...

Ki AH M Maana mimi nina matumaini makubwa sana katika kuenea kwa Kiswahili.

Ma SW M Ndivyo, ehee.

Ki AH M Kwa hiyo tukisema kwamba watu wote hapo wataanza kusema kiingereza, ninyi mtakuwa watu wa pekee hapa Tanzania, lakini wengine wanatumia Kiswahili.

Ma SW M Basi watu wanataka sana Kiingereza. Sasa kama ungalikuwa mfanya utafiti makusudi... hata... Makonde kuwa Kiswahili, basi sisi tungependa sana. Na hapa bahati yako umekuja kwa sababu umepata wazee. Kama ungechukua vijana, hivi Kiswahili hungalipatapata.

Ki AH M Vijana hatutaki, maana wao wanachafua kila kitu. Lakini ni upuzi ule. Ni tofauti kabisa kati ya mambo mawili, yaani kati ya kujua lugha moja na lugha mbili na kuzichanganya kabisa, na kati ya kuhifadhi ziwe tofauti. Mnaona vijana mara nyingi wanatumia Kiingereza, wanachanganya, wanaokota neno moja moja kutoka Kiingereza, ili waionyeshe kwamba ndio wamesoma. Kwa hiyo lugha inaharibika.

Ki AH M Kwa hiyo mimi sikatai kwamba wasisome wajue Kiingereza. Ndio lazima, maana hapio ndipo tunaweza kuwasiliana na nchi nyingine. Mimi nimesoma sana lugha pia na najua maana yake. Lakini lugha yangu, mimi katika nchi yangu ni lugha ambayo naipenda sana katika nchi yetu, Kifini, lugha halisi ambayo tumeunda kwa ajili ya taifa letu. Sasa ipo. Tuliitaka kutawaliwa na Wasweden, tumetaka kutawaliwa na

Warusi. Wote walitaka kuingiza lugha zao. Kusema kwamba Kifini ni lugha ya kishenzi. Sisi tumesema 'hapana'.

Ma SW M Ndio sababu mmepakana nao wale.

Ki AH M Sasa hakuna asemaye lo lote. Imekwenda mpaka juu. Tunaheshimu lugha hii. Ndivyo itakavyokuwa na Kiswahili. Sasa ningependa kujua sasa kama mna habari zo zote kuhusu Waarabu, yaani enzi zile za zamani hata kabla ya... kabla ya Wajerumani kuingia katika eneo hili la Tanzania? Labda hapa hasa Wajerumani hawakuingia, au kulikuwa na dalili yo yote kwamba Wajerumani wangaliingia hapa hasa, kwenye kijiji hiki? Hapana? Je, Waarabu waliwahi kufika katika eneo hili? Mna habari yo yote, hapo zamani?

Ma SW M Hamna.

Ma XX M Huyu mmojawapo wa Wamakonde kutoka Msumbiji, Mseto, bwana na...

Ki AH M Sawasawa.

Ma XX M Karibuni. Kiti kipo hapo.

Ma SW M Hapa Waarabu hawakuwahi kuja hapa waka... chukua kwa sababu wao barabara tu ya kupanda huko milimani kufuata kununua watumwa. Humu hawakuweza kukaa kwa sababu ilikuwa hawakupatikana watumwa.

Ki AH M Hm, yaani wao ndio walikuja kwa ajili ya kupata watumwa.

Ma SW M Ndio. Sasa humu hawakupatikana, kwa hivyo hawakudumu humu. Ili wao wamewapatia kwa juu juu huko juu ya nini... Wamepanda mpaka sehemu mbali bara huko mpaka nani huko Songea kwa watu, ndio walikojaribu kuwa... wapata nani, lakini humu Mwambao mwote hawakuweza kumpata ntu kwa kununua Waarabu.

Ki AH M Ndio. Na katika eneo hili watumwa hawakuchukuliwa. Kabisa. Na vipi upande wa Msumbiji, huko upande wa Msumbiji, au? Mna habari?

Ma SW M Juu ya nini, hawa Waarabu?

Ki AH M Ndio, kama wao waliwahi kwenda huko?

Ma SW M Huko mnapata waliwahi watu wake kufika, sehemu kama... kuna sehemu hizo walizoweza kukaa kule kama eneo mbali kabisa kule na kuna sehemu hapa... panaitwa nini sijui hapo, mpaka sasa wanakaa watoto wao wengi kabisa. Hapo Waarabu walikaa... walipita za juu. Maana yake ukienda kueleza kwa kutokea nani hapa Komoro ni rais anakufikia. Kwa hiyo alipitia zile.

Ki AH M Hm. Habari za Wareno, je, Wareno waliwahi kupita hapa au kuonekana kwa wakati wo wote? Bila shaka ni muda mrefu tu sana tangu wakati ule lakini mna habari yo yote?

Ma SW M Wareno katika muda mrefu walipitia hapa. Hata hii ilikuwa ni yao hii mpaka kuweka kuna huko inaitwa huko Jiwe la Mzungu, kupita Lindi. Mbele huko ndio waliweka mpaka humo Lenu. Alitawala sehemu hii Lenu. Aliyekuja kumtoa Mreno nanii... ni Mjermani.

Ki AH M Ndio, ndio. Kwa hiyo ninyi mmeishi hapa katika aina fulani ya usalama kwamba hamkupata msukosuko wo wote hapa. Na njia yenu kuu ile ya kuishi ni ipi? Uvuvi?

Ma SW M Uvuvi.

Ki AH M Na kazi nyinginezo?

Ma SW M Kazi nyingine ni kulima.

Ki AH M Kulima. Kulima nini? Mazao gani?

Ma SW M Mazao ya vyakula tu.

Ki AH M Kama?

Ma SW M Kama mtama, mpunga, na karibuni hii mazao ya biashara yamelimwa karibuni katika huyuhuyu Mwingereza huyu. Maana siku za nyuma walipokaa... wazee waliopo wakati wa Wajerumani hawakuweko habari za korosho... zao hili, hawakulihimiza wale. Habari za korosho ilihimizwa katika kuja kwa Mwingereza.

Ki AH M Ndio, ndio. Kumbe ni... Na siku hizi nimeona kwamba wana mashamba ya chumvi huko.

Ma SW M Ndio.

Ki AH M Hii pia ilikuwepo?

Ma SW M Haikuwepo, hata. Iliingia juzijuzi tu. Ee, hata tulipoanza kudai nchi yetu haikuwepo shamba hata moja.

Ki AH M Kweli. Serikali ndiye... ndiyo iliyoanza kuleta kazi hiyo hapa?

Ma SW M Ndiyo. Ilianzia kule Lindi, ndio iliko tumeanza kuiona kwetu sisi. Na halafu ilikuwa Lindi ikahama ikaja hapo nani Ufukoni hapo karibu ya... kulekule kabla ya Ntwala kule. Ndio wakaweka shamba hapo kabla mtu wingine hajachukua Mswahili yo yote wao walichukua. Hapo walipoendelea kwenda ilipo.. walipomaliza ...mifuko yote kuchukua watu mashambani kwa ajili ya chumvi.

SIDE B

Ma SA2 M Salim Saidi Alawi.

Ki AH M Endelea.

Ma SA2 M Mambo ninayoongeza kuhusu historia tuliyoishi nchi hii, tulikuwa na taabu kubwa sana habari ya usafiri. Hawa wazee wetu walipokuja hapa, ilikuwa nchi hii haiingii gari. Watu walikuwa nasafiri kwenda mm... Mikindani kabla ya Ntwara wanayo wakati huo. Ilikuwa inakwenda kwa mitumbwi tu, au kwa njia za miguu. Sisi tulipokaa tukaona mambo haya mpaka lini. Karibuni hivi walipoanza baba wa taifa kudai nchi huu, tukaona labda itakuja maendeleo. Mwaka na hamsini na nne tukaona kwamba sisi tujitoleze sisi wenyewe tu, tukate pori tulime barabara hii mpaka kule kuingilia kule. Kwa hivi tukalima barabara hii sisi wenyewe bila pesa za kutoka wapi. Tuka... tukawa tunachimbua visiki mpaka kufikia katika barabara ile inayokwenda Ruvuma. Na tukafahamisha serikali na sisi tumejaribu sijui inaweza ikapita gari au inaweza kuwa namna gani. Wakajaribu kupitisha gari mpaka ikafika hapa.

Ma SA2 M Basi, tukaona tena njia hii ya kusafiri na gari inafaa. Tulipoambiwa serikali ndio tena wao... nao pia wanaitumia lakini hawakutumia nsaada wo wote. Haikupatikana nsaada wake njia hii mpaka kuanza vita vya Msumbiji. Katika kuanza vita vya Msumbiji ndio tena wakaja kutengeneza barabara hii, kwa sababu sisi ya kujilinda. Kwa mujibu wa kujenga barabara mpaka kufika hapa pwani hapa na kutuletea silaha tena, ili tuweze kujifunza. Lakini wakati huo kabla ya kukumbuka sisi wenyewe kwamba tuwe na barabara sijui ilikuwa ndio lini tung... mpaka hatujapata barabara. Hii barabara hii tumejitolea sisi wenyewe, tukakata pori, mpaka tukafikisha kule Madimba. Tulikuwa tunalima kwa vipande kwa shauri ya wenzetu, sisi tulilima

kutoka hapa mpaka Ngoji. Wenzetu wa Ngoji walilima pale mpaka kufikia Madimba kule, katika pacha ile. Ee.

Ki AH M Na sasa barabara ipo.

Ma SA2 M Sasa barabara ipo, lakini mpaka sasa iko hivihivi tu ya sisi wenyewe. Kwa sababu ukati wa kifuko inawezekana gari zisipite kama mashimo... Kwa hivyo kitu kilicho tuna... tuna nini... sisi kama ilikuwa ndio wewe uliokuja ndio tunakuomba kwamba shida yetu sisi hasa ni barabara. Nchi hii haisafiriki wakati wa masika.

Ki AH M Na basi lipo linalosafirisha watu?

Ma SA2 M Hatuna basi. Maana wale waliokuwa na basi walisema, 'Hatuwezi kupeleka basi njia hii, kwa sababu njia mbaya, ina mashimo na hivi. Yaani wametumia mpaka sasa, hata mabasi yenyewe sasa hao hawana vile, kwa sababu bei zimepanda juujuu za kununulia mabasi. Sasa wanashindwa. Kwa hiyo sisi tunakwenda kwa taabu sana. Watu watakapotaka Ntwara aidha hutumia miguu au hii Mikokoteni magari yetu matipa ya kupakia magunia haya, basi. Kama tuna moja hapa kijiji, ikiwepo hapa ndio inatusaidia. Lakini kitu cha usafiri ndio tulichokuwa na taabu sana.

Ki AH M Inaonekana kweli. Lakini kwa njia ya bahari mnaweza kwenda Mtwara, sio?

Ma SA2 M Kwa njia ya bahari tunaweza kwenda Ntwara kwa njia za mitumbwi. Lakini unafahamu mtumbwi wa tanga, basi wengine wanaweza kuchukua siku tatu au siku nne kama upepo mbaya. Lakini mahali pafupi sana kama upepo mzuri, basi mwendo wa masaa manne tu.

Ki AH M Kweli.

Ma SA2 M Ee. Lakini unaweza kuchafukia upepo hapa. Vizuri tulikuweco tulipata siku za nyuma, tulikuwa na boti. Ilikuwa ndogo tu kama za kuvulia hivi, ooh ilikuwa inasaidia. Kama ikawa na boti hapa ni rahisi sana Ntwara, mahali padogo sana.

Ki AH M Haya, nashukuru sana. Je, umemaliza?

Ma SA2 M Ee.

Ki AH M Haya, Ninyi wengine, je?

Ma SW M Hakuna, bwana ameeleza.

Ki AH M Sasa kidogo kama... kati yenu kuna wavuvi hata mmoja, ambaye anavua samaki?

Ma SA2 M Wapo. Ndio kazi yetu.

Ki AH M Kwa kuwa mimi ni mvuvi halisi katika nchi yangu.

Ma SW M Wewe?

Ki AH M Ndio mimi. Kila wakati ndio navua samaki. Ndio. Kwa hiyo nengependa kidogo kujua mbinu zile ambazo mnazitumia katika kuvua samaki katika eneo hili. Nani?

Ma SW M Mimi ndimi.

Ki AH M Basi.

Ma SA2 M Sema jina lako.

Ma SW M Mimi Salum Waziri, mzaliwa wa Msimbati. Mimi ni mvuvi wa samaki toka nikaanza kuzaliwa. Kazi yangu ni uvuvi na kulima. Tatizo nililo nalo katika uvuvi vifaa. Kwa sababu tunatumia vifaa vile vya toka zamani. Sababu sisi tulikuwa na vifaa vya duniduni, kwa sababu kuna Kiswahili wanaita duni, ni kitu kisichofaafaa. Unapata kamba, katani. Katani unafumua, unatoa... unatoa taka, unamaliza una.. unasokota, unasuka mavu. Basi unapata kipande, unakwenda baharini unasengeza sengeza, unapata samaki.

Ki AH M Unasuka wavu?

Ma SW M Unasuka wavu. Sasa tukiendelea tuko na kazi ilikuwa kubwa sana, kusokota kazi. Tukapata taili za motokaa. Ndani mule kuna waya... uzi ule. Tunafunua tunatoa taka zile, halafu tinasoka wavu, tunakwenda kuvua.

Ki AH M Ahaa, tairi zile za motokaa?

Ma SW M Za motokaa. Tunapata uzi ule ule ndani. Tukatumia huo kwa kujisaidia, tukenda, tukashindwa, kwa sababu hali yenyewe ya chini. Hasa mimi nikashindwa hali ya chini. Kupata taili moja ni kazi kubwa. Sasa ikabidi nini... ikabidi kutafuta kamba yo yote ya uzi wa gunia, basi ninazo. Nasuka tu hivihivi. Basi unakwenda, siku tano siku sita umekwisha unatupa. Na kwa siku tano unatupa. Basi, kazi ikawa hivi. Sasa kisha kubakia kwa kipindi hiki tulicho nacho sasa, tunatumia, kuna kamba zile za nyavu zile za nailon zinatoka... Sasa zile tunazitumia, zinakuja, tunanunua, basi tunavulia.

Ki AH M Zinaletwa mpaka hapa?

Ma SW M Zinaletwa mpaka hapa. Lakini katika kuletwa kwake, zina taabu kupatikana kwake. Na muda wa kwanza ilikuwa tunanunua, mwavu mmoja tunanunua shilingi kumi na tano mpaka ishirini, zile nyavu ndogo. Sasa zimeruka zimefika mmoja shilingi mia tano. Sasa tumeshindwa katika hayo. Sasa ndio tumeishi... mimi naweza... mimi nimekaa tu. Sasa kinachonisaidia ni mvuvi wa mshipi. Unajua mshipi?

Ki AH M Ndio. Tena nimefanya sana. Hata Unguja siku nzima nimevua huko kwa mshipi, Unguja kusini, kwa mtumbwi.

Ma SW M Sasa tunapata mshipi, unatengeneza kamba. Basi unaofanya kamba moja... maana yake kamba moja kuliko nyingi na kamba moja ni kwa nafuu nafuu. Unatengeneza kamba kuwa ndefu, halafu unachukua ndoana, unafunga, basi unakwenda baharini kwenda kujisaidia. Hio ni kazi ninayofanya mimi. Sina boti, isipokuwa natumia mtumbwi.

Ki AH M Na tanga vilevile?

Ma SW M Na tanga. Hii ndio kazi ninayotumia mimi.

Ki AH M Kuvua mnavua zaidi kwa upande wa mto huo wa Ruvuma, au huko baharini kabisa?

Ma SW M Mto wa Ruvuma ndio tunakokwenda.

Ki AH M Huu ni nzuri zaidi?

Ma SW M Ee.

Ki AH M Ni samaki za aina gani mnapata?

Ma SW M Samaki, yuko samaki anaitwa... Kuna samaki anaitwa ndamaso, kuna samaki anaitwa jolwe, kuna samaki anayeitwa lapinga, kuna samaki anayeitwa mlavifi, kuna samaki anayeitwa kungu, kuna samaki anayeitwa changu, kuna samaki anayeitwa agamu, kuna samaki anayeitwa liyonga, yaani ni moja. Kuna samaki anayeitwa papa. Kuna samaki anayeitwa taa. ... Hao ndio tunaovua.

Ki AH M Na zipi zile nzuri kuliko nyingine? SW Samaki nzuri ni jolwe, kolekole wale. Hao ndio wazuri sana. Na changu.

Ki AH M Changu vilevile. Changu zinapatikana kwa wingi kidogo?

Ma SW M Zinapatikana kwa wingi.

Ki AH M Mimi napenda changu sana.

Ma SA2 M Mimi nataka kuongezea. Mimi naitwa Salim Saidi Alawi, mzaliwa wa hapa Msimbati. Sisi kwa upande huu wa kivuvi hasa kwa hapa Msimbati, leo hapa, kabla ya... tumefurahi sana kustamka kwamba wewe ni mtu wa nani... Finland. Na ndiko mahali tunakopata misaada sana. Na kisiwa hiki tunataja mambo ya kulima lakini hakuna kitu kinachopatikana nani mapato makubwa ya kuweza kutosha kama ni uvuvi. Lakini hatuna vifaa vyo vyote vya kuvulia. Hatuna vifaa vyo vyote vya kuvulia. Wenzetu mlioendelea mnavua na meli mnavua na nini? Kama unafanya... unapata utajiri mkubwa sana, lakini tunashindikana hii anavyoeleza ni vinyago vya kuweka begani.

Ma SA2 M Wengine wanakwenda kuvua kwa ntumbwi tu hivihivi. Hakuna nini hii. Lakini huku samaki ni bikira. Bikira unajua? Kitu ambapo hakijatumika. Samaki wapo tele sana, kwa sababu ni mavuvi madogo tu. Huko kunako... kunavuliwa mitego... na sisi tumpate samaki. Lakini ... kwa sababu hakuna mitego mikubwa ya kuweza kuchukua samaki. Kwa hivyo imani yetu kubwa tunakueleza wewe mwalimu uliyokuja kuleta hayo, ili utufanyie nsaada nkubwa sana. Kisiwa hiki cha Msimbati ili muwe muwafikirie ili kwamba wao hasa serikali au marafiki kama ninyi mkataka kutusaidia, ingekuwa sana sisi mtupatie zana za uvuvi, na kutupa mafunzo kamili ya uvuvi. Tungekuwa katika raha sana.

Ki AH M Unaona sisi huko tuna maziwa mengi sana, yaani kila mahali kuna maziwa tu, pia bahari ipo. Kwa hiyo karibu kila mmoja anajua kuvua samaki. Kwa hiyo ni kazi mojawapo kubwa kabisa huko kwetu. Na sijui kama mmewahi kuona kuna boti ya Wafini wanakuja mara nyingine hapa kuvua samaki.

Ma SA2 M Ndio. Wanawapata wengi, ndio maana tumepata tamaa, wakawa na tufanyie sisi kutupa mafundi na kutupatia vyombo vile, tungekuwa rafiki wa kudumu sana.

Ki AH M Basi, tutawaelezea tu. Tutawaelezea. Na huenda Mungu akitujalia wakati siku fulani ndio mambo yataendelea.

Ma SA2 M Ndio bwana.

Ma SW M Mimi Salum Waziri, mzaliwa wa Msimbati. Wewe ni mvuvi mwenzangu. Kama ni mvuvi mwenzangu, kwa sababu mambo ya uvuvi unayajua. Mvuvi kazi yake ni kutaabika. Kwa sababu unapokwenda baharini, unachukua chombo kidogo na unapokwenda... mara nyingine unapinduka, unaogeleaaa... hapo ukafika kesho yake pengine ukapotea, watu tunapotea. Kwa sababu vifaa vyetu tunavyotumia ni vidogo sana. Sasa ninachokiomba, kama kuna uwezekano, kwa haya tunayozungumza hapa, kama serikali, tunaomba, itufanyie nsaada vile vifaa vya kutega vya kutosha kidogo. Kwa sab... bahari hii... na sisi ni nkubwa sana.

Ki AH M Yaani vifaa vya kutegea?

Ma SW M Ehee, vya kutegea.

Ki AH M Vipi vyombo, upande wa vyombo? Lakini vyombo vya kusafiri?

Ma SW M Ya kusafiri, ee... Kwa sababu bahari kubwa sana. Kama tuseme mwaka jana walikuja jamaa wa Finlandi. Nafikiri walikuja hapo, kwa sababu walitumia meli. Zile meli sisi tulizona sisi tunatokea hivi. Sisi tukaogopa zile mpaka pembeni pwani. Zikakona hapo zikaenda hivi. Sisi tulisema meli tu za wasafiri. Nafikiri

tulifanya mpango hapa nafikiri silaha wa kuzitoa pwani wa kuchungiachungia. Kwa sababu hatujaona mambo yale. Sisi tumezoea mtumbwi ndio kutu... kidogo kidogo. Lakini tuliona meli tatu zinakuja.

Ki AH M Meli tatu kweli?

Ma SW M Ee, tatu.

Ki AH M Wao wana moja tu. Leo asubuhi nalisikia mara ya kwanza kutoka rafiki yangu mwingine mmojawapo huko Mtwara. Wana meli kama mita 10 hivi. Sio chuma, ni aina ile ya plastiki. Na mashine kubwa. Hio ndio inakuja hapa.

Ma SW M Ndio inakujakuja hapa.

Ki AH M Zile nyingine ni za nani, sijui. Lakini wanasema kwamba samaki ndio wengi hapa.

Ma SW M Wengi sana. Sasa ndio hio, na wewe kama mvuvi mwenzao nataka kunisaidie.

Ki AH M Ee, ndio, tuna... tunapeleka habari na maana kuna mambo ambayo kutoka huko Finland kwetu ndiyo imefanyika kwa misaada ya kuvulia samaki hapa Tanzania. Misaada imeshafanyika tayari. Kwa hiyo kama mnaeleza habari hizi, kwamba samaki maadamu samaki wakiwepo mahali fulani, pana nafasi ya kufanya kazi pale. Kama samaki hakuna, hakuna haja ya kuleta vyombo.

Ma SW M Na kwa kuongeza, maana yake mtu wa bara anasaidia upanga, jembe, shoka, yule anasaidiwa kule. Lakini mtu wa pwani nsaada wake ukitaka umwelewe sana ni mwavu. Unaona wenziwe wote wanadumu hapa kama ni la mzee huyu. Ni nyavu tu inayodumu sisi. Iwe hapa kama ungesema nyavu zimekuja nafikiri sisi tungalichukua leo kukubeba kwa kukutembeza juu namna hii.

Ki AH M Yaani nyavu zile zenyewe unazosema unaweka begani unapokwenda, ni zile za kutupia au zile za kutega?

Ma SW M Hapana, zaidi kutega tu.

Ki AH M Ndio, kutega. Ni kama urefu gani?

Ma SW M Ni kipande tu kama nyumbani pale, basi.

Ki AH M Na kimo cha kwenda juu?

Ma SW M Kiasi tu pata hivi tu, basi.

Ma SA2 M Kiasi ya kupata hivi au..

Ki AH M Mita mbili na... au mita mbili na nusu. Hizo ndizo nyavu ambazo mimi pia natumia sana. Naweka kumi, kumi na tano mfululizo na kupata samaki wengi.

Ma SW M Ndio mnepata, kwa sababu... sasa ndio hizi ndio sisi tunaomba sana. Hiki kiwe serikali ipitie macho sana swala hili. Kwa sababu sisi tunapoletwa majembe au panga au kitu gani, kwa sababu tuna... vitu hivi. Maana yake mtu wa pwani toka zamani ni asili yake ni uvuvi. Ukipata kitu kile, basi, sisi tumeshafaidiwa.

Ki AH M Yaani taabu kubwa zaidi ni kupata nyavu za kutosha.

Ma SW M Ehee, nyavu za kutosha.

Ki AH M Ndio. Mnasema kwamba wavu mmoja bei yake ni sikuhizi shilingi ngapi? Wavu mmoja.

Ma SW M Kwa sababu hizi nyavu tuna... zitumia sasa, kwa kipindi hiki, zamani tulikuwa tunatumia nyavu ndogo, kama ya sehemu ya hapo.

Ki AH M Ndio.

Ma SW M Basi, tulikuwa tunapata samaki. Lakini sasa tumebadilika, kwa sababu samaki wameishaondoka haiko baharini sana. Tunatumia mwavu upana wake mpaka nyumba ile. Hizo ndizo unapata samaki sasa.

Ki AH M Ndio, ndio.

Ma SW M Kubwa.

Ma SA2 M Bei kwa sasa hivi, kwa sababu kwetu hakuna nyavu. Nyavu zinatoka Msumbiji mpaka tunaweza kupata sisi kule. Sasa, Msumbiji kwa kuwa fedha yao wenzetu imeanguka zaidi. Halafu zinakuwa ghali kabisa hazitanunulika. Kwa hivyo tunavyotazamia sisi kupata nyavu ni huku. Lakini kwetu kwa kuwa hakuna ukiulizia... labda Tanga sijui. Wameweka nani wapi sijui nani Bagamoyo sijui. Kwa hivyo kwetu hakuna kabisa kupata mwavu.

Ki AH M Yaani sehemu za Mtwara hakuna nyavu?

Ma SA2 M Hata mahali pamoja. Hata pamoja.

Ki AH M Kweli?

Ma SA2 M Toka hapa... Mwaka juzi ilikuwa waliweka Lindi pale palipatikana wavu. Sasa hakuna. Nasikia wako huko Bagamoyo. Mbali sana Bagamoyo.

Ki AH M Unaona, bahari ni kubwa. Bila shaka nyavu zinatakiwa mahali pengi. Huenda wanachukua hukohuko, labda hazifiki mpaka hapa kusini.

Ma SA2 M Mimi nataka kuuliza kitu kimoja.

Ki AH M Ndio.

Ma SA2 M Mimi naitwa Salim Saidi bin Alawi, hapa Msimbati. Kuna kitu kimoja... ni ile yaani sisi ya bahari zinitwa majongozi. Unajua jongoo, au makojoyo?

Ki AH M Ndio.

Ma SA2 M Unajua. Sasa, pia yanashindikana sasa kupata sisi hapo, kwa sababu hatuna utaalumu, hatuna nguvu ya kupatia. Nguvu yake ni nini? Kama ilikuwa inapatikana ile ges ya kuweka ngongoni na unazama chini. Basi ile mpaka kuondoka wewe kila siku ilikuwa ntu kupata laki moja, laki moja na nusu, hata laki mbili. Anapata. Kwa sababu sasa yale makojoyo bei yake ni kubwa sana. Lakini hayapatikani kwa sababu mengi ntu haitafika hivihivi. Sijui zile zinapatikana kwa njia gani zile ges za kuweka mgongoni.

Ki AH M Unaona hizi sio utamaduni wetu. Sisi kabisa hatujui mambo haya. Haya tumeziona hapahapa tu. Sisi hatuna haja nazo.

Ma SA2 M Asante sana.

Ki AH M Haya, asanteni sana.

Ma SA2 M Mimi naitwa Saidi Salim Alawi. Ndio nilisikia ya wazazi wangu wa nyuma. Alisema kwamba humu baharini wengine tunakokwenda anatokea pweza pengine akakamata chombo, ili chombo isiweze kwenda. Lakini pweza huyo anasema sio kuliwa, ni kama ni shetani. Au pengine wakamwone mtu mleefu kabisa

kama atakacho hicho chombo wote wakiri wakapotea kwa ntu nleefu sana ndio wakawajia kiri, na... yule kiri imepita. Au pengine kwa bahati yao pengine mtu akawa ngonjwa, kutokana na miujizi unayoona hivi.

Ma SA2 M Haya yanatokea, na wakati mwingine wanasema tulivyosikia kwamba walikuwa watu wanaoumizwa sana na papa. Kuna papa anayeitwa mblani. Pengine akiona chombo, unaweza ukakiona chombo ukafikiri tanga limekwenda juu kabisa namna hii. Sasa chombo kile mpaka kufikia pengine akaweza kufanya ngalawa hata akapiga chombo na watu wakaweza kuzamia. Ni mambo ya zamani, lakini kwa siku hizi nafikiri hatujasikiliza bado. Haya yalikuwa watu wanatuambia wazazi wetu waliopitapita.

Ki AH M Lakini wewe mwenyewe hujawahi kukuta hayo?

Ma SA2 M Mimi sijawahi kumkuta.

Ki AH M Mwenyekiti, umesikia wewe?

Ma SW M Mimi nimesikia, sina nyongeza zaidi. Kama alivyozungumzia mzee huyu yanatosha.

Ma ST M Sisi hatuna zile.

Ma SA2 M Sasa wewe ungesikiliza zaidi mambo ya uvuvi sisi tulio. Mambo mawili yanayotutatiza haya: uvuvi na usafiri sisi... Matatizo makubwa.

Ma ST M Au wewe? Sisi uvuvi tunashindwa kwa vifaa vya... ikiwa... Mimi Salim bin Isa Tandika, wa kijiji hiki cha Msimbati. Kuvua ndio maisha yetu. Lakini kinachotushinda vyombo vya kuvulia. Kinachotushinda vyombo vya kuvulia, kuanza nyavu, mpaka na vyombo. Tunayo madao tu. Na kuvua wapo mafundi tu. Unasikia? Lakini vifaa hatuna. Na kama vifaa hatuna, hatuwezi sisi kuwa wavuvi barabara. Tunajua kuvua... elimu tunayo ya kuvulia, lakini hatuna nyavu. Elimu ya kuvulia tunayo, lakini hatuna nyavu. Tunapompata mtu wa kutupa vifaa tunaweza kuwa wavuvi, kwa sababu elimu ya kuvua tunayo. Anapokuja yeye yule mwenye kutoa vifaa akas.. mimi nitazidi kufundisha uvuvi njia utokanao kwetu nitamfundisheni ninyi. Iwe ni kama elimu nimesomesheni. Sisi tu tayari. Lakini tunashindwa. Hatuna vifaa.

Ki AH M Na ninyi hamjawahi kuwa na mradi wo wote kutokana na serik... kwa upande wa serikali kwa kusaidia uvuvi?

Ma ST M Yuko kijana mmoja. Yeye ni mvuvi. Anazo nyavu kama kumi za nailon. Lakini mshahaba yake ndogo, kwa sababu ana dao tu la kutweka.

Ki AH M Anakaa hapahapa?

Ma ST M Papa hapa. Yeye huenda kama ikiwa amepata nyavu, na kumwongeza taratibu za nguvu ya kuvulia, yeye anaweza kuwa mvuvi, na anaweza kuwa ni fundi wa Kiafrika/kiafiki.

Ki AH M Ndio. Sasa samaki wakianza kupatikana kwa wingi sana, tutafanyaje kwa zile... wale samaki? Si wataoza?

Ma ST M Tunao wachuluzi.

Ki AH M Yaani zinanunuliwa mara moja?

Ma ST M Mara moja tu. Na hawajapatikana bado samaki wa kushinda wachuluzi wa mji hii. Wanapatikana tu samaki ya kale/kali tu. Lakini hawawezi kushindwa ununuzi wa... Au labda nikutajie mvuvi huyu?

Ki AH M Ndio.

Ma ST M Huyu mvuvi Bakari Maaruf. Yeye anavua. Pana chombo chake anacho cha ki... cha tanga, sio chombo cha mashine.

Ma SA2 M Mimi naitwa Salum Saidi Alawi. Kutokana na uvuvi tulio nao, hawapatikani kisamaki wa kwetu kushindika bila kununuliwa. Lakini iwapo tunapata vifaa, vifaa vya kutosha, itabidi lazima tuwe na masanduku ya friji, lazima tuwe na nini... samaki, tunakuwa tuna... kwenda kuuza Ntwara, tunakwenda kuuza kwingine. Kama tukiwa na vifaa vya kutosha, hapa hawawezi kununulika samaki, kwa sababu wanakuwa wengi kabisa, ee. Tukisaidiwa tu vifaa vile vikubwa na masanduku ya friji ya kuweka.

Ki AH M Haya, tafadhali taja jina lako kwanza.

Ma LA M Lyachefu Aleda.

Ki AH M Na ulizaliwa wapi?

Ma LA M Ntambo li Makonde, Msumbiji.

Ki AH M Ulikaakaa huko kwa muda mrefu, au?

(inaendelea kwa Kimakonde)

Ma PS M Mimi naitwa Pita Sikota, mzaliwa wa Msumbiji.

Ki AH M Eneo gani huko Msumbiji?

Ma PS M Eneo la Msumbiji?

Ki AH M Ndio, yaani pwani pwani au?

Ma PS M Pwani pwani, Nsimbo, Ntamba.

Ki AH M Ndio.

Ma PS M Sehemu ya Ntamba, sehemu ya pwani pwani. Ndio niliyozaliwa mimi, kutoka Msumbiji kuja huku. Huku nilikuja ukati wa ukoloni wa Manamba. Nilikuja ukati wa Manamba. Umanamba. Wanawasomba watu Msumbiji, Tanga, mpaka Moshi, mpaka Arusha. Ndio ukati niliyokuja mimi huku. Ukati wa kikoloni.

Ki AH M Ndio, sawasawa.

Ma PS M Ukati wa Manamba, Manamba. Wanakata katani. Ndio niliyokuja mimi. Niko kijana.

Ki AH M Ulikuja kufanya kazi ile ya kukatia katani?

Ma PS M Ee, nilikuja kukata ile katani ile, ukati wa zamani.

Ki AH M Kwenye mashamba yale makubwa yaliyo pale kati ya... kati ya miji ile?

Ma PS M Ee, kuanzia, baada ya kutoka Msumbiji nimefikia Moshi, Kilimanjaro.

Ki AH M Ooh kweli umesafiri nchi nzima?

Ma PS M Ee, kwenda kukata katani.

Ki AH M Ndio.

Ma PS M Sasa nimerudi kule mwaka sabini na saba kufika nchi hii. Kuludi sasa na kwenda kwetu. Sasa kwetu sikwenda. Nimekwama kwa hukuhuku tena. Ee.

Ki AH M Na hapo umekaa muda gani?

Ma PS M Hapa baada ya kuja mwaka sabini na saba, nilihesabu mwaka sabini na saba niliyokuja nchi hii wa hapa Msimbati, mpaka wa leo. Sijui miaka mingapi, nimesahau katikati hapo.

Ki AH M Kama kumi na tatu.

Ma PS M Ee, ee.

Ki AH M Na kazi unayofanya sasa ni nini?

Ma PS M Sasa hapa Msimbati nafanya kazi kulima tu. Kulima.

Ki AH M Samaki, je?

Ma PS M Iih, sijui. Kuvua sijui, bahari wenyewe huku, nikitumbukizwa kwenye bahari nakuwa kama jiwe.

Ki AH M Haya, afadhali usiende.

Ma PS M Ee, nakuwa kama jiwe. Lakini kazi yangu kulima, kupanda mtama, mihogo, mihindi, matangwe yo yote tu, chakula cho chote, basi. Na... nakuja nazo sokoni, napata senti kutumia, na bibi yangu na watoto wangu, basi.

Ki AH M Ndio, haya. Na sijui kama unaweza kueleza kidogo kuhusu Kiswahili cha huko, maana bila shaka umewahi kwenda huko Msumbiji ukikaa hapa.

Ma PS M Nimezaliwa hukohuko.

Ki AH M Lakini hata wakati ukikaa sasa hapa, unakwenda huko mara kwa mara, sio?

Ma PS M Mwanzo wa kuludi niliyotoka Moshi mpaka hapa sijakwenda.

Ki AH M Hujaenda.

Ma PS M Wanakuja wandugundugu kuniangalia hapahapa. Ee.

Ki AH M Kwa nini hujaenda?

Ma PS M Aa-a. Siludi sasa, uzito wa uzee. Unajua mzee ukiwa u kijana miguu inakuwa myepesi. Sasa ukienda kufika pa zee, basi kila kitu unakuja kwa uzee tu. Uzito.

Ki AH M Lakini hali ya Kiswahili, kuna watu wanaojua Kiswahili upande wa Msumbiji?

Ma PS M Hali ya Kiswahili ya Msumbiji ndio kama niliyosema. Kuna kilugha za kutumia. Kila ntu anatumia kulekule pao. Sio ya kutembea naye. Sasa sisi tunatumia lugha ya palepale kwetu, sehemu ya kwetu, tuliokuwa sisi Wamakonde watupu. Tunatumia kilugha cha kwetu, kama alivyosema bwana. Ee, tunatumia kilugha kilekile. Sasa hii kilugha ya Kiswahili ndio kama tuliokuja huku. Maana yake kutoka miaka hii ya sasa ndio tuna... tunadokoo kidogokidogo, kwa Kiswahili.

Ki AH M Maana yake ng'ambo ya mto, huko. Hawatumii kabisa Kiswahili?

Ma PS M Aa-a. Wanatumia cha kulekule kama ya mto kinatumia kilugha kingine tena, ee, Kimwani. Kiswahili ndio hapahapa tunaopatia waliotoka kule wakija huku.

Ki AH M Sawa, haya. Na wakati ulipokuwa huko Arusha, sehemu za Arusha, ulitumia Kiswahili vilevile bila shaka?

Ma PS M Ee, hichi Kiswahili tu. Na kilugha cha kinyumbani tunakutana ukati tukirudi kazini tunaweka, tunakuwa pale kwenye manyumba yetu, na bibi zetu na wazee wetu. Tunaongea kilugha hiki kya Kiswahili, ee.

(proofread 19.11. 1990)

Proofread by MY

Edited by TR, November 1996

DAHE 112

Place: Mtwara, Majengo

Time: 12.10.1990

Interviewee(s): 1. (DN), 2. (SM4), 3. (SA1), 4. (MM4), 5. (MB2), 6. Anonyme (XX), (X1), (X2) etc.

Interviewer(s): David Massamba (DM)

Recorder: Sony Professional

Language: Standard Swahili (Ki), Kimalaba (La)

Topic: 1. Short history of DN, SM, SA1 and MM, 2. Different Swahili dialects, 3. A list of Kimaraba words with explanations

Ki DM M Naam, mzee, unaitwa nani?

La DN M Mimi Dismas Nalinga. Mzaliwa wa Newala Mmakonde.

Ki DM M Unafikiri una umri gani mzee?

La DN M Miaka sabini na moja.

Ki DM M Miaka sabini na moja.

La DN M Ndiyo.

Ki DM M Umekulia Newala au umekulia Mtwara?

La DN M Nimefika Mtwara mwaka na arobaini na tisa.

Ki DM M Toka wakati huo uko hapa hapa?

La DN M Toka wakati huo niko hapa hapa. Mpaka hivi leo.

Ki DM M Asante sana. Mzee, unaitwa nani?

La SM4 M Mimi Saidi Mbaya.

Ki DM M Saidi...

La SM4 M Saidi Mbaya.

Ki DM M Mh. Umezaliwa wapi?

La SM4 M Mzaliwa mimi kuzaliwa na nimezaliwa Malawi.

Ki DM M Malawi.

La SM4 M Lakini kuishi nimeishi hapa sana. Nimekuja kijana.

Ki DM M Ndio.

La SM4 M Ehe, katika tarehe hizo ulizosema, unasikia, mimi nimekuja hapa kwa ishirini na nane. Kuingia hapa. Basi, sizarudi tena. Nalikwenda mara moja kwa livu kuja hapa, lakini makazi yangu ni hapa ya Malawi siyajui, ninayoyajua ni ya humu.

Ki DM M Sawa. Humu wapi? Hapahapa Mtwara au sehemu nyingine?

La SM4 M A'a. Hapa hapa Mtwara kwa hapa Tanzania.

Ki DM M Ahaa.

La SM4 M Maana yake, Dar es Salaam nimekaa miaka kumi na sita.

Ki DM M Ahaa.

La SM4 M Sio mpaka imeanza hii, ile vita ya nanii- Hitler, niko Dar es Salaam, nikaondoka mimi kwenda nanii - Misri.

Ki DM M Ndiyo.

La SM4 M Mm. Sasa, kurudi kwa huko moja kwa moja, na yule nzungu kuja hapa. Nilipokuja hapa ndiyo sijatoka tena...

Ki DM M Hapa Mtwara.

La SM4 M Hapa. Nimekuja hapa Mtwara yaani ni hamsini na mbili.

Ki DM M Ahaa.

La SM4 M Ee, inanza gati hii, yaani kufunguliwa. Nipo.

Ki DM M Naam, shukrani. Na mzee, unaitwa nani?

La SA1 M Mimi Saidi Abdallah Mponda, mzaliwa wa Sudi, Tarafa ya Lindi.

Ki DM M Ehee. Naam, Umekulia Lindi au?

La SA1 M Mimi, nimekulia Sudi, nimesoma Sudi, Kurani. Nimechezwa Sudi...

Ki DM M Naam.

La SA1 M Jando.

Ki DM M Naam.

La SA1 M Nimetoka pale, nikenda zangu Lindi.

Ki DM M Naam.

La SA1 M Kupata maarifa ya elimu ya akhera, unasikia?

Ki DM M Sawa.

La SA1 M Nilipotoka pale, pale Lindi, nikajifunza kushona cherehani. Baada ya kujifunza kushona cherehani nikashona pale, nikatoka mwaka hamsini. Kuja hapa. Mtwara. Hapa Mtwara nimekuja na hamsini na

hamsini na mbili, nimeondoka nimekwenda Dar es Salaam. Kwenda kufanya kazi zangu za kushona. Nilirudi Dar es Salaam. Mwaka sitini, mwezi wa tano nimekuja hapa Mtwara. Katika kuja hapa sijaondoka tena, kwenda pahali po pote. Nipo hapa Mtwara.

Ki DM M Umri?

La SA1 M Na umri wangu ni miaka sitini na tatu.

Ki DM M Miaka sitini na tatu, ee. Mzee, unaitwa nani?

La MM4 M Mimi naitwa Masudi Abdillahi Mtondoima.

Ki DM M Masudi Abdillahi Mtondoima?

La MM4 M Mtondoima.

Ki DM M Umezaliwa wapi?

La MM4 M Nimezaliwa katika kijiji cha ujamaa Kilambo.

Ki DM M Kilambo.

La Mwaka elfu moja na tisa na sitini na tano.

Ki DM M Mh.

La MM4 M Nilisoma shule ya msingi pale Tangazo, nikamalizia elimu yangu ya msingi mwaka themanini na nne. Basi toka hapo, nimetoka Kilambo, nipo hapa Mtwara.

Ki DM M Mh.

La MM4 M Umri wangu ni kama miaka ishirini na nne.

Ki DM M Kwani Kilambo ni wapi?

La MM4 M Kilambo, ni kando kando ya mkoa wa Mtwara, ambapo ni mpakani sana na Msumbiji. Kwa kutoka hapa kama kilomita thelathini hivi, unaelekea upande wa kusini mwa Tanzania. Kwa hiyo huko kijiji cha Kirambo wastani ni kwamba... ukishafika Kilambo, kuendelea mbele ni kwamba ni Msumbiji.

Ki DM M Msumbiji.

La MM4 M Ee, ni mpakani kabisa.

Ki DM M Wewe ni Mmakonde au?

La MM4 M Mimi ni Mmakonde.

Ki DM M Mmakonde.

La MM4 M Ndiyo.

Ki DM M Na mzee samahani, sikukuuliza wewe ni?

La MB2 M Mimi ni Mmaraba.

Ki DM M Mmaraba?

La MB2 M Ee, Maraba. Imechimbuka katika umakonde.

(interruption)

Ki DM M Mzee umeniambia kuwa wewe ni Mmaraba.

La MB2 M Mm.

Ki DM M Ni Mmalaba au Mmaraba?

La MB2 M Mmaraba.

Ki DM M Mmaraba?

La MB2 M Mmaraba.

Ki DM M Sio Mmalaba?

La MB2 M A'a, Mmaraba.

Ki DM M Ee, Kimaraba ni Kiswahili?

La MB2 M Si Kiswahili.

Ki DM M Si Kiswahili?

La MB2 M Si Kiswahili.

Ki DM M Ehee.

La MB2 M Ni-- ni-- ni-- lugha kutokana na Mmakonde...

Ki DM M Ahaa.

La MB2 M Si Kiswahili, ni lugha kutokana na Mmakonde, kimechujwachujwa katika umakonde.

Ki DM M Ahaa.

La MB2 M Mmakonde yuko-- anazungumza kindani kabisa. Mmaraba anazungumza idh-hadi, yaani kinachosikikasikika, kinakwenda kinakwenda kinakwenda kinaungana na Kiswahili.

Ki DM M Mh.

La MB2 M Kinakwenda kinakwenda, kinaungana na Kiswahili, hakiko mbali na Kiswahili. Anapojifunza Kiswahili mara anapata.

Ki DM M Sawa. Kwa hivyo, inawezekana kwamba-- kwa hakika Kiswahili na Kimaraba ni lugha mbili tofauti, lakini zimeathiriana?

La MB2 M Zimeathiriana.

Ki DM M Hivyo ndivyo?

La MB2 M Ndivyo, kwa sababu Kiswahili na Kimaraba mbalimbali, sio Kiswahili ndio Kimaraba, au Kimaraba ndio Kiswahili sio hivyo ni juavyo mimi.

Ki DM M Sawa. Je, wanaozungumza Kiswahili huku sehemu za mwambao huu, wanazungumza namna gani?

La MB2 M Ee?

Ki DM M Wanazungumza za Kiswahili cha namna gani, maana kuna Kiswahili vya aina mbalimbali.

La MB2 M Kama kipi?

Ki DM M Kuna... ukienda kwa mfano Mombasa, wanazungumza kimvita...

La MB2 M Mh?

Ki DM M Ukienda Tanga, wanazungumza Kimtang'ata.

La MB2 M Mh.

Ki DM M Na kama hivyo. Hapa, mnazungumza Kiswahili cha namna gani?

La MB2 M Tunazungumza Kiswahili. Hilo swali limekuwa gumu kidogo.

Ki DM M Limekuwa gumu?

La MB2 M Mm, hilo swali limekuwa gumu, kwa sababu mtu wa Mombasa, anasema "heve", mimi nasema: "Hewe!" - "Heve!" Anastaajabu: "Heve?" Ee. Na sisi waswahili tunasema "ala", ee.

Ki DM M Nimewahi kusikia watu-- baadhi ya watu wakisema kwamba kuna Kiswahili kinachoitwa Kimgao. Wewe, umewahi kusikia kitu cha namna hiyo?

La MB2 M Mimi, hapo Sudi na Mgao ni pamoja.

Ki DM M Ahaa Sudi na Mgao ni pamoja?

La MB2 M Sudi na Mgao, Sudi imekaa huku ninii, halafu unavuka unakwenda Mgao.

Ki DM M Ahaa.

La MB2 M Ee, unatoka Sudi unavukia Mgao.

Ki DM M Ahaa.

La MB2 M Ee. Kwa hichi hichi ninachozungumza ni Kimgao.

Ki DM M Ni Kimgao?

La MB2 M Ee, ni Kiswahili cha Mgao. Lakini wale wa Mgao na wa Sudi Wamaraba. Lakini Kiswahili...

Ki DM M Wanakitumia?

La MB2 M Wanakitumia. Mwanamke anazungumza Kimaraba, mwanamme anazungumza Kiswahili, lakini wanaelewana.

Ki DM M Ahaa.

La MB2 M Anaweza kusema: "ida, wewe ukaenda", amezungumza mwanamke: "ida, wewe ukaenda". Unaweza kumwambia unaweza kutoka wewe mwanamme: "Njoo bibi!" Akaja. Lakini hasemi akizungumza "njoo bibi", yeye anasema: "nilikwida".

Ki DM M "Nilinkwida"?

La MB2 M Nilinkwida. Nilinkwida hambihambi.

Ki DM M Ehee. Yaani, wewe unamsemesha Kiswahili anakujibu Kimakonde, Kimaraba?

La MB2 M Ee, Kimaraba. Unaelewa hivyo?

Ki DM M Ee, sawa sawa.

La MB2 M Hata ukimwita mtoto: "we, Abdallah nani, njoo", anaweza akakujibu hivi: "nilinkwida wawa".

Ki DM M Na "wawa" ndio?

La MB2 M Baba.

Ki DM M Ahaa

La MB2 M Ee.

Ki DM M Lakini anapokuwa anajibu hivyo, sasa ni Kimaraba?

La MB2 M Ee, ni Kimaraba. Lakini amesikia...

Ki DM M Kiswahili?

La MB2 M Kiswahili.

Ki DM M Ahaa.

La MB2 M Ee unanielewa hivyo?

Ki DM M Sawa sawa. Na hiki Kingao, kinatofautiana vipi na lugha inayotumiwa kwa mfano Dar es Salaam au Unguja?

La MB2 M Utasikiliza, utasikiliza utelezitelezi wake.

Ki DM M Ehe?

La MB2 M Utaupata utelezitelezi wake. Sasa mtu wa Unguja, na mtu wa Dar es Salaam, utasikia tofauti utaona tofauti ukisikiliza.

Ki DM M Sawa.

La MB2 M Lakini wanaelewana.

Ki DM M Ndiyo.

La MB2 M Ee? Mtu wa Unguja na mtu wa Dar es Salaam wanaelewana, mtu wa Dar es Salaam na mtu wa Mgao wanaelewana. Unanipata hiyo?

Ki DM M Nakupata.

La MB2 M Ee. Sasa wewe na mimi tunaelewana kama Kingao kinafuatana kidogo.

Ki DM M Mh.

La MB2 M Kwa sababu hakina utelezi.

Ki DM M Hakina utelezi.

La MB2 M Hakina utelezi, ee. Hakina utelezi.

(interruption)

Ki DM M Unasemaje?

La MB2 M Nilivyotaka kusema ni kwamba utelezi...

Ki DM M Kuhusu nini hasa?

La MB2 M Kuhusu tofauti ya Kiswahili kinavyozungumzwa.

Ki DM M Ehe?

La MB2 M Tofauti kubwa inayotofautisha ni erufi za matamko...

Ki DM M Mh?

La MB2 M Kwa sababu Mswahili wa huku kusini.

Ki DM M Mm.

La MB2 M Sisi tulie na jamii ya Kimalaba na Wamakonde, ni kwamba tunapozungumza, sana neno "m", tunaliachia, tunalitamka "n".

Ki DM M Mh.

La MB2 M Kwa mfano, kama tunataka kuzungumza "mtu", tunaitwa "ntu".

Ki DM M Mh.

La MB2 M Tunataka kusema "mchele", wengi wetu wanasema "nchele".

Ki DM M Sawa sawa. Naam, tuendele. Labda-- tukitaka kurahisisha mambo tuanze kwa kuulizana maswali kuhusu mambo yanayohusiana na lugha. Majina, kwa mfano. Tukianza na sehemu za mwili, mmeanza kunitajia sehemu mbalimbali za katika Kiswahili cha huku.

La MB2 M Kichwa.

Ki DM M Kichwa.

La MB2 M Ni kichwa.

Ki DM M Ndiyo endelea na sehemu zingine.

La MB2 M Sasa unataka.

La XX M Yaani mwili mzima utaje

Ki DM M Naam.

La MB2 M Ehe, mdomo.

Ki DM M Ndiyo.

La MB2 M Pua.

Ki DM M Ndiyo.

La MB2 M Macho.

Ki DM M Mmm.

La MB2 M Sikio.

Ki DM M Mmm.

La MB2 M Mkono.

Ki DM M Mm.

La MB2 M Kidole.

Ki DM M Mm.

La MB2 M Miguu.

Ki DM M Naam.

La MB2 M Tumbo.

Ki DM M Mnasema mkono au mukono?

La MB2 M Mkono.

Ki DM M Mkono?

La MB2 M Mkono.

Ki DM M Tena.

La MB2 M Mkono.

Ki DM M Ehe.

La MB2 M Mguu, sikio.

Ki DM M Sawa.

La MB2 M Tumbo, pua, jicho, ulimi, meno, jino.

Ki DM M Sawa.

La MB2 M Ehe.

Ki DM M Mengine mzee wewe?

La MB2 M Unasikia? Ehe, kiganja cha mkono.

Ki DM M Eee.

La MB2 M Kiganja cha mkono.

Ki DM M Ehe kuna kiganja kingine cha nini?

La MB2 M Cha mguu.

Ki DM M Cha mguu?

La MB2 M Ee.

Ki DM M Hicho mnaita kiganja vilevile?

La MB2 M Ehe, unyayo.

Ki DM M Unyayo?

La MB2 M Ee, unyayo.

Ki DM M Lakini mnasema kiganja cha mguu?

La MB2 M Ah, ah.

Ki DM M Ee?

La MB2 M Kiganja mikono, unyayo wa mguu. Kisigino cha mguu, kisigino cha mkono.

Ki DM M Aa cha mkono pia kisigino?

La MB2 M Hiki ni kisigino.

Ki DM M Mhm.

La MB2 M Na hiki kisigino.

Ki DM M Ndiyo.

La MB2 M Ee.

Ki DM M Sawa. Na ndani ya tumbo kuna nini? Mzee naam. Ndani ya tumbo kuna nini?

La MB2 M Kuna utumbo.

La XX M Kuna utumbo.

Ki DM M Ehe kuna utumbo?

La XX M Kuna utumbo.

Ki DM M Na nini tena?

La XX M Ee baada ya utumbo na moyo.

Ki DM M Ehe.

La XX M Ehe.

La X1 M Endelea.

La XX M Sasa hapo tena kaka katika hapo ndio sielewi tena ya katika utumbo maana yake nimesema tumbo.

Ki DM M Mhm.

La XX M Na moyo.

Ki DM M Naam.

La MB2 M Kuna utumbo, kuna moyo, kuna maini, kuna mapafu, kuna figo kuna bandama, sasa na vilivyoko vingine hivyo anavijua daktari. (kicheko)

Ki DM M Sawasawa, sawasawa, sawasawa. Hii sehemu mnaitaje hii?

La MB2 M Hii?

Ki DM M Ehe.

La MB2 M Goti.

Ki DM M Goti? Na hiki kichubwana kilichoko hapa kama kijisahanisahani kijiwejiwe hiki, mna neno lolote mnalotumia ku...ee? Hapana?

La XX M Hapana.

Ki DM M Sawa

